# Wise as a Serpent, Gentle as a Dove

## Surviving as a Sheep in the Midst of Wolves

**TAFSIRI YA KISWAHILI**

*"From a sheeple to a sheep. The road from the false, tolerant love of the world to the tough, true love of God."*



*James Joseph Miller, Jr.*

# Hekima kama ya Nyoka, Mpole kama Njiwa

## Kuishi kama Kondoo kati ya Mbwa-mwitu

*"Kutoka maisha ya kuwa kama kondoo na kuwa kondoo. Barabara ya kutoka kwenye upendo wa uwongo na uvumiliano wa dunia hadi kwenye upendo mgumu na wa kweli wa Mungu."*

na

James Joseph Miller, Jr.

Hakimiliki © 2018 James Joseph Miller, Jr

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki au sehemu yoyote yake haiwezi kutolewa tena au kutumiwa kwa namna yoyote ile bila ruhusa ya kuandikwa ya mchapishaji isipokuwa kwa matumizi ya nukuu fupi katika hakiki ya kitabu.

Kimechapishwa na DiggyPOD, Inc., nchini Marekani.
Uchapishaji wa kwanza, 2018.

www.GlobalMissionForChildren.org

**YALIYOMO:**

**Utangulizi:** Kabla – Wakati wa – Baada

**Sura ya 1:** Kanisa

**Sura ya 2:** Kufungwa Nira na Familia na Marafiki

**Sura ya 3:** Kufungwa Nira na Adui wa Mungu

**Sura ya 4:** "Usihukumu"

**Sura ya 5:** Kupokea Upendo au Chuki ya Mungu Kunakutegemea Wewe

**Sura ya 6:** Toba ya Kibiblia

**Sura ya 7:** Kuteseka au "Maisha Bora Sasa Hivi"?

**Sura ya 8:** Je, Ni Lazima Niishe kwa Utakatifu na Ukamilifu?

**Sura ya 9:** Dhambi ya Kaburini ya Kutotenda

**Sura ya 10:** Mwenye Rehema na Kuridhiana Sana

**Sura ya 11:** Yesu hakuwa Rafiki wa Watenda Dhambi

**Sura ya 12:** Kuanguka Kutoka kwa Neema

**Sura ya 13:** Je, Wewe ni Mfuasi?

**Sura ya 14:** Njia ya Msalaba

# UTANGULIZI: KABLA – WAKATI WA – BAADA

Ninapoanza, ninataka kwanza kutoa utukufu wote kwa Yesu, Bwana na Mwokozi wangu. Tafadhali fahamu kuwa ninatumia “HERUFI KUBWA” kusisitiza maneno au mawazo, ila sio kupasa sauti.

**“KABLA”**

- Kokeini ya dola 4,000 mapuani mwangu
- Vinywaji vya pombe 800
- Mamia ya vidonge vya maumivu
- Madawa haramu (SSRI's) prozac, lithi, risperidone, abilify, ritalin, paxil, zoloft, wellbutrin, n.k.
- Malipo ya nyumba na gari ya dola 12,000
- Makumi ya maelfu niliyotumia kula mahotelini, kwenye baa, kwenda likizo, kucheza kamari, “kupenda” marafiki zangu, n.k.

Hapo juu ni mfano wa matumizi ya mwezi mmoja katika maisha yangu kama pagani (kabla ya wakati nilipoamua kwa kweli kutubu: kumgeukia Kristo katika huzuni ya kimungu na kuachana na dhambi zangu zote). Nilikuwa napata makumi ya maelfu kila mwezi kama mwanabiashara wa “kutegemea jitihada zake mwenyewe” na kutumia maelfu na maelfu zaidi ya mapato yale. Dola 110,000 katika malipo ya kadi za mkopo, malipo ya rehani ya dola 575, tingatinga la kuchimba aina ya Kubota, magari 6 pamoja na gari la kipekee la Hummer HI

lenye pua lililoinama, pikipiki ya kipekee, jeti ya baharini, n.k. zote zilizokaa kwenye barabara ya nyumbani kwangu. Nilikuwa ninaishi maisha ya "Ndoto ya Mmarekani"!

Baada ya miaka mingi ya kutia bidii ili nijenge biashara yangu ya mawasilianoanga, nilikuwa najiona "nishafika" jinsi pesa zilivyomiminwa. Nilipiga gumzo za "kidunia" na kufikiri nilikuwa nishafanikiwa. Hii ilikuwa hadi maisha yangu ya kutomwamini Mungu yalipoanza kuniandama. Nilikuwa rafiki wa dunia na "walinipenda"! Nilikuwa mlevi, mraibu wa dawa za kulevya, msherati, mchezaji wa Kamari, aliyewashawishi wengine kuvuta dawa za kulevya, mwenye tamaa, mpenda pesa, mwabudu sanamu (michezo na zinginezo), mdharau wa mamlaka, mwongo, na nilifanya dhambi zingine zote ambazo unaweza kuzifikiri, Nilikuwa "stadi" wa zote. Sitaingia kwenye maelezo ya ndani kwani hilo silo lengo la kitabu hiki lakini nilitaka kukuchorea picha ya maisha yangu ya "kabla" ili nikupe matumaini unapoendelea kusoma kuhusu Neema ya kimiujiza ya Mungu.

Lengo langu la kukiandika kitabu hiki, na niamini hili ndilo lililokuwa wazo la mbali zaidi akilini mwangu ila kaka mmoja mpendwa akanihimiza nikiandike, ni kufungua macho ya "Wanaojidai kuwa Wakristo" wanaoamini kuwa wataingia Mbinguni kwa kupitia mlango wa mbele kwa sababu "wanamwamini Yesu". Nitahakiki kwa kutumia Biblia, bila wasiwasi wowote, kuwa "kuamini" si kile ambacho asilimia 99 na zaidi ya wanaojidai kuwa Wakristo wanachokifanya leo. Ninaomba kuwa waliopotea watampata Yesu kwa kweli na na

nina matumaini kuwa kitakuwa kifungua-macho si tu kwa waliodanganywa mbali pia kwa wanaotafuta.

Baada ya zaidi miongo miwili ya "utu-uzima", maisha yangu yakaendelea kujipinda chini na nilikuwa nimezama kwenye dhambi kadri ya uwezo wangu. Ningekaa macho kwa siku nne hadi tano mfululizo kwa matumizi ya kokeini, pombe na matumizi ya madawa yalikuwa ni kanuni, si kwa uchaguzi tena. Unaona, shetani anajua hasaa jinsi ya kubonyeza vitufe vya mtu mradi umkubalishe (uridhiane), hata kwa kiasi kidogo tu. Kile kinywaji "kimoja au viwili" vya kikawaida tu kwenye baa kinageuka kinywaji cha dakika 30 kila siku baada ya miaka kadhaa. Mstari wa kwanza tu "uliouhitaji" wikendi unabadilika kwa haraka kuwa mazoea ya mistari 100 kila wikendi na kisha mamia ya mistari unayotumia siku 4 au 5 kila wiki. Katika upeo wa utendaji dhambi wangu, nikapatwa na ugonjwa wa kichwamaji wa schizophrenia uliosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya na sikuweza kukumbuka nilichokuwa nimefanya katika siku zilizopita. Kwa kweli ilikuwa "kuzimu duniani"!

Nilipaswa kuuza kampuni ya mawasilianoanga niliyokuwa nimetengeneza tangu mwaka wa 2000 hadi 2004 na ingetengeneza mamilioni.  Shughuli hii ilifeli katikati wa mwaka wa 2004 kwa sababu mshiriki mmoja wa biashara alidaiwa na serikali na kampuni za kibinafsi mamilioni ya madola. Hilililiniathiri sana kwani nilikuwa na uhusiano wa karibu na mwanamume huyu na nilidhani kuwa alikuwa mkweli na aliyefanikiwa sana. Iligeuka alikuwa mtenda

dhambi mwingine tu ambaye hangeaminiwa. Mapato yangu wakati ule yalishuka kutoka dola 60,000 kila mwezi hadi takriban dola 12,000. Yanaonekana kuwa "mapato" mazuri sana lakini kumbuka nilikuwa nadaiwa zaidi ya dola 12,000 malipo ya kila mwezi. Hili kwa kweli lilinirusha kwenye ulevi wa zaidi ya mwaka mmoja na nusu ambao ungeshinda ule wa wanamuziki mashuhuri wa roki. Pia niliacha kulipa nyingi ya bili zangu na kampuni ya ununuzi tena ikachukua magari yangu yote ila moja na matumizi ya kokeini na pombe yalikuwa yamepita mipaka. Nilikuwa nimefika mahali ambapo nilikuwa nawapa walanguzi wa dawa za kulevya vito nilivyomiliki kama malipo kwani mazoea yangu wakati ule yalikuwa yananigharimu zaidi ya dola 10,000 kila mwezi! Sikuwahi kuhubiriwa au kupendwa upendo wa kweli (kukemewa) na Mkristo yeyote, hata wakati mmoja! Biblia inasema; ***Walawi 19:17 "Usimchukie ndugu yako moyoni mwako. Karipia jirani yako kwa uwazi ili usishiriki hatia yake."*** Nilipatana na maelfu ya watu katika maisha yangu kwenye biashara, nikisafiri ulimwenguni, n.k. na sikuhubiriwa kuhusu Kristo hata mara moja! Hakuna hata MARA MOJA ambayo NILIPENDWA kwa kweli!

**"WAKATI WA"**

Mnamo Januari 2006, nilidaiwa na mwanamume mmoja aliyekuwa akiiosha nyumba yangu pesa fulani. Sikuwahi kuzungumza na mwanamume huyu mazungumzo ya kina ila mazungumzo ya juujuu tu (habari, unaendeleaje, n.k.); tukipitana tu kwani nilimwajiri awe akisafisha ofisi na nyumba

yangu. Alikuja nyumbani kwangu asubuhi moja kuosha na nilikuwa sijamlipa kiasi fulani cha pesa. Sikuwa na pesa na nilikuwa nimempa mhasibu wangu kitabu changu cha cheki ili nisiandike cheki mara nyingi sana. Nilijua nilikuwa kwenye shida kuu. Nikamwambia tupatane kwenye mgahawa uliokuwa umbali wa takriban dakika thelathini baada yake na wafanyakazi wake wamemaliza na tungeenda sote kuichukua cheki yake. Hii ilikuwa mojawapo wa siku nadra ambazo sikuwa nimelewa. Ningechukua siku moja ya "kutokunywa" kila wiki kwani siku nyingi nilikuwa kwenye hatua ya kuporomoka.

Alikubali na tukapatana baada ya muda usiokuwa mrefu. Niliingia garini mwake na ghafla nikaanza kumlilia BWANA! Nilikuwa ninalia kama mtoto huku nikisema kuwa nilikuwa nimechoka na maisha ya dhambi niliyokuwa nikiyaishi, jinsi ambayo sikuwa na marafiki wa kweli na nilikuwa natumiwa tu kwa sababu ya pesa zangu, n.k. kwa kweli nilikuwa na "marafiki" mia, lakini hakuna yeyote aliyekuwa wa kweli. Mkristo wa kweli na mtiifu ndiye tu anayeweza kuwa rafiki mwaminifu na wa kweli. Tukaenda ofisini ya mhasibu wangu iliyokuwa umbali wa takriban dakika 15, tukachukua cheki na tukarudi nyumbani kwangu. Kwa masaa machache yaliyofuata nilikiri dhambi zangu zote kisha nikalala. La msingi, niliokoka kimiujiza tarehe 16, Januari mwaka wa 2006!

Niliamka asubuhi iliyofuata baada ya usingizi mzito ambao sikuwa nimeupata kwa miaka mingi na kupata takriban karatasi 22, 8 na ½ x 11 zikisema "Yesu ananipenda" na "Nina

rafiki wa kweli katika Yesu", n.k. Nilipatwa na mchanganyiko wa hisia niliposoma haya. Nilifikiri kwa upande mmoja "Nina kinyangarika wa Yesu mkononi mwangu hapa" na upande mwingine, nilihisi uzito mkubwa umeondolewa juu yangu. Mojawapo ya barua hizi ilisema nimpigie msafishaji kwa hivyo nikafanya hivyo. Nilikuja kujua aliniambia yeye ni "mchungaji" na nikakubali aje nyumbani kwangu kama alivyokuwa amependekeza wakiwa na "rafiki" yake ambaye alikuwa mwanamke. Waliniletea chakula na sinema inayoitwa "The Passion". Kwa wakati ule sikujua kuwa sinema hiyo haikuwa ya Mungu lakini ilieleza wazo hata hivyo. Waliondoka masaa machache baadaye na nikakubali kukutana nao nyumbani kwao kwa muda wa takriban dakika 30 kila siku na kuhudhuria "kanisa" yao. Niliishia kufanya hivi na baada ya muda, nikahama na kuanza kuishi naye ili kuliondokea eneo nililokuwa ninaishi nipate mwanzo mpya.

Sababu iliyonifanya niite sehemu hii "wakati wa" ni kwa sababu, nikitazama nyuma, huu ulikuwa mojawapo wa wakati wenye kufurahisha na kuhuzunisha maishani mwangu. Kwa upande mmoja, nilikuwa nimeokoka na namfuata Yesu, kwa upande mwingine, wacha nieleze hili kwani hapa ndipo wengi wenu mlipo; mmedanganywa, "mnaamini" kuwa mtaingia Mbinguni katika hali yenu ya sasa ya "kuamini" ilhali bado mnang'ang'ana na dhambi".

Shida ilikuwa walikuwa "Wapentekosti" wenye kupotosha kwa ulimi (yaani wenye haiba) lakini sikujua bora zaidi. Niliishi huko kwa miezi na sikuwahi kuwasikia wakihubiri toba ya

dhambi, kuishi kwa utakatifu, n.k. Pia HAWAKUWAHI shiriki imani yao barabarani, hadharani, n.k. Ilikuwa ni uzoefu wa kawaida tu wa "Kanisa Kuu" ambao zaidi ya asilimia 99 yenu wanaishi leo. Enda kwenye jumba linaloitwa "kanisa", fanya mambo ya "kikanisa" kama kuhudhuria mkutano wa maombi ya usiku ya Jumatano, n.k. lakini hawakuwahi kuenda NJE kuhubiri. Nilishuhudia maovu mengi sana ambayo sitazungumzia kuhusu kwa wakati huu lakini ninazungumza kuhusu kila kitu kutoka kudanganyana hadi maovu yanayoonekana kuwa mabaya zaidi. Haikunichukua muda mrefu katika mazingira haya kuanguka kutoka kwenye imani.

Nikiwa bado ninaishi katika nyumba ya "mchungaji" huyu, nilipatana na rafiki wa zamani kwenye mgahawa/baa aliyenisalimia. Alikuwa ni rafiki wa utotoni ambaye hatukuwa tumeonana kwa miaka mingi sana. Nilidhani kuwa nilikuwa ninaweza kujidhibiti. Ningeweza kwenda na niketi kwenye baa na nikunywe "kinywaji kimoja au viwili". Kukubalisha hamira hiyo kidogo kulinipelekea vinywaji 20 vya pombe na shetani akarudi ndani yangu. Haikuchukua muda mrefu na nikarudia kuwa nakunywa mara kadhaa kila wiki; na ikaendelea kwa miaka sita kamili (hadi 2012). Wakati ule niliamini kwa kweli kuwa nilikuwa nimeokoka na nitaenda mbinguni. Kila mara niliambiwa kuwa "ninaendelea kuwa bora", sikuwa mwanamume ambaye nilikuwa kitambo; wakasema kuwa "ninaelekea kufikia ukamilifu" (uongo mbaya wa utakaso endelevu ambapo wanahubiri kuwa mtu anaweza kuwa ndani ya dhambi kwa hiari na bado afike mbinguni). Huwezi kuwa "Mkristo mlevi", huwezi kuwa "Mkristo shoga", huwezi kuwa

“Mkristo anayefanya uasherati”, n.k. Dhambi hizi zote, na zaidi, zinatuongoza kwenye moto wa mateso wa milele.

Mifano mingine michache ya uongo unaozungumzwa ni “hakuna anayekuzuia kutenda dhambi kabisa na hatutakuwa wakamilifu hadi tu tufike mbinguni”. Walisema “Jimmy, hutumii dawa za kulevya tena, hunywi siku 6 kwa wiki tena, utafika hapo, mwache Yesu afanye kazi ndani yako”. Nilikuwa ninavuta sigara lakini kulingana na wao, hilo halikuwa kutenda dhambi pia. Niliambiwa uongo wote mbaya kutoka kwa “upendo” huku nikiangamia kuelekea kwenye moto wa mateso. Msomaji, huu si upendo, ni CHUKI! Kwa mara nyingine ninarejelea Warumi 19:17 (ni chuki kutomkemea jirani yako ili aachane na dhambi)!

Hatimaye niliamua kuacha kutumia madawa yote, kabisa, na kumrudia Yesu mwishoni mwa mwaka wa 2012! Hii ilikuwa pamoja na kuwachana na miligramu 54 za Dilaudid nilizokuwa ninakunywa kwa ajili ya uchungu KILA SIKU, mojawapo ya dawa za kutia usingizi zilizo na nguvu zaidi duniani; na kipimo kile kingeweza wengi nguvu. Niliweza kufanya kazi nayo kwani nilikuwa nimezoea dawa za kulevya maisha mwangu mwote. Je unaeza kuamini kuwa nilikuwa nimeandikiwa dawa zile kama dawa za “ugonjwa wa kiakili” na “rafiki yangu mchungaji” alikuwa ananihimiza kuendelea kuzitumia kwani alisema nilionyesha “mabadiliko makubwa”. Ndio, baada ya upasuaji mara tisa kwenye kiwiko cha mguu kati ya mwaka wa 2010 na 2012, Daktari wa uchungu niliyekuwa naye hapa Florida alikuwa anapunguza kipimo cha Dilaudi na nilikuwa

ninakuwa hafifu sana kutokana na kupunguzwa kwa kipimo kile. Niliishia kutafuta na kupata daktari wa matibabu TN aliyeniandikia dawa halisi za uchungu za “kutibu ugonjwa wa kiakili”. Pia nilikuwa nikitumia dawa nyingi za “ugonjwa wa kiakili” mara kwa mara kutoka 1993 hadi 2012.

Mnamo tarehe 17 Desemba, 2012, nilienda hospitalini kwa muda wa siku tatu kufuatilia hali yangu kwani nilikuwa nawacha kutumia dawa ghafla. Nilitoka na kurudi nyumbani nikijua kuwa itakuwa vita vikubwa zaidi maishani mwangu. Kwa mara ya kwanza kabisa katika maisha yangu ya utu uzima, ningekuwa huru kabisa wa vitu vyote vya kigeni. Bila kuingia katika maelezo ya kina, miezi mitano iliyofuata nilikuwa karibu nisiweze kusonga. Siku moja mwezi wa Mei 2013, nililia Mungu machozi mengi baada ya kuwa mwaminifu kama nilivyoahidi kutoka tarehe 17 Desemba ya mwaka uliotangulia na kusema, “Bwana, ninaomba aidha unipeleke nyumbani mbali na uchungu huu au uniokoe kutoka kwake”. Kimiujiza, siku iliyofuata niliamka na mauchungu haya yote ya kuachana dawa za kulevya yalikuwa yamekwisha.Asifiwe!

Ni wakati huu pia ambapo, HATIMAYE nilikabili “rafiki yangu mchungaji”, kitu ambacho nilifaa kuwa nilifanya miaka 6 iliyopita, na nikamwambia atubu. Sikufanikiwa lakini angalau nilimweleza dhambi zake na nikampenda kwa kweli kama vile Yesu anavyoamuru. Nilimuuliza ni kwa nini hakunipenda kweli na kuniita kutoka kwenye dhambi zangu, jibu lake? “Sikutaka kukupoteza kama rafiki na kukusukuma mbali”. Ni

jinsi ya kidunia na yenye laana! Bado ninaomba kuwa aweze kutubu au atachomeka milele kwenye Ziwa la Moto.

**"BAADA"**

Nilipompa Kristo kila kitu changu: nikasulubisha matakwa yangu yote, ndoto, n.k. na hatimaye nikarudi kwa Bwana Yesu na macho yangu yalifunguka, ukweli wa Biblia ukaanza kudhihirika maishani mwangu. Hivi ndivyo mtu anavyojua kwa kweli anatembea na Yesu. Niliacha kujali kuhusu hisia za watu katika namna isiyo ya kimungu, ili kuwafurahisha badala ya Mungu. Sasa ninajali roho zao za milele kama Yesu anavyoamuru. Mafunzo ya Biblia kuhusu waumini kwa mfano; "watachukiwa na wote", na "dunia itakuchukia" na "adui watakuwa ndani ya nyumba yako" upesi yakadhihirika katika maisha yangu. Hii ndiyo sababu nilikiandika kitabu hiki, kwa maombi kusaidia kufungua macho na masikio ya waliodanganywa, "Yesu anakupenda jinsi ulivyo", "Mkristo". Ni lazima uelewe kuwa Yesu anakuamuru "utii amri zake" na "utembee kama alivyotembea":

***1 Yohana 2:3-6 "Na tunaweza kuwa na hakika kwamba TUNAMJUA, IKIWA TUNATII AMRI ZAKE. 4 Mtu yeyote akisema, ninamjua 5 Lakini mtu yeyote anayetii neno lake, huyo ndiye ambaye upendo wa Mungu umekamilika ndani yake kwa kweli. HIVI NDIVO TUNAVYOJUEA KUWA TUMO NDANI YA KRISTO.6 Mtu anayesema anadumu ndani ya Kristo anapaswa kuishi kama Yesu Kristo mwenyewe alivyoishi***

Nilianza huduma mwaka wa 2012, Umisheni kwa Watoto Ulimwenguni, shirika inayosaidia wamishonari asilia Afrika na Asia na huwa ninaisimamia kwa ujitoleaji wa kila siku. Ni furaha ya maisha yangu kumtumikia kutoka wakati ninapoamka hadi wakati nitakaolala. Mwaka wa 2012, kwa kweli, ni mwaka ambao sitawahi kuusahau. Ninaomba kuwa baada ya kusoma kitabu hiki kuwa hiki kitakuwa ndicho kipindi chako cha "2012" unapogundua kuwa "kuamini" si tu na midomo yako lakini pia na roho yako yote, akili, na nguvu. Ikiwa hufuati Kristo kibiblia, nimatumaini yangu kuwa sitakuwa adui yako kwa kukwambia ukweli bila kuficha; lakini endapo nitakuwa adui, utukufu wote unamrudia Yesu. Ninachagua kupenda kama Yesu anavyopenda haijalishi gharama.

***Wagalatia 4:16 "Je, sasa nimekuwa adui yenu kwa sababu nawaambieni ukweli?"***

Sura zinazofuata ni za niliyojifunza BAADA ya kutubu kwa kweli na Roho Mtakatifu akanielekeza kwenye ukweli, si "injili" ya juujuu ambayo watu wengi "wanahubiri" leo. Ninaomba uweze kutubu kulingana na Biblia (ikihitajika). Ni uamuzi wa milele.

## SURA YA KWANZA: "KANISA"

Nimetengeneza mfululizo wa video unaoweka wazi kanisa ya kisasa ambao nimeuita "Kufichua Kanisa Ibuka". Unaweza kuufikia kwa kutembelea tovuti ya **(https://eternalevangelism.com/emergent)**. Jina lingine ni "Kanisa linalojali Mfuasi" Majina mengine yanayohusishwa na makanisa ibuka ni: baada ya uinjilisti, baada ya uhifadhi, baada ya msingi, baada ya waanzilishi, wainjilisti vijana, n.k. Mapango haya maovu ya shetani yanatoa mafundisho kama "Neno la Imani" "Litaje na Ulidai" "Mafanikio", "Uponyaji na Miujiza" (Yenye haiba na Kiinjilisti), Ndimi za Uongo, Marekebisho Mapya ya Kimitume, n.k. Petro wa Pili Sura ya 2 inaeleza bayana hali ya "kanisa" leo, ninapendekeza uisome, kisha uendelee kutoka hapa. Petro anazungumza kuhusu manabii waongo na walimu waongo MIONGONI mwa washiriki wa kanisa ambao watajitokeza na kuleta uzushi mbaya; na WENGI watafuata mbwa-mwitu hawa. Tunaweza kuona bayana kuwa hili limekuja kupita kwa njia kubwa. Zaidi ya asilimia 99

ya wanaosimama nyuma ya madhabahu wamelaaniwa. Wagalatia 1:8-9 wazushi wengi ambao hawazungumzi ukweli.

Paulo, hapa chini, anasema bayana kuwa mbwa-mwitu hawa watakuwa “kati yenu”:

***Matendo ya Mitume 20:29-32 "Najua kwamba nikishaondoka, mbwa mwitu wakali watakuja kati yenu nao hawatakuwa na huruma yoyote juu ya kundi lenu. 30 Na hata KATI YENU NINYI*** (AKIZUNGUMZIA KANISA) ***patatokea watu watakaosema maneno ya kupotosha ili WAWAVUTE BAADHI YA WANAFUNZI wawafuate. 31 Kwa hivyo MUWE MACHO na MKUMBUKE jinsi NILIVYOMWONYA KILA MMOJA KWA MACHOZI USIKU NA MCHANA kwa muda wa MIAKA MITATU. 32 Na sasa nawakabidhi kwa Mungu na kwa neno la neema yake ambalo linaweza kuwajenga na kuwapa ninyi urithi pamoja na WOTE AMBAO WAMETAKASWA."***

Nimekuwa kwa mengi ya “makanisa” haya na yote yanafanana. Huwa wanatekenya masikio ya watenda dhambi na huwa hawaiti watu kwenye toba ya kweli katika huzuni ya kimungu kama ilivyoandikwa kwa uwazi katika ***2 Wakorintho 7:10-11*** “***Kwa maana huzuni ikitumiwa na Mungu huwafanya watu watubu dhambi zao wapate kuokolewa; nao wanakuwa hawana majuto. Lakini huzuni ya kidunia husababisha kifo. Tazameni faida mlizopata kutokana na huzuni hii: bidii mliyo nayo; juhudi mliyofanya kujitetea, uchungu wenu, hofu yenu, upendo wenu, shauku yenu, na jinsi mlivyokuwa tayari***

***kutoa adhabu inayostahili. Kwa kila njia mmethibitisha kuwa hamna hatia katika jambo hilo."***

Kutoka kwenye nyimbo za kisasa za "Kikristo" (Contemporary "Christian" Music (CCM)) hadi kwenye migahawa, mapango haya ya shetani ni hukumu ya kizazi kiovu, si baraka. Moyo wangu unalia kwa ajili ya roho hizi kwa sababu zinaenda moja kwa moja hadi kwenye moto wa mateso. Nilikuwa katika kanisa hizi kwa miaka 6 na nilikuwa ninazipenda nilipokuwa "mtenda dhambi aliyeokoka" nikifikiria nilikuwa ninaenda moja kwa moja hadi Mbinguni. Nilikuwa nimekosea. Biblia inasema kuwa Yesu ni rafiki yako tu IKIWA utatii:

***Yohana 15:14 "Ninyi ni rafiki zangu IKIWA MTAFA NYA NINAYOWAAGIZA."***

Yeye huandika tu wokovu wa wale "wanaomtii":

***Waebrania 5:9 "na baada ya kufanywa mkamilifu, akawa chanzo cha wokovu wa milele KWA WOTE WANAOMTII."***

Wale wanaofanya dhambi ni wa shetani:

***1 Yohana 3:8 ohn 3:8 KILA ATENDAYE DHAMBI NI WA SHETANI; kwa maana shetani ametenda dhambi tangu mwanzo. Mwana wa Mungu alikuja ili aziangamize kazi za shetani."***

Nilikuwa kipofu namna gani? Ni vipi nilipokosa kuona ukweli huu wote ulio bayana kwenye Biblia? Ni rahisi, nilikuwa

mtenda dhambi na nilitaka kuwa na dunia NA pia kuwa na Yesu kwa wakati mmoja kama wengi wa wanaomkiri Kristo wanavyofanya. Shida ni, huwezi kuwa na zote kama wengi wenu mnavyofikiria. Walio "vuguvugu" hutemwa kutoka mdomoni Mwake.

***Ufunuo wa Yohana 3:15-16 "Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto.***
***16 Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu."***

Rafiki wa dunia ni adui wa Mungu.

***Yakobo 4:4 "Ninyi viumbe wasio waaminifu! Hamfahamu kwamba URAFIKI NA DUNIA NI UADUI NA MUNGU? Kwa hiyo anayependa kuwa RAFIKI WA DUNIA ANAJITANGAZA KUWA ADUI WA MUNGU. "***

Andiko baada ya andiko likajidhihirisha kila ukurasa baada yangu mimi KUUTAFUTA ukweli na sikumwamini nabii wa uwongo "anihubirie" mistari michache inayosikika kuwa mizuri mara moja kila wiki akiwa na duka lake la mikopo hapo nyuma linalosubiri madola. Roho Mtakatifu akafungua uelewa wangu lakini ilikuwa BAADA tu ya kuwajibika kikamilifu kumfuata Yesu na Serikali yake (masharti ya kiadili). Nilionyeshwa kuwa Neema ya Mungu hufunza kuwa tunastahili kuishi maisha matakatifu kwenye ulimwengu wa

sasa. “Kanisa” ya uongo hufunza kuwa Yesu ndiye utakaso wako haijalishi jinsi unavyoishi hapa duniani. Takataka!

***Tito 2:11-12 "Kwa maana NEEMA YA MUNGU iletayo wokovu IMEDHIHIRISHWA KWA WATU WOTE. Neema hiyo inatufundisha KUKATAA UOVU NA TAMAA ZA DHAMBI, tupate kuishi maisha ya KIASI, YA HAKI NA YA KUMCHA MUNGU, KATIKA ULIMWENGU HUU.***

Ushawahi kuangalia kwa makini maandiko ambayo nimeyaandika kwenye kurasa chache zilizopita? Sababu inayofanya watu kutaka “wachungaji” hawa waongo na wanaotekenya masikio ni kuwa hawataki kutubu kwa kweli kama jinsi Yesu anavyoamuru. Ikiwa watakuja kwenye mwangaza, matendo yao maovu yatafichuliwa na hayataendelezwa. Wacha tumalize sura hii kwa mistari ambayo huwa HAISOMWI katika “kanisa” za uongo leo. Ni hakika kuwa unayafahamu maandiko ya “Yohana 3:16” na mstari wa 17 pia; kwa huzuni, mbwa mwitu hawa kwenye madhabahu nyingi sana hawataenda kwenye mstari wa 21 wa Yohana 3, usijali mstari 36! Tunafaa kuhubiri USHAURI MZIMA wa Mungu, si kuchaguachagua hapa na pale yatakayotia watu kwenye kifungo kwani wanakupa ukweli nusu na kukupa kijisehemu tu cha Biblia.

***Yohana 3:18-21 "Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini AMEKWISHA KUHUKUMIWA; kwa sababu hakumwamini Mwana pekee wa Mungu. Na hukumu yenyewe ni kwamba: Nuru imekuja ulimwenguni lakini watu wakapenda giza***

*(DHAMBI)* ***kuliko nuru*** *(YESU)* ***kwa sababu matendo yao ni maovu*** *(WAMETENDA DHAMBI)****. Kwa kuwa kila mtu atendaye maovu*** *(SIN)* ***huchu kia nuru*** *(YESU)****, wala hapendi kuja kwenye nuru ili matendo yake maovu yasifichuliwe.*** *(WANAPENDA DHAMBI ZAO KULIKO YESU)****Lakini kila mtu anayeishi MAISHA YA UAMINIFU*** *(HATENDI DHAMBI)* ***huja kwenye nuru*** *(ANAKUJA KWA YESU)****, kusudi iwe wazi kwamba matendo yake yanatokana na utii kwa Mungu."***

Mungu anachukia dhambi:

***Warumi 1:18 "Ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni dhidi ya uasi na uovu wa wanadamu ambao kwa uovu wao wanauficha ukweli usijulikane "***

Na mwenye dhambi:

***Yohana 3:36 "Ye yote anayemwamini Mwana ana uzima wa milele; asiyemtii Mwana hatauona uzima bali ghadhabu ya Mungu itakuwa juu yake daima."***

Sasa, kabla ujaribu kupinga ukweli niliouandika hapo juu, tafadhali elewa kuwa kitabu kizima cha Agano la Kale kinaelekeza kwa Yesu. Tunaona katika Agano la Kale kuwa ili kupata upatanisho baada ya kutenda dhambi, ni lazima kungekuwa na "sadaka". Yesu alipokuja na akatufia msalabani, alikuwa sadaka kamilifu ya dhambi tunayohitaji ili kuosha dhambi zetu (dhambi za kale TU, SI dhambi za sasa au za wakati ujao).

***Waebrania 10:14 "Maana kwa dhabihu <u>moja tu</u>*** *(YESU)* ***amewafanya kuwa wakamilifu milele wale wote wanaotakaswa."***

***2 Petro 1:9 " Lakini mtu ASIYEKUWA na sifa hizi ni KIPOFU, haoni mbali, na amesahau kuwa AMETAKASWA DHAMBI ZAKE ZA ZAMANI."***

***Warumi 3:25 " Mungu alimtoa awe dhabihu ya upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake*** *(YESU)**. **Alifanya hivi ili kuonyesha haki yake, kwani kwa uvumilivu wake hakuziadhibu DHAMBI ZA ZAMANI."***

Kwa hivyo, ni kweli kuwa upendo wake UNAPATIKANA kwa kila mtu, hata kwa mwenye dhambi mbaya zaidi; ni uongo kusema kuwa Anapenda wenye dhambi "jinsi walivyo kwenye dhambi"..... Sikiliza kwa makini Yesu anampenda nani, Anasema:

***Yohana 14:21 "<u>Mtu anayezishika amri zangu na kuziti miza</u> ndiye anayenipenda. Na mtu anayenipenda, Baba yangu atam penda; <u>nami</u>*** <u>*(YESU)*</u> ***<u>nitampenda</u> na kujidhihirisha kwake."***

Ni lazima utii miza za Mungu ili Akupende kama mtoto Wake.

Yesu anasisitiza hili anapoeleza ni nani ambaye Baba yake anapenda:

***Yohana 14:23-24 "Yesu akamjibu, "Mtu akinipenda atashika mafundisho yangu na Baba yangu atampenda, nasi tutafanya makao yetu kwake. Mtu asiyenipenda hayashiki mafundisho yangu na mafundisho niliyowapeni si yangu bali yametoka kwa Baba yangu aliyenituma."***

Cha msingi, ukimpenda Yesu, utatii "miza Zake."

***Mithali 7:2 "UZISHIKE AMRI ZANGU UKAISHI, Na sheria yangu kama mboni ya jicho lako."***

***Yohana 14:15 "Mkinipenda, MTAZISHIKA AMRI ZANGU."***

***Yohana 15:10 "MKIZISHIKA AMRI ZANGU, mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake."***

Tutafunga sura hii kwa kufichua dhambi za madhabahu. Ninataka kuweka wazi kuwa si kila mtu aliyeketi kwenye kanisa ya kimadhabahu, ila ni wengi wao. Ninatumia asilimia zaidi ya 99 kwa ajili ya mfano huu kama vile tu ninavyofanya kwenye mifano mingine nikizungumza kuhusu "kanisa kuu". Kwa madhabahu mengi kwa mfano Wakatoliki (wanaoabudu Mariamu, Papa n.k.), Waumini wa Kanisa la Sabato (wanaokayaa kanisa kuhusu jehanamu ya milele/ kuamini wenye dhambi watamalizwa kabisa ila hawatateketea kwenye moto wa mateso wa milele, na kudumisha Jumamosi kuwa "Sabato" kwa njia isiyofaa n.k.), Wayahudi (Uyahudi) wanachukia Yesu (Mungu Mmoja wa Kweli) na kufunza

mafundisho haya katika masinagogi zao, Wamethodisti (United Methodists) (wanaokubaliana na machukizo ya ndoa za watu wa jinsia moja”), Wakalvini (kwa kosa la pamoja la kugawanya visivyofaa na kutoheshimu ukweli kama wa “uchaguzi”, “kuamuliwa kimbele mambo yatakayompata mtu”, na “kuchaguliwa” nikitaja tu baadhi yake na pia hawaamini kuwa mwanadamu ana uhuru wa nafsi) n.k., mtu hawezi kuwa anashiriki madhabahu haya yote na aweze kuokoka huku anakosa kutii neno (Yesu).

Kuna mifano ambako mtu anayekuja kwa Kristo kwa kweli na kisha aachane na madhabahu fulani punde tu macho yake yanapofunguliwa na Roho Mtakatifu na yakaweza kuuona Ukweli. Tafadhali tambua, nyingi za kanisa “zisizo ka kimadhabahu” zimekuwa dini katika theolojia yao na zinaweza kukuwa za uongo pia. Wengi wa waongo hawa huwa kwenye “Imani ya Marcioni” ambao imani yao laanifu ni kama upatanishi, hakuna kuchukua kiapo kabisa, na huwezi ukaoa tena hata baada ya talaka ya KIBIBLIA, nikitaja mifano michache tu. Wanaamini kuwa Yesu alikuja kumkosoa Musa. Maneno ya Musa NI maneno ya Yesu, ujinga ulioje kufikiria vingine. Mafundisho mengine ya kimapepo. ***Waebrania 13:8 “Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele.”*** Kupata mafundisho kamili **(eternalevangelism.com/jesus-correct-moses)**
Leo, kuna zaidi ya madhabahu 600 tofauti na maelfu ya madhabahu madogo, huku kila moja ikifunza mafundisho tofauti ya kibinadamu, kila moja ikiwa na aina tofauti ya kuabudu, kila moja ikiwa na aina tofauti ya mipango ya

kibinadamu ya wokovu, na kila moja ikijivika jina tofauti ya kidini. Hakuna usawazisho kwa kimaandiko kwa fujo hii, ***"33Maana Mungu si Mungu wa fujo, ila wa amani." 1 Wakorintho 14:33***. Je unafikiri Mungu anawaza nini kuhusu haya yote? Mambo kama haya hayawezi kumfurahisha Bwana.

Jina madhabahu "denomination" linatokana na jina mzizi moja kama la asili "denominator" tunapozungumzia visehemu, inayomaanisha kugawa. Ugawanyaji wa kidini ni dhambi – kumaanisha kumkiri Yesu huku unagombana na ukweli wa mafundisho ya kibinadamu si kumtii Mungu; na kwa hivyo ni dhambi. Kama tutakavyozungumzia kwenye sura zijazo, tumeamuriwa kujitenga kutoka kwenye dini kama zile. Mungu hakumpa binadamu uhuru wa kuchagua aina yake ya "Ukristo" kulingana na malezi yake au mapendeleo yake ya kidini au mapendeleo mengine. Neno la Mungu linasema, "***Ndugu, ninawasihi kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo: PATANENI NYOTE KATIKA KILA JAMBO MSEMALO; yasiweko mafarakano kati yenu*** *(MADHABAHU)****; MUWE NA FIKIRA MOJA NA NIA MOJA." 1 Wakorintho 1:10.*** Hili halifanyiki katika umadhababu. Madhabahu ni za asili ya kibinadamu na hazina mamlaka yoyote ya kibiblia kuwepo. Kila madhabahu inabishana na Kanisa moja ambayo Kristo aliijenga. Biblia inapigana na madhabahu. Maelfu ya madhabahu yana masharti yao na hili kwa kweli ni dhambi kulingana na Mungu.

***Waefeso 4:4-6 "4Kuna MWILI MMOJA na ROHO MMOJA, kama vile tumaini mliloitiwa na Mungu ni moja. 5KUNA BWANA MMOJA, IMANI MOJA NA UBATIZO MMOJA; 6kuna Mungu***

***mmoja na Baba wa wote, ambaye yuko juu ya wote, afanya kazi katika yote na yuko katika yote."***

***1 Wakorintho 12:20 "20Ukweli ni kwamba, SEHEMU ZA MWILI NI NYINGI, lakini MWILI NI MMOJA."***

***1 Wakorintho 12:25 "25ili KUSIWEKO NA UTENGANO KATIKA MWILI bali viungo vyote vishughulikiane."***

Ni lazima tusikilize maneno ya Yesu, kila wakati. Hatuwezi kuchagua ukweli ambao tunataka kuamini ilhali hatusikizi mwingine. Yesu anasema vizuri katika ***Matayo 16:18b "nitalijenga KANISA LANGU; wala kifo chenyewe hakitaweza kulishinda."*** Jina "kanisa" liko katika hali ya umoja kumaanisha MOJA na jina "langu" ni la kumiliki kumaanisha ni la Bwana. Bwana alijenga kanisa Lake MOJA tu. Yesu HAKUWAHI kuahidi kujenga hata madhabahu moja. Kanisa la Kristo, lililojengwa kwenye "Mwamba", Wenyewe, lilianza karibia miaka 2000 iliyopita.

Hakukuwa na madhabahu katika karne ya kwanza na kwa mamia ya miaka iliyofuata. Bwana hakuanzisha hata moja ya madhabahu, yalianzishwa na binadamu. Zaidi ya madhabahu yote yalianzishwa takriban miaka 500 iliyopita. Bwana hakujenga hata moja ya zaidi ya madhabahu 600 tofauti zikiwa na zaidi ya visehemu 35,000 ili binadamu apate kuchagua ni kanisa gani ambayo angependa kujiunga nayo. Hii yote ni kazi ya binadamu. Kusisitiza haya, kuna mamia ya dini tofauti zenye maelfu ya visehemu; kila sehemu ina jina lake,

mafundisho yake ya kipekee yaliyotengenezwa na binadamu na matendo yanayopinga Biblia Takatifu. Inawezekanaje ata moja ya mafundisho haya kuwa ya kweli? Haiwezekani. Kitu chochote kinachopinga au ni tofauti na Biblia ni mafundisho ya uongo yaliyotengenezwa na shetani ili kufanya watu wapotee milele. Kanuni hizi za imani zinazoleta ugawanyaji na wanazozifuata zimetoka kwenye akili potovu za wanadamu ila si kutoka kwa Mungu. Vitabu vyao vyenye masharti ya kibinadamu ndicho kiunganishi cha kikundi hiki kama dini. Makanisa ya Ubatizo huhubiri Mwongozo wa Ubatizo, Makanisa ya Kikatoliki huhubiri "Katekisimu ya Kanisa la Katoliki", Makanisa ya Kimethodisti huhubiri Mwongozo wa Kimethodisti, n.k. Sababu kuu ya ugawanyaji wa kidini wa madhababu ni kuwa binadamu huwa hakubali neno la Mungu kama mamlaka ya juu zaidi. Wote huongeza na/au kutoa kutoka kwenye vitabu 66 za mwongozo wa Neno la Mungu na watalipa na roho zao.

***Ufunuo wa Yohana 22:18-19 " 18Mimi Yohana nawapa onyo wote wanaosikia maneno ya unabii yaliyomo katika kitabu hiki: mtu yeyote AKIONGEZA chochote katika mambo haya, Mungu atamwongezea MABAA yaliyoandikwa katika kitabu hiki. 19Na mtu yeyote akipunguza chochote katika maneno ya unabii yaliyomo katika kitabu hiki, MUNGU ATAMNYANG'ANYA SEHEMU YAKE KATIKA ULE MTI WA UZIMA, NA SEHEMU YAKE KATIKA MJI MTAKATIFU, ambavyo vimeelezwa katika kitabu hiki. "***

Sasa kwa sababu nimeonyesha uongo kwenye "kanisa kuu" sasa tutaendelea na kuangalia sehemu zingine ambazo ni lazima tuitikie Injili kwa njia inayofaa, au tutaangamia.

## SURA YA 2: KUFUNGWA NIRA NA FAMILIA NA MARAFIKI

Baada ya kumrudia Kristo mwaka wa 2012 na nikaanza kuhakiki toba yangu kupitia kazi zangu (mazoea na vitendo - ***Matayo 3:8 na Matendo ya Mitume 26:20***), nilianza kuona ukweli halisi wa mambo kwenye Biblia ukidhihirika katika maisha yangu. Ikiwa hushuhudii haya pia, uko katika hatari kubwa ya adhabu ya milele. Tunajua kuwa "kuwa rafiki wa ulimwengu ni kuwa adui wa Mungu? Yeyote anayetaka kuwa rafiki wa ulimwengu anajifanya adui wa Mungu" ***(Yakobo 4:4)*** kama tulivyotaja hapo juu. Kwa hivyo, unapokuwa rafiki wa Yesu ***(Yohana 15:14)***, dunia inakuchukia. Hakuna mtu atakayekosa kupitia haya na hapa ndipo ambapo watu wengi hufeli kwani hawawezi kuvumilia kujitenga kabisa na marafiki, familia, n.k. kama jinsi Biblia inavyotaja bayana kuwa yatatendeka mtu anapokuwa mfuasi wa kweli wa Kristo.

Tuangalie aya mbili za Biblia zinazozungumzia kitakachotendekea familia wa KARIBU:

***Luka 12:51-53 " 51Mnadhani nimekuja kuleta amani duniani? Hata kidogo; si amani bali UTENGANO. 52Na tangu sasa, JAMAA YA WATU WATANO ITAGAWANYIKA; watatu dhidi ya wawili, na wawili dhidi ya watatu. 53BABA ATAKUWA DHIDI YA MWANAWE, mwana dhidi ya baba yake; mama dhidi ya bintiye, binti dhidi ya mama yake; mama mkwe dhidi ya mke wa mwanawe na huyo dhidi ya mama mkwe wake."***

***Matayo 10:34-36 " 34Msidhani kwamba nimekuja kuleta amani duniani. Sikuja kuleta amani bali upanga. 35MAANA NIMEKUJA KULETA MAFARAKANO KATI YA MTU NA BABA YAKE, kati ya binti na mama yake, kati ya mkwe na mkwe wake. 36Na maadui wa mtu ni WATU WA NYUMBANI MWAKE."***

Biblia inasema ni lazima "ukubali gharama" ili kuwa mfuasi Wake na uweze kuubeba msalaba wako KILA SIKU. Yesu alimaliza kazi YAKE msalabani; sasa pia inabidi uubebe msalaba wako. Wengi hawajaubeba.

***Luka 14:26-28 "26Mtu yeyote akija kwangu, asipowachukia baba na mama yake, mke wake, watoto, ndugu na dada zake, naam, hata na nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu. 27Mtu asipochukua msalaba wake na kunifuata hawezi kuwa mwanafunzi wangu. 28Kwa maana, ni nani miongoni mwenu ambaye akitaka kujenga mnara hataketi kwanza***

***akadirie gharama zake ili ajue kama ana kiasi cha kutosha cha kumalizia?"***

***Luka 9:23-25 "23Kisha akawaambia watu wote, "Mtu yeyote akitaka kuwa mfuasi wangu,*** *NI LAZIMA AJIKANE NAFSI YAKE, AUCHUKUE MSALABA WAKE KILA SIKU, ANIFUATE.* ***24Maana, mtu anayetaka kuyaokoa maisha yake mwenyewe, atayapoteza; lakini atakayeyapoteza maisha yake kwa ajili yangu, atayaokoa. 25Je, kuna faida gani mtu kuupata utajiri wote wa dunia kwa kujipoteza au kujiangamiza yeye mwenyewe?"***

Mojawapo ya ngome ambazo nimeziona ni wakati Mkristo bandia anapofikiri kuwa anaweza kuishi maisha ya kiulimwengu na asikizane na watu wote, pamoja na wanafamilia wao ambao hawajaokoka wakati Biblia inasema bayana kinyume chake. Mtu anapokuja kwa Kristo kwa kweli ni lazima akubali kuwa familia yao nzima (ya Kikatoliki, Presbiteri, Waumini wa Kanisa la Sabato, Mormoni, Mashahidi wa Yehova, Kalvinisti, Othodoksi, Methodisti, Ubatizo, n.k.) itaenda kwenye moto wa mateso, ila tu wale ambao watatubu kutoka kwenye madhabahu hizi za uwongo wakiwa ilhali bado wako hai. Mungu haheshimu watu na watoto Wake pia hawafai kufanya ivo. Mungu alisema kwa uwazi kabisa kuwa watoto wake HAWAFAI kabisa kufunga nira na watu hawa wanaopinga Biblia na, kwa kweli, watu wote wasioamini, katika dhambi zao na mafundisho ya uongo ya kidini. Tunafaa kuwashuhudia/kuwahubiria (kuwapenda) kulingana na amri Zake kwa kuwaita watoke kwenye dhambi zao waingie kwenye Mwanga Wake wa ajabu. Watu wengi watawachukia Wakristo

wa kweli kwa kuonyesha upendo huu wa kweli kwani ni wachache tu wanaoufuata mwito wake.

***2 Wakorintho 6:14-15 " 14Msiambatane na watu wasioamini.*** *(HII INAJUMUISHA WAKRISTO BANDIA)* ***Je, wema na uovu vyapatana kweli? Mwanga na giza vyawezaje kukaa pamoja? 15Kristo anawezaje kupatana na Shetani? Muumini ana uhusiano gani na asiyeamini?***

***Zaburi 26:9-10 " 9Usiniangamize pamoja na WENYE DHAMBI, wala usinitupe pamoja na wauaji, 10watu ambao matendo yao ni maovu daima, watu ambao wamejaa rushwa."***

Roho wa Mungu unaoishi ndani ya waumini wa kweli huwezi kamwe kuvumilia giza na vilevile giza haiwezi kumvumilia Roho wa Mungu. **IKIWA** kweli unaishia na kukaa katika Kristo, dunia itakuchukia. Watu watakao kudharau ni wale wanaokiri kuwa Wakristo zaidi. Kwa nini? Kwa sababu wanaamini kuwa wataokolewa milele wakiwa bado KWENYE dhambi zao na wanataka dunia NA Yesu. Hili haliwezekani.

***1 Yohana 5:18-19 "Tunafahamu kuwa KILA ALIYEZALIWA NA MUNGU HAENDELEI KUTENDA DHAMBI; kwa sababu Mwana wa Mungu HUMLINDA na yule mwovu hawezi kumgusa. Tunajua kuwa sisi ni wa Mungu na kwamba ULIMWENGU WOTE UNATAWALIWA NA YULE MWOVU."***

***Yohana 15:19 "  Kama mngekuwa wa ulimwengu, ULIMWENGU UNGEWAPENDA WALIO WAKE; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali mimi niliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ULIMWENGU HUWACHUKIA."***

Watu wengi sana huchukia familia yao kwa kuambatana nao na hawatawahi kuwaita watubu. Ina maana kuwa "wanazipenda" familia zao kwa njia ya kiulimwengu, ya kuvumiliana, kwa njia isio ya kimungu iliyo kwenye msingi wa hisia ila si amri za Mungu. Upendo Wake ni wa kweli ***1 Yohana 4:8 "Yeye asiyependa, hakumjua Mungu, kwa maana MUNGU NI UPENDO."*** Upendo wa kiulimwengu ni bandia na ikiwa huishi ndani Yake na kutii masharti Yake ya kimaadili, huna upendo wa kweli.
***1 Yohana 4:16 "Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. MUNGU NI UPENDO, naye AKAAYE KATIKA PENDO, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake."*** Anayechukia "ndugu" yake kwa kukosa kumwonya kuhusu moto wa mateso wa milele. ***1 Yohana 4:20 "Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona."***

Mkristo wa kweli humpenda "ndugu" (jirani) yake na kutii miza Zake ***1 Yohana 5:3 "Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito."***

Je unapenda Mungu kwa kuita watu watubu au una upendo bandia wa kiulimwengu unaowapongeza wakiwa kwenye

dhambi huku wakielekea hukumuni? ***Marko 12:30-31***
***"30Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa akili yako yote na kwa nguvu zako zote. 31Na ya pili ndiyo hii: Mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi."***

Huwa pia wanachukia watoto wao binafsi kwa kutotumia fimbo ***(Mithali 13:24);*** na pia kwa kuwatuma kwenye shule za kishetani (za uma na za watu binafsi). Mama na Baba wanafaa kufunza (kufunza - ***Mithali 22:6***) watoto wao wenyewe, si kuwa na "mwalimu" mbaya awafunze na kuwafundisha kuhusu ubinadamu, "kuvumilia" mahusiano ya jinsia moja, n.k. masaa 7 kila siku, siku 5 kila wiki. Hili kwa kweli halina umungu!

Hata kama Biblia inasema mtu ni mbaya kushinda mtu asiyeamini ikiwa hawalishi watu wake (***1 Timotheo 5:8)***, pia inasema bayana kuwa hata wenye dhambi huwalinda watu wao. Kwa hivi hiki si kitu cha kipekee kwani hata waliopotea (wenye dhambi) wanajua kuwalinda watu wao (familia, n.k.). Tuangalie amri hizi:

***1 Timotheo 5:8 "8Lakini kama mtu hawatunzi watu wa jamaa yake, hasa wale wa nyumbani kwake, basi, mtu huyo ameikana imani, na ni mbaya zaidi kuliko mtu asiyeamini."***

***Utahukumiwa milele kulingana na unavyowatunza "WENGINE".***

***Luka 6:33-34 "33Tena, kama mkiwatendea mema wale tu wanaowatendeeni mema, mtapata tuzo gani? Hata wenye dhambi hufanya vivyo hivyo! 34Na kama mnawakopesha wale tu mnaotumaini watawalipeni, je, mtapata tuzo gani? Hata wenye dhambi huwakopesha wenye dhambi wenzao ili warudishiwe kima kilekile!"***

Tunaona bayana kuwa ni lazima tufanye YOTE. Tuwatunze watu wetu **NA** tuwatunze wengine. Ni lazima uwe na ***"dini safi na isiyo na hitilafu"***.

***Yakobo 1:27 " 27Dini iliyo safi na isiyo na hitilafu mbele ya Mungu Baba ni hii: Kuwasaidia yatima na wajane katika shida zao, na kujilinda mwenyewe usichafuliwe na ulimwengu huu."***

Sura hii imedhihirisha baadhi ya ukweli mkali wenye upendo unaosema bayana kuwa utachukiwa na upate mgawanyiko, hata kutoka kwa familia yako binafsi unapokuwa Mkristo wa kweli. Sasa, umehesabu gharama? Uko tayari kuwa mfuasi wa kweli? Umempa Yesu KILA KITU chako au umeketi kwenye uzio ambao ni wa shetani? Biblia inakuamuru kwa uwazi kuwa usifunge nira na mtu yeyote ambaye si Mkristo (hasaa wale wanaokiri kuwa Wakristo lakini wanatenda dhambi na/au wanaamini mafundisho ya uongo). Kufunga nira inamaanisha "kuambatana" na/au kuunga utendaji wao wa dhambi, kuwa na ushirikiano wa kiroho nao, n.k. ninaomba uweze kusikiliza ombi hili.

*2 Wakorintho 6:14-18 " 14Msiambatane na watu wasioamini. Je, wema na uovu vyapatana kweli? Mwanga na giza vyawezaje kukaa pamoja? 15Kristo anawezaje kupatana na Shetani? Muumini ana uhusiano gani na asiyeamini?*

*16Hekalu la Mungu lina uhusiano gani na sanamu za uongo? Maana sisi ni hekalu la Mungu aliye hai. Kama Mungu mwenyewe alivyosema: "Nitafanya makao yangu kwao, na kuishi kati yao; Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu."*
*17Kwa hiyo Bwana asema pia: "ONDOKENI KATI YAO, mkajitenge nao, msiguse kitu najisi, nami nitawapokea.*
*18Mimi nitakuwa Baba yenu, nanyi mtakuwa watoto wangu, waume kwa wake, asema Bwana Mwenye Uwezo."*

Usitie nguvu mkono wa mwovu usije ukawa mwovu kama wao.

*Mithali 11:21 "  Uwe na hakika na hili: Waovu hawataepuka kuadhibiwa, bali wenye haki watakuwa huru."*

*Mithali 17:15 " Yeye asemaye kuwa asiye na haki ana haki, naye asemaye kuwa mwenye haki hana haki: BWANA huwachukia sana wote wawili."*

# SURA YA 3: KUFUNGWA NIRA NA ADUI WA MUNGU

Nimezungumzia dhambi ya kufunga nira na watu wa familia na “marafiki” ambao hawajaokoka kwenye sura iliyotangulia. Sura hii itaangazia dhambi ya kufunga nira na kikundi kingine cha adui wa Mungu, Wakristo wanaokiri. Pia, nilizungumzia dhambi la uwongo wa madhabahu ambao umeongezeka “miongoni mwa wanaojidai Wakristo”. Huwa ninasikia kila mara kutoka kwa Wakristo wanaokiri kuwa ni lazima tusimame kwa “umoja” na wengine “wanaohubiri” injili. Shida ni kuwa, kundi hili la watu hupuuza kapisa dhambi mbovu ambazo “wafanyakazi” wenzao wanazifanya ambalo kwa kweli ni chuki.

Kwa mfano, kwa muda mfupi nilikuwa mmoja wa jamii ya “Wahubiri wa Mitaani (Street Preacher)” na nikakuja kugundua kuwa wengi wao ni wanafiki wakubwa. Sasa niruhusu niseme, sisemi kuwa WOTE wa wahubiri mitaani wanaelekea kwenye moto wa mateso, baadhi yao ni waumini wa kweli wanaowaita waliofungwa kwenye Mwanhgaza.

Ninatumia zaidi ya asilimia 99 kama njia ya kusema "wengi wao". Mbona? Wacha tuangalie kwa undani. Ninasifu Mungu kwa wachache huko nje wanaohubiri kwa kweli kwa waliofungwa watoke kwenye dhambi kwa bidii za kujenga ushirikiano wa wenyeji (Kanisa) kama jinsi Mitume walivyofanya.

"Wahubiri hawa wanaojiona kuwa wa kimungu" ni baadhi ya watu wanafiki zaidi, waoga, na wanaokosa umungu duniani. Kwa kweli utapata Wakalvinisti walaaniwa wakihubiri na watu wasioamini, wakihubiri na waarmenia, wakihubiri na watu wa kanisa ya ubatizo, n.k. Kwa kweli inatatanisha! Wanafunga nira na kuwaunga mkono "kwa ajili ya kuhubiri injili". MUNGU anasema hiki ni kichaa! Mbali na imani tofauti za mafundisho, watu wengi hawamwamini Mungu na huwafanya washiriki wa Westboro Baptists kuonekana kuwa kama waimbaji wa kwaya wasioshirikiana na watu wengine. Nilipowatazama wakizama ndani na ndani zaidi kwenye dhambi, nilijitenga nao na kuwakemea hadharani kama nilivyoamuriwa Desemba 2006. Haijalishi utakuwa na marafiki wangapi au kiasi gani ambacho ita "waumiza", utengano huu umeamuriwa, usifanye kosa kuhusu amri hii. Roho yako imo hatarini.

Mazoea mengine ya kuchukiza miongoni mwa wanaojiita Wakristo ni "Masemina mengi ya Kikristo"! Amini usiamini hili lakini wengi wa wanaokiri kuwa "Wakristo" huwa na masemina ambako wanakuja pamoja, wengi wakilipa mamia ya dola (au zaidi) kusafiri kusikiliza wahubiri, n.k. Kwa kawaida, kundi lile lile huja pamoja kila mwaka mara kadhaa. Shida ni

kuwa kuna watu ambao huhudhuria kutoka madhabahu na imani mbalimbali. Tayari tumezungumza kuhusu jinsi madhabahu yanachuzika Mungu. Jambo ambalo si la kimungu zaidi ni kuwa na wakalvanisti wakikaa kando yako "wakifunza" na kushirikiana na wasioamini, waarmenia, n.k. Imani zao ni tofauti lakini wanafunga nira pamoja kwa uangamizi wao kamili. Moyo wangu unahuzunika.

Semina ya karibuni iliyokuwa imehudhuriwa na watu wengi ilikuwa na mzungumzaji mmoja aliyekuwa na chaneli ya YouTube yenye zaidi ya video 60 zinazopinga ukalvisti ilhali zaidi ya wazungumzaji wenzake wawili walikuwa wakalvisti kamili! Zungumza kuhusu kuutia nguvu mkono wa mwovu na unafiki wa hali ya juu. Mahali penye moto mkali zaidi jehanamu pametengwa kwa ajili ya mashetani hawa wenye nia mbili, kiukumeni, na uwoga! Wanachukia majirani zao na Mungu kwani wanateremka na kutumbukia kwenye ziwa lao. Siwezi kufikiri kuhusu kiasi cha damu iliyo mikononi mwao.

Hii ni taarifa ya kweli kutoka kwa mtu asiyeamini Kristo ambaye ni mkiukumeni mitaani "mhubiri" ambaye amekuwa mitaani kwa miongo mingi. Anafikiri kuwa jambo tu ambalo mtu anafaa kukubaliana nalo ni "kanuni za msingi" zilizoandikwa na kiukumeni "*Chama cha Kitaifa cha Waevanjeliko (National Evangelical Association)*".

"*Nilisoma, kwenye mfululizo huu, ambapo baadhi ya watu ambao sio Wakalvanisti wanahimiza watu kutohubiri na Wakalvanisti. Hili linafaa kuangaliwa kama jambo la Warumi 14 hali ya dhamira.*

*Inafaa kuwa pia hali ya kujifunza tofauti kati ya cha msingi, mushimu, misingi ya imani ya Wakalvanisti, ambazo Wakalvanisti wanaamini, na mambo yasiyo muhimu, mafundisho ya kisekondari, zilizo kwenye Ukristo. Kwa mfano, maoni ya mtu kuhusu kuamuriwa kimbele mambo yatakayompata mtu hayajawahi kihistoria kuchukuliwa kuwa muhimu kupata wokovu. Madai ya upagani yamehifadhiwa kwa mafundisho ya msingi na muhimu zaidi ndani ya Ukristo. Kwanza, Kanisa la Kikatoliki, limetumia madai haya kwa mafundisho ya kisecondari na mafundisho yasiyo ya wokovu katika Ukristo. John Calvin pia alitumia madai haya kwa mafundisho yasiyo ya wokovu, n.k.*

*Hizi ndizo kanuni za msingi za Ukristo. Unaweza kupata taarifa hii ya imani kwenye tovuti ya Chama cha Kitaifa cha Waevanjeliko (National Evangelical Association). Tafadhali angalia jinsi ilivyoandikwa kwa ufupi.*

*Taarifa ya Imani*
*Tunaamini kuwa Biblia imeongozwa, na ndiyo Neno la Mungu pekee ambalo halijakosewa na lenye mamlaka.*

*Tunaamini kuwa kuna Mungu mmoja, milele anaishi katika miungu mitatu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.*

*Tunaamini uungu wa Bwana Yesu Kristo, kuwa alizaliwa kwa bikira, maisha yake yasiyo ya dhambi, miujiza Yake, kifo Chake wakilishi na chenye upatanisho kupitia damu aliyomwaga, kufufuka kwake, kupaa kwake kwenda upande wa kulia wa Baba, na kwenye kurudi kwake tena katika nguvu na utukufu.*

*Tunaamini kuwa kwa ajili ya wokovu wa watu waliopotea na wenye dhambi, kuzaliwa upya na Roho Mtakatifu ni muhimu sana.*

*Tunaamini katika huduma ya sasa ya Roho Mtakatifu ambaye akiishi ndani ya Mkristo anamwezesha kuishi maisha matakatifu.*

*Tunaamini katika kuokoka na waliopotea; wanaokolewa na kupata ufufuo wa maisha na waliopotea na kuingia kwenye ufufuo wa laana.*

*Tunaamini katika umoja wa kiroho wa waumini katika Bwana Yesu Kristo."*

Hiki ni kichaa kisicho na umungu! Ni lazima tuwe katika makubaliano kamili ya MAFUNDISHO YOTE na wale tunaofunga nira nao. Mtu si kaka au dada ikiwa hawakubaliani na Biblia YOTE. Wakatoliki waovu wanaamini "misingi" iliyotajwa hapa juu ilhali hilo haliwafanyi kuwa waabudu masanamu wanaoleta Mkristo wa injili isiyo ya kweli. Wajinga! Biblia inasema nini kuhusu watu hawa ambao hawaleti injili ya kweli ya Yesu Kristo?

***Wagalatia 1:8-9 " Lakini hata ikiwa sisi au malaika atokaye mbinguni AKIHUBIRI INJILI NYINGINE tofauti na ile tuliyowahubiria sisi, basi mtu huyo ALAANIWE milele! 9 Kama vile tulivyokwisha kusema kabla, sasa nasema tena, IKIWA MTU YEYOTE ATAWAHUBIRIA INJILI KINYUME na ile mliyoipokea na ALAANIWE milele."***

Waza Mitume wakisema, “Bora tunakubaliana asilimia 60 ya mafundisho ya Mungu, sote tuko sawa basi”. Kufuru! Kwa kweli ni kama “Eneo la Kisikusiku” kwa watu wanaojiita Wakristo leo. Tuko na mtaala wa sehemu nyingi unaokemea madhabahu ya kishetani ya kalvinisti/ njia zilizobadilishwa katika **(https://eternalevangelism.com/calvinism).**

“Mahubiri” haya yasio ya kimungu SI “majadiliano ya kujaribia” yamelaaniwa. Inachukua hekima kutofautisha kati ya ukweli na uwongo iwe nje mitaani, kanisani, au kwenye mitandao ya kijamii, na hata mahali kwingineko. Zaidi, wengi wa wazushi hawa huhubiri kwa usemi mchafu na uliojawa na chuki tele.

Ni lazima uwe na: ***Tito 2:8 “Maneno yako yasiwe na hitilafu yoyote ili adui zako waaibike wasipopata chochote kibaya cha kusema juu yetu.”***

Mtu anaweza akaonekana kutembea kwenye utakaso, aishi kwenye utakaso, na ahubiri utakatifu (mafundisho ya kweli ya Kristo) lakini atakosa kufika kwenda binguni kwa sababu walikuwa waoga sana na wenye kuheshimu binadamu wengine kwa kukosa kuwapenda watu waliokuwa karibu zaidi nao. Watu waliotajwa hapa juu (Wakalvini, Wabaptisti, Wakatoliki, n.k) ni wazushi wasioamini na huleta mafundisho yasio ya kweli ili kuelekeza msikilizaji katika maangamizi! BWANA anaamuru:

***2 Wakorintho 6:14 "14Msiambatane na watu wasioamini. Je, wema na uovu vyapatana kweli? Mwanga na giza vyawezaje kukaa pamoja?"***

***2 Wakorintho 6:17-18 "17Kwa hiyo Bwana asema pia: "ONDOKENI KATI YAO, MKAJITENGE NAO, msiguse kitu najisi, nami nitawapokea. 18Mimi nitakuwa Baba yenu, nanyi mtakuwa watoto wangu, waume kwa wake, asema Bwana Mwenye Uwezo."***

Mkristo anayehubiria au kushuhudia waliopotea (asiyefuata mafunzo ya Kristo) ni lazima atumie kwa kijumla maneno yanayofaa kibiblia kama jinsi Bwana Yesu anavyoamuru na pia mafundisho ya Injili yadhihirike, kwa ukaribu iwezekanavyo, kwa maneno ambayo Roho Mtakatifu anayofunza, na si kwa maneno ya kupendeza ya hekima ya binadamu mwenyewe. Usemi au lugha kama hiyo inafaa kuchaguliwa ambayo inakubalika, ni rahisi, na inaelekeza moja kwa moja kwenye lengo ambalo linatoa mawazo tu ya mambo ambayo yanakubalika kwenye Maandiko ya ukweli. Kuwapa wenye dhambi sababu ya kukuhukumu kwa kutotumia maneno yasio na hitilafu yoyote ni DHAMBI. Kwa hakika hakuna mazungumzo maharibifu au usemi mbaya unafaa kutoka kwenye mdomo wa Mkristo halisi; anafaa tu kusema maneno yanayosaidia, yenye neema, na masafi. Kwa hakika, ni sawa kutumia kemeo linalofaa panapohitajika lakini ni lazima liwe la kibiblia, si la kimwili au kidunia. Hakufai kuwa na mazungumzo ya kijinga au ya uchafu yanayofaa kutoka

kwenye mdomo wa Mkristo ambayo hayafai na hayatumiki kukemea kwa njia inayofaa.

***3 Yohana 1:11 "11Mpenzi wangu, usifuate mfano mbaya*** (KUIGA)***, bali mfano mwema. Kila atendaye mema ni wa Mungu; lakini anayetenda mabaya hajapata kumwona Mungu."***

Kosa lingine kubwa ni kuambatana na mtu anayeambatana na mmoja wa wazushi. NDIO, rafiki ambaye ni rafiki (anakataa mwingine kwa sababu ya dhambi/mafundisho mabaya ya kibiblia/injili nyingine) wa adui wa Mungu SI rafiki wa mwamini wa kweli wa Yesu Kristo. Siezi kueleza ni mara ngapi huwa ninasikia kauli za uzushi kama ifuatayo:

"*sikubaliani na usemi kuwa wanaohubiri nami lazima wasiwahi kuhubiri na wale ambao huwa sihubiri nao*" ama "*Naeza nikawa sikubakiani na mafundisho yao yote lakini bado nitahubiri pamoja nao kwa lengo moja sawa" ama "huwa hawahubiri ukalvini, au OSAS, au _______ (jaza mafundisho au dini isiyo ya kweli) mitaani kwa hivyo huwa bado ninahubiri pamoja nao"* (kumaanisha kuwa bado huwa wanafundisha au kuhubiri mafundisho yasiyo ya kweli wakiwa kwenye ushirikiano wa faragha). Waovu! "Uhuru" ni jina ambalo wazushi hawa hupenda kutumia kuteteta dhambi zao na uambatano na watu wasioamini.

Kutumia Waroma 14 kwa njia isiyofaa na kudai kuwa ni "uhuru" kunaweza kusababisha watu wengi kukubali mafundisho ya kidhambi kupitia uwongo wa wengi wanaounga mkono kifungu hiki. Kutoridhiana na Maandiko kumeelekeza

wengi kwenye njia ya maangamizi wanakoanza kuchukua kila jambo la kidhambi kwa kutumia kauli ile. Unapolihoji kundi hili la mbwa mwitu, wataungana dhidi yako na kukuita "ndugu mdhaifu". Lingekuwa jambo la kuchekesha ikiwa hawangekuwa wanamaanisha. Huwa wanakubali marekebisho ya kibiblia na ndio wasio waaminifu kwa Kristo; uwoga, udhaifu, na unafiki. Jitengeni mbali sana na mashetani hawa na wanoambatana nao.

***2 Wakorintho 7:1-2 "1Basi, wapenzi wangu, tukiwa tumepewa ahadi hizi zote, na tujitakase na chochote kiwezacho kuchafua miili na roho zetu, tuwe watakatifu kabisa, na tuishi kwa kumcha Mungu. 2Tunaomba mtupe nafasi mioyoni mwenu! Hatujamkosea mtu yeyote, hatujamdhuru wala kumdanganya mtu yeyote."***

Mambo ya kutokubaliana, mafundisho, na dhambi yanaweza yakachanganywa pamoja na tutapata dimbwi la matendo ya machukizo. Biblia inakemea wazushi hawa.

***Warumi 14:5-6 "5Mtu anaweza kufikiria siku fulani kuwa ya maana zaidi kuliko nyingine; mtu mwingine aweza kuzifikiria siku zote kuwa sawa. Kila mmoja na afuate msimamo wa akili yake. 6Anayeadhimisha siku fulani anaadhimisha siku hiyo kwa ajili ya kumtukuza Mungu; naye anayekula chakula fulani anafanya hivyo kwa kumtukuza Bwana maana anamshukuru Mungu. Kadhalika naye anayeacha kula chakula fulani anafanya hivyo kwa ajili ya kumtukuza Bwana, naye pia anamshukuru Mungu."***

Huu ni ufafanuzi hatari kukubali mafundisho na matendo ya kidhambi na kuyafanya haya yote “kwa jina la Mungu.” Kikundi chenye maono sawa ya “kuhubiri” kitaamua ni nini ambacho kinaweza au hakiwezi kuwekwa kwenye orodha waliyoitengeneza ya uhuru “unaokubalika” katika “dhambi” za ushirikiano. Hili si tofauti na mafunzo ya kibinadamu ya maelfu ya dini tulizozungumza kuhusu katika sura ya kwanza. Jaribu kujiingiza kwenye kikundi hiki na utakemewa, utaitwa “kurutu”, “ndugu mdhaifu” au utaambiwa ujitenge mbali na njia zao ikiwa “hutafanya kama wao”. Hawa wana uwezekano mdogo zaidi wa kurekebishwa kwa sababu ya mawazo haya ya kimakundi. Ni roho wa kishetani na toba ni nadra. Ila ninaamini KILA kitu kinawezekana Mungu akiwa kati. Kwa hakika wengi hukanusha na hawatawahi kuja kwa (au kumrudia) Kristo.

Jina lingine wanalotumia kutetea dhambi zao ni “dhamira”. Swali lazima liulizwe, je mfuasi wa Kristo anaweza kufuata dhamira yake mwenyewe akiwa na uhakika kamili akilini mwake kuhusu mafundisho na matendo ya kidhambi? Jibu ni HAPANA, vinginevyo, ukweli utakuwa unatofautiana kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine. Aibu!

Kwa bahati mbaya, utamaduni wa binadamu na “washauri” huamua wanachokiona kuwa sahihi na makosa kulingana na dhamira yao binafisi. CHACHU KIDOGO HUCHACHUSHA DONGE LOTE LA UNGA!

***1 Wakorintho 5:6-7 "5Mtu anaweza kufikiria siku fulani kuwa ya maana zaidi kuliko nyingine; mtu mwingine aweza kuzifikiria siku zote kuwa sawa. Kila mmoja na afuate msimamo wa akili yake. 6Anayeadhimisha siku fulani anaadhimisha siku hiyo kwa ajili ya kumtukuza Mungu; naye anayekula chakula fulani anafanya hivyo kwa kumtukuza Bwana maana anamshukuru Mungu. Kadhalika naye anayeacha kula chakula fulani anafanya hivyo kwa ajili ya kumtukuza Bwana, naye pia anamshukuru Mungu:"***

***Mithali 14:34 "Haki huinua taifa; Bali dhambi ni aibu ya watu wowote."***

Mfumo wa kisasa wa "Kanisa Kuu" na washerati, wasio na heshima, na watukanaji wamekubali mambo yaliyo ya aibu na hufanya majaribio dhahiri kueleza sababu ya matendo yao katika "uhuru" na "upendo" kwa majirani yao. Huu ni upendo usio wa kweli ambao nilikuwa nao. Wao hutumia njia ya "kuwa dhaifu katika imani" kujaribu kuwapuuza waamini wanaowakemea.

***Warumi 14:1-3 "1Mkaribisheni kwenu mtu aliye dhaifu, lakini msibishane naye juu ya mawazo yake binafsi. 2Watu huhitilafiana: mmoja imani yake inamruhusu kula kila kitu; lakini mwingine ambaye imani yake ni dhaifu, hula tu mboga za majani. 3Mtu ambaye hula kila kitu asimdharau yule ambaye hawezi kula kila kitu; naye ambaye hula tu mboga za majani asimhukumu anayekula kila kitu, maana Mungu amemkubali."***

Mistari hii inatumika kama visababu tu vya kupokea dhambi kwenye duara lao la ushirika au mahubiri wakati Mungu hatawapokea katika duara lake. “Wahubiri wa mitaani” walio vipovu wa mafundisho hutwambia kuwa hatufai “kupinga” au “kuhukumu” kwa sababu ni mambo yenye mabishano. Takataka!

Uwongo mkubwa ni kuwa haya SI mambo yanayokubalishwa kubishaniwa ilivyodhihirishwa kwenye Maandiko kwa sababu mambo yenye mabishano hayakubaliki katika eneo la dhambi la kuvunja amri za Mungu.
“Warumi 14” ipo kwenye muktadha wa mambo ambayo hayajakatazwa (yenye dhambi) wala kukubalika. Katika mstari wa 14, 16, na ishirini, ni mambo yanayoonekana na Paulo kuwa “mazuri”, “meupe”, au “safi” katika kupokea mmoja kwa mwingine kwenye ushirika wetu kwa msingi wa uhuru unaokubalika Kimaandiko, SI kwenye mambo ya kidhambi na tabia zinazoiga maovu ambayo “watakatifu” hawa ambao kwa kweli ni wenye dhambi hujaribu kutetea. Kutoka kikundi kimoja hadi kingine na kuuita “uhuru” ni makosa hatari.

Wengi pia huanguka kwa sababu “wanahubiri” kwa namna ambayo dunia inaiona aidha kama “burudani” au inachochea hasira, kwa njia isiyofaa! Hawawaelekezi watu kuwa na uhusiano mzuri na Kristo katika mambo yote wanayoyafanya. Kazi zao ni kama “matambara machafu” kwani huwa hawahubiri injili na kwa uhakika wanachukia “ndugu” yao.

**1 Wathesalonike 5:22 “na EPUKENI KILA aina ya uovu.”**

***Warumi 13:12 “12Usiku unakwisha na mchana unakaribia. Basi, tutupilie mbali mambo yote ya giza, tukajitwalie silaha za mwanga.”***

Shida ni kuwa waliojawa na mafunzo ya kidini hupuuza kabisa ukamili wa Maandiko na kutumia mafundisho yao yaliyopindwa kama msingi wa kutetea Maandiko na kutumia mafundisho yao yaliyopindwa kama msingi wa kutetea “mahubiri” haya mabaya yanazungukia mistari fulani tu, hasaa Warumi sura ya 14. Wanataka kugeuza Maandiko na kufunza jambo ambalo ni tofauti kabisa na maana ya kweli iliyokusudiwa.
Wale wanaopinda Maandiko watapinda mistari yoyote, ama Biblia nzima, lakini mara nyingi watatumia sehemu tatanishi ili kuridhisha maelezo yao maongo. Mavutio ya wanaopinda Maandiko hupendeza watu wa kundi lile kwa kutoa kisingizio cha anasa zao na dhambi za wafuasi wenzao, pamoja na zao binafsi. Hakuna anayekubali kurekebisha madhara yao na mawazo ya “kimakundi” hutawala wanapoitwa kwenye toba. Na wanapoona makosa na “kutubu”, huwa si toba ya kweli ila ni ya kulazimishwa kwani hawataki kutolewa kwenye “kikundi”, kabisa, ambalo litafanyika wanapotubu kwa kweli kwa huzuni ya Kimungu na kutii amri zake ZOTE. Toba ya uongo inafanyika sana katika makundi haya. Tutaangalia toba ya kweli katika sura nyingine huko mbele.

***2 Petro 3:17-18 "17Lakini ninyi, wapenzi wangu, mmekwisha jua jambo hili. Basi, muwe na tahadhari MSIJE MKAPOTOSHWA NA MAKOSA YA WAASI, mkaanguka kutoka katika msimamo wenu imara. 18Lakini endeleeni kukua katika neema na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu uwe kwake, sasa na hata milele! Amina."***

Maneno ya Petro ambayo umeyasoma ni dhahiri kuwa yameandikwa ili wafuasi wa Yesu wawe macho na wajitahadhari na wanaopinga Neno la Mungu. Anatarajia kuwa dada na kaka wake wa kweli ya Kristo waweze kuwatambua wanaobadilisha Neno la Mungu. Kila mfuasi wa Kristo aliyejazwa na Roho anafaa aweze kuwatambua watu ambao Petro anatuonya kuhusu hapo juu, hakuna shaka kuhusu hilo. ***Warumi 14:5 "5Mtu anaweza kufikiria siku fulani kuwa ya maana zaidi kuliko nyingine; mtu mwingine aweza kuzifikiria siku zote kuwa sawa. Kila mmoja na AFUATE MSIMAMO wa akili yake."***

Waongo hawa huamini kuwa tunaweza kuweka chochote kile kwenye mstari huu bora "tunafuata msimamo wa akili zetu," na kukihalalisha. Ni wendawazimu! Wanagawa Warumi 14 kwa njia isiyo sahihi bila kujua kuwa inazungumza kuhusu "siku za kipekee" kwa sababu Wayahudi walikuwa na tamaduni za kibinadamu kuhusu KUFUNGA mara kadhaa kila wiki. Wale ambao hawakufuata mtindo huu walionekana kuwa watakatifu dhaifu. Paulo alikuwa tu anatangaza kuwa tunachokifanya au tusichokifanya ni sawa katika hali za siku za kiyahudi za kujifunga na matendo ya ulaji. "Siku" ambazo Paulo alikuwa

akizungumza kuhusu ni zile za utamaduni wa kufunga zinazotajwa katika Zekaria 7:5-6.

Paulo hakuhimiza watu kuchukua mila na tamaduni za kipagani ili kumwabudu Mungu nazo na wala hakukubali "mahubiri" yaliyojawa na machukizo. Hili ni zaidi ya kile ambacho Paulo alikuwa ameongozwa kuandika kukihusu. Petro alituonya tusielewe kwa njia isiyofaa maandishi ya Paulo.

Warumi 14 inazungumzia aina fulani ya chakula katika siku za kujifunga na jinsi imani za watu kuhusu kujifunga hazifai kuingiliwa. Siku za kujifunga zinafaa kufuatwa kulingana na dhamira ya mtu binafsi, ila si yako mwenyewe. Mtu anaweza kula, au akose kula, azingatie siku ile au akose kuizingatia. Kila binadamu anaweza kufuata SIKU ZA KUFUNGA, au akose, kulingana na dhamira zao binafsi.

***Warumi 14:20 "20Basi, usiiharibu kazi ya Mungu kwa sababu ya ubishi juu ya chakula. Vyakula vyote ni halali, lakini haifai kula chakula ambacho kitamfanya mtu aanguke katika dhambi."***

Tumeitwa kutengwa katika Ukweli, si kuunganishwa katika uongo.

***1 Yohana 2:4-6 "4Mtu akisema kwamba anamjua, lakini hazitii amri zake, basi mtu huyo ni mwongo, na ukweli haumo ndani yake. 5Lakini mtu yeyote anayeshika neno la Mungu, huyo***

***ndiye aliye na upendo kamili wa Mungu ndani yake. Hivi ndivyo tunavyoweza kuwa na hakika kwamba tunaungana naye: 6mtu yeyote anayesema kwamba ameungana na Mungu, ANAPASWA KUISHI KAMA ALIVYOISHI YESU KRISTO."***

Kutengeneza mafundisho katika kupinda Maandiko kulingana na ufafanuzi wa mtu binafsi wa kifungu fulani haugawi Neno kwa njia inayofaa. Watu wengi wanafaa kutubu kutoka kwenye kisingizio hiki cha “Warumi 14”. Na hatimaye, ***Matayo 18:15-20*** inazungumza kuhusu ushirikiano au kanisa la KIENYEJI tu, ila si dhambi za umma ambazo ni ujuzi wa kawaida, wala Matayo 18 haizungumzi kuhusu kuweka wazi na kukemea mafundisho maongo ambayo tayari yameshashirikishwa hadharani.

***2 Yohana 1:8-11 “8Basi, jihadharini ninyi wenyewe ili msije mkapoteza kile mlichokishugulikia, bali mpate tuzo lenu kamili. 9Asiyezingatia na kudumu katika mafundisho ya Kristo, bali anayakiuka, hana Mungu. Lakini anayedumu katika mafundisho hayo anaye Baba na Mwana. 10Basi, kama mtu akija kwenu bila kuwaleteeni mafundisho hayo, msimkaribishe nyumbani kwenu, wala msimsalimu. 11Maana anayemsalimu mtu huyo, anashirikiana naye katika matendo yake maovu.”***

Mafunzo zaidi kuhusu somo hili yanapatikana hapa **(https://eternalevangelism.com/appropriate-preaching).**

# SURA YA 4: “USIHUKUMU”

Mojawapo ya kauli inayotumika sana na wenye dhambi, pamoja na “watenda dhambi waliookoka” ni “usihukumu”! Mbona? Wapo kwenye dhambi na hawataki kurekebishwa. Wanafurahia njia zao za uovu na dhambi kwa kiasi kikubwa na wanamchukia Mungu kwa kweli. Wakosaji wakuu? Wanaokiri kuwa Wakristo wakiwa wameketi kwenye viti vya kanisa kila Jumapili.

Siwezi kukumbuka ni mara ngapi ambazo nimesikia, “Usihukunu, ili nawe usihukumiwe?” ***Matayo 7:1*** hukiriwa kwa maudhui yasiyofaa na wenye dhambi (hasaa “wenye dhambi” waliokoka) wanaotetemeka kila mara mtu anapohubiri dhidi ya dhambi, hasaa dhambi zao. Kwa hakika ni jambo tata kusikia watu wakiudhika sana unapowapa mistari dhahiri ya Biblia zinazozungumzia utakatifu kwa mfano ***Waebrania 12:14*** ***“14Jitahidini kuishi kwa amani na watu wote. Ishini maisha ya utakatifu, kwa sababu hakuna mtu atakayemwona Bwana bila ya maisha kama hayo.” Matayo 7:1*** katika muktadha huu (mistari 1-5) inafunza bayana jinsi ambayo mtu anafaa kuhukumu baada ya kujihukumu BINAFSI. Yesu anaamuru hukumu adilifu iliyo kwenye mipaka ya amri za kiadili. Hukumu ni upendo wa kweli unapojali roho ya mtu iliyopotea.

Zaidi ya mara 700 kwenye Biblia Takatifu jina “hukumu/amua” na aina zake nyingi (kuhukumu, anayehukumu, hukumiwa, uamuzi, n.k.) limetumika. Kuna kitabu kizima kinachoitwa

“WAAMUZI’ kilichoandikwa wakati Mungu alipowainua waamuzi kuwaongoza watu wake. Tutadhihirisha bila shaka lolote kuwa Mungu ANATARAJIA watu wake kuhukumu. Wewe ni mwenye dhambi asiye na upendo ikiwa hutafanya hivi. Kuhukumu kunadhihirisha upendo wa kimungu ukiwa katika matendo.

Kabla uhukumu wengine kwa upendo, ni lazima kwanza ujihukumu mwenyewe. Ni lazima utoe boriti kwenye jicho lako binafsi kabla ujaribu kutoa kibanzi kwenye jicho la jirani yako. ***1 Wakorintho 11:30-31: “30Ndiyo maana wengi kati yenu ni dhaifu na wagonjwa, na wengine kadhaa wamekufa. 31Kama tungejichunguza wenyewe vizuri hatungeadhibiwa hivyo.”***

Ikiwa wewe ni Mkristo wa kweli anayetembea katika utakatifu na ni sahihi kibiblia, basi wewe ni mmojawapo na ni mwana wa Mungu. Ikiwa utakataa kujihukumu kwanza kama mwana wa Mungu, basi kwa hakika Mungu atakuhukumu. Ikiwa unatenda dhambi za kutenda mambo ambayo Mungu hajahalalisha na au dhambi za kutotenda kilicho chema na ulichoamuriwa kufanya, Atakuona kuwa mwenye makosa!

Unapokosa kujihukumu, utakumbana na shida katika maisha haya pale Mungu anapokuhukumu. Yesu anasema katika ***Matayo 7:4-5 ” 4Au, wawezaje kumwambia ndugu yako, Ndugu, ngoja nikuondoe kibanzi jichoni mwako, wakati wewe mwenyewe unayo boriti jichoni mwako? 5Mnafiki wewe! Ondoa kwanza boriti iliyoko jichoni mwako na hapo ndipo utaona waziwazi kiasi cha kuweza kuondoa kibanzi kilichoko jichoni***

***mwa ndugu yako.”*** Hakimu mzuri hawezi akakosa kujihukumu mwenyewe, kwa hakika, huwezi ukawa hakimu mwadilifu ikiwa huishi kwa utakatifu. Utakuwa wewe ni mnafiki tu!

Wengi wanaokiri kuwa “Wakristo” huamini kuwa mtakatifu hafai kuhukumu, ilhali kila mtu (hata wenye dhambi) huhukumu kila siku ya maisha yao. Kwa hakika, ni chuki iliyo wazi kutohukumu “matunda” (kazi) ya mtu*. **Matayo 7:16-17 “16Mtawatambua kwa matendo yao. Je, watu huchuma zabibu katika miti ya miiba, au tini katika mbigili? La! 17Basi, mti mwema huzaa matunda mema, na mti mbaya huzaa matunda mabaya.”*** Mtu anawezaje kujua ikiwa tunda la mtu ni nzuri au mbaya? Ni lazima uhukumu, uangalie, ujaribu, utazame.

Njia tu ambayo unaweza kumsaidia mtu na kuwaita kwa upendo watubu ni kwa kutambua kuwa wapo kwenye dhambi? Jinsi gani? Kwa KUHUKUMU. Biblia, ambayo ni neno la Mungu hata inatuamuru tuhukumu; lakini ni lazima tuhukumu kiadilifu. Wacha tuweke hisia na maoni kando na tuone Biblia inavyosema. Hayo ndiyo mamlaka ya kwanza, si sisi wala mafundisho yasiyo ya kweli yanayopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine au uongo unaofunzwa kwenye “seminari” au “shule ya biblia” ambazo ni machukizo.

Baba wa uongo hataki uhukumu kwa sababu anajua kuwa kuhukumu kwa njia adilifu KUNAMPENDEZA Mungu kwani tunatii amri zake. Mtu husema, “Wengi huuliza ikiwa tunafaa kuhukumu watu BINAFSI?” 100% ndio! Paulo ANAKEMEA Wakorintho kwa KUTOHUKUMU*. **1 Wakorintho 5:11-13***

***"11Nilichoandika ni hiki: msishirikiane na ndugu Mkristo aliye mzinzi, mchoyo, mwenye kuabudu sanamu, mchongezi mlevi na mlaghai. Mtu wa namna hiyo, hata kula msile naye. 12Je, ni shauri langu kuwahukumu watu walio nje? Hao Mungu atawahukumu. Je, ninyi hampaswi kuwahukumu wale walio katika jamii yenu ninyi wenyewe? 13Mfukuzeni mbali nanyi huyo mwovu!"*** Paulo yuko katika shida kubwa kwa "kuwapoteza Wakristo hawa" kama wanavyosema wazushi wa "USIHUKUMU"! Anawaambia kwa njia wazi kuwa WAKUHUMU WATU jambo ambalo ni adilifu na lenye upendo. Ni kwa jinsi gani ambayo tunaweza kutii amri kama ***Warumi 16:17-18? 2 Wakorintho 6:17? 2 Timotheo 3:5-6? 1 Yohana***, n.k. ikiwa kuhukumu watu ni makosa? Mungu amejipinga mwenyewe kwa kiasi kikubwa kwa hivyo maneno yake hayawezi kuaminika ikiwa Mkristo hawezi akahukumu kwa upendo. Tambua ***Malaki 3:18: "Hapo ndipo mtakapotambua tena tofauti iliyopo kati ya waadilifu na waovu; naam, kati ya mtu anayemtumikia Mungu na asiyemtumikia."*** LO! Kwa hakika Bwana anasema si makosa kuhukumu. Tazama ***Ufunuo wa Yohana 2:2 "Najua matendo yako, bidii yako na uvumilivu wako. Najua kuwa huwezi kuvumilia watu waovu na kwamba umewapima wale wanaojiita mitume na kumbe sio, na umetambua ya kuwa wao ni waongo:"***

Je unafikiria kwa kweli Bwana angependezwa na Wakristo hawa ikiwa ni makosa kuhukumu? La hasha. Je unawezaje kumwona mtu kuwa mwongo ikiwa hutahukumu? Unawezaje kumwita jirani yako anayetenda dhambi kwenye Mwangaza wa Ajabu wa Yesu ikiwa hutahukumu? Haiwezekani! Kuhukumu kwa njia inayofaa "kumpenda jirani yako"

kunamheshimu Mungu. Kupuuza hili kunapuuza maandiko yote. Mungu anatutarajia kuhukumu kwani ndio upendo wa kweli wa roho ya mwenzio.

Mungu anawaamuru Wakristo kwa uwazi wahukumu*. Zaburi 37:30 "Mtu mwadilifu husema maneno ya hekima, kwa ulimi wake hunena yaliyo ya haki"* Mkristo wa kweli HATAKATAA kuhukumu na hatazungumza mabaya kuhusu wanaofanya hivo. Atafurahi katika hukumu ya kiadilifu*. Amosi 5:14-15 "14 Tafuteni mema, wala si mabaya, mpate kuishi; hivyo Bwana, Mungu wa majeshi, atakuwa pamoja nanyi, kama msemavyo. 15 Yachukieni mabaya; yapendeni mema; mkaithibitishe haki langoni; yamkini kwamba Bwana, Mungu wa majeshi, atawafanyia fadhili mabaki ya Yusufu".* Unayapenda maovu na kuyachukia mema ikiwa huhukumu*. Mithali 17:15 "Yeye asemaye kwamba asiye haki ana haki; naye asemaye kwamba mwenye haki hana haki; Hao wote wawili ni chukizo kwa BWANA."*

Usimuonye mwovu (mwenye dhambi)? Basi damu yao ii mikononi MWAKO ndivyo asemavyo BWANA.

***Ezekieli 33:8-9 "8Nikimwambia mtu mwovu: 'Wewe mtu mwovu hakika utakufa'; lakini wewe husemi chochote ili kumwonya yule mtu mwovu aachane na mwenendo wake; mtu huyo hakika atakufa kwa kosa lake; walakini nitakudai wewe kifo chake. 9Lakini ukimwonya mwovu aachane na mwenendo wake, naye haachani na mwenendo wake mbaya, yeye atakufa kwa kosa lake; lakini wewe utakuwa umeyaokoa maisha yako."***

Usikufe moyo katika kuhukumu, WENGI hawatakusikia kwani ni wachache tu watakaoingia Mbinguni na ni lazima kuwe na "**UASI KWANZA**" kabla Yesu arudi. Tutazungumza, kwa upana, "uasi" huu mkuu katika sura itakayofuata baadaye kwenye kitabu. ***2 Wathesalonike 2:3 "Mtu asiwadanganye kwa namna yo yote maana siku hiyo haitakuja kabla ya UASI KUTOKEA KWANZA na yule mwasi adhi hirishwe, yule ambaye mwisho wake ni kuangamizwa kabisa."***

Je wewe ni mtu wa kiroho? Basi ni lazima uhukumu "vitu vyote" ***1 Wakorintho 2:15. "Mtu wa kiroho anao uwezo wa kupima KILA KITU, lakini yeye hapimwi na mtu."*** Watu waovu (wenye dhambi) huwa hawaelewi hukumu, wanaomtafuta Mungu huelewa ***Mithali 28:5. "Watu wabaya hawaelewi na hukumu; Bali wamtafutao Bwana huelewa na yote."***

Ni lazima tumfuate Kristo, tuwe kwenye neno na tuweke upanga wetu ukiwa na makali kila wakati. Solomoni alipokea ufalme wake na akaomba Mungu hekima na maarifa ya kuhukumu. ***1 Wafalme 3:9 "9Kwa hiyo, nakuomba unipe mimi mtumishi wako moyo wa kusikia ili kuamua watu wako, niweze kutambua mema na mabaya; maana ni nani awezaye kuhukumu watu wako walio wengi hivi?"*** Omba hekima na uwezo wa kuhukumu kiadilifu. ***Yakobo 1:5 "Lakini kama mmoja wenu ametindikiwa hekima, basi, anapaswa kumwomba Mungu ambaye atampatia; kwani Mungu huwapa wote kwa wingi na kwa ukarimu."***

Usiwahi kuhukumu vitu ambavyo huna mamlaka ya kuhukumu. Usiwe mwanasheria mkali. Hatufai kuwa wepesi wa kuhukumu. ***Wakolosai 2:16: "Kwa hiyo, basi, msikubali kupewa masharti na mtu yeyote kuhusu vyakula au vinywaji, siku za sherehe, sikukuu ya mwezi mpya au Sabato:"*** Haya hayafai kuwa mambo makubwa leo. Sherehe za Wayahudi (amri za kisherehe, si amri za kimaadili) hazihitajiki kwa Wakristo wa Mataifa (angalia Matendo ya Mitume sura ya 15); kwa hivyo mambo haya yanafaa kusababisha ubishi tu ikiwa mtu atafayafanya kuwa mahitaji kimakosa – kwani anapinga hukumu ya Mungu kuhusu suala hili (kwa mara nyingine, angalia Matendo ya Mitume sura ya 15).

Usipendelee watu kama tulivyoeleza katika sura ya hapo awali. Usikose kutoa hukumu ya upendo: ***Mithali 24:23 "Haya nayo pia ni maneno ya wenye akili. Kupendelea watu katika hukumu si kwema."*** Tunafaa kufanyia kila mtu haki bila kupendelea marafiki au jamaa zetu. Hakimu mwadilifu huwa hashawishiki na ushawishi wa nje ***(Isaya 42:1, 19-21).***

Usiwe mwepesi wa kuhukumu. Uwe na ukweli wote kabla ya kutoa hukumu. ***Yeremia 5:1 "Kimbieni huko na huko mjini Yerusalemu; pelelezeni na kujionea wenyewe! Chunguzeni masoko yake mwone kama kuna mtu atendaye haki mtu atafutaye ukweli; akiwako, basi Mwenyezi-Mungu atausamehe Yerusalemu."*** Hakimu wa kweli hutafuta ukweli na kukusanya ukweli mwingi iwezekanavyo. Kwa upande mwingine, usikose kutoa hukumu ikiwa dhambi ni dhahiri.

Uwe mwenye huruma unapotoa hukumu. Yesu anasema katika ***Matayo 7:2: "Kwa maana hukumu uta kayotamka juu ya wenzako ndio itakayotumiwa kukuhukumu, na kipimo utakachotoa ndicho utakachopokea."*** Mtu huvuna analichokipanda ***Wagalatia 6:7-8 "Msidanganyike, Mungu hadanganywi. Kwa maana kila mtu ata vuna kile alichopanda. [8] Mtu apandaye katika tamaa za mwili, ata vuna kutoka katika mwili uharibifu; lakini yeye apandaye katika Roho, atavuna kutoka katika Roho uzima wa milele."*** Usikose kufuata Biblia ama uwe na ukali mwingi kuhukumu wengine katika njia isiyo adilifu kwani Mungu anaahidi kuwa hukumu sawa itakurudia. Tunafaa tukumbuke, ingawa hatufai kuridhiana au kuficha ukweli wa Neno la Mungu, Amekuwa mwenye huruma kwetu hata kama hatukustahili. Kemeo nzuri la upendo kwa kweli limeamriwa kwa wasioskia ***1 Timotheo 5:20 "Wale wanaoendelea kutenda dhambi uwaonye hadharani kusudi wengine wapate kuogopa."*** Kama jinsi kidonda kinavyopona ***Mithali 27:6 "Majeraha kutoka kwa rafiki yaonyesha uaminifu, bali kubusu kwa adui ni kwingi sana."*** Kwa hakika tunafaa kuonyesha huruma ya kibiblia kwa wengine unapojaribu kuwarudisha kwa Kristo. Ila ukumbuke kuwa wengi hutusi huruma ya Mungu. Mungu katika matendo yake ya huruma na watu huwa haiachi hukumu na kwa hivyo huwa hapuuzi dhambi za watu, hiyo inaweza kuwa ni chuki tu ambayo wengi wa wanaokiri kuwa Wakristo hufanya. Hakuna yeyote awezaye kumrudia Kristo bila toba ya kweli kutoka kwenye dhambi. ***Mithali 28:13 "Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; Bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema."***

Kizazi chetu kiovu kimeelezwa vizuri katika ***Isaya 59:8: "Njia ya amani hawaijui; wala hapana hukumu ya haki katika miendo yao; wamejifanyizia njia zilizopotoka; kila apitaye katika njia hizo hajui amani."*** Hakuna imani kwa wanaokataa kuhukumu. Kwa hakika, huu ni wakati wa ubinadamu na "ishi na wacha aishi" Paulo anasema katika ***1 Wakorintho 1:10 "Nawasihi ndugu zangu, katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba mpatane ninyi kwa ninyi, na pasiwepo na utengano kati yenu. MUUNGANE PAMOJA KIKAMILIFU KATIKA KUWAZA NA KATIKA KUAMUA."*** Ikiwa kuhukumu ni makosa, basi mbona Roho Mtakatifu akamwongoza Paulo kusema kauli ile? Haiwezekani! Paulo anaendelea kueleza amri hii ***1 Wakorintho 2:15 "Mtu wa kiroho anao uwezo wa kupima kila kitu, lakini yeye hapimwi na mtu."*** Kuhukumu si dhambi: kutoa hukumu ni amri ambayo Wakristo waadilifu hutii.

Mwisho, wengi wa Wakristo wanaokiri wangemwita Yohana Mbatizaji aina zote za majina kama mtoaji hukumu, mwenye chuki, asiyejali, mwanasheria, mwenye kiburi, anayejidai, n.k. na hawangetaka kuhusishwa kivyovyote na yeye. Ila, Yesu alisema kuhusu Yohana katika ***Luka 7:28 "Nawaambia, kati ya binadamu wote, hakuna aliye mkuu kumzidi Yohana. Hata hivyo aliye mdogo kabisa katika Ufalme wa Mungu ni mkuu kuliko Yohana."*** Yohana Mbatizaji, kama wale Mitume wengine wa Yesu 11 kati ya 12, alichinjwa kwa kuwapenda wengine kwa kuwaita kutoka kwenye dhambi watubu. Mtume wa 12, Yohana, alichemshwa kwenye mafuta kabla ya kupelekwa uhamishoni kwenye kisima cha Patmos alikopokea kitabu cha Ufunuo wa Yohana. Je unapendwa au unachukiwa na dunia?

Hili litaamua kama umeokoka kwa sasa ama la. Kutoa hukumu si upendo tu mbali ni tendo takatifu lililoamrishwa.

Sasa, “Wawestboro” na “wahubiri wa mitaani” wengine wanachukiwa kwa sababu **zisizo za kiadilifu** na mwisho wao utakuwa pamoja na mapagani wanaowahubiria. Ni wenye dhambi wanafiki wasio na msimamo, wanaohubiria wenye dhambi. ***1 Petro 3:13-17 "Ni nani atakayeweza kuwadhuru nyinyi KAMA MKIZINGATIA KUTENDA MEMA? Lakini, hata kama ITAWAPASA KUTESEKA KWA SABABU YA KUTENDA MEMA, basi, MNA HERI. MSIMWOGOPE mtu yeyote, wala MSIKUBALI KUTIWA KATIKA WASIWASI. Lakini mtukuzeni Kristo kama Bwana mioyoni mwenu. Muwe tayari kumjibu yeyote atakayewaulizeni juu ya matumaini yaliyo ndani yenu, lakini fanyeni hivyo kwa upole na heshima. Muwe na dhamiri njema, kusudi mnapotukanwa, wale wanaosema ubaya juu ya mwenendo wenu mwema kama Wakristo, waone aibu. Maana ni afadhali kuteseka kwa sababu ya kutenda mema, kama Mungu akipenda, kuliko kuteseka kwa sababu ya kutenda uovu. "***

## SURA YA 5: KUPOKEA UPENDO AU CHUKI YA MUNGU KUNAKUTEGEMEA WEWE

Mungu anapenda na kuchukia kikamilifu. Hukumu yake ni kamilifu na neno lake ni la milele na la kweli. Ninapohubiri na

kushuhudia Kristo kama Mfuasi wake, wenye dhambi husema kila mara, "Mungu anatupenda bila masharti yoyote"! Nina mwalika mtu yeyote kudhihirisha hili kutoka kwenye Biblia. Haiwezekani kwa sababu huo ni uwongo dhahiri.

Hutapata hata mstari mmoja kwenye Biblia unaosema kuwa Mungu anampenda mwanadamu bila masharti, pamoja na "wanaokiri kuwa Wakristo" ama "wenye dhambi" bila masharti, masharti yake matakatifu; amri ya kimaadili ambayo ilikuwa tangu mwanzo na itakuwa mpaka mwisho. Wengine hujaribu kupinga maandiko kama ***Waroma 5:8 "Lakini Mungu amethibitisha kwamba anatupenda, maana wakati tulipokuwa bado wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu."*** ama ***Yohana 3:16 "Kwa maana Mungu aliupenda ulimwengu kiasi cha kumtoa Mwanae pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."*** Wanapojaribu kudhihirisha upendo endelevu wa Mungu.

Ila, ikiwa mtu atagawa neno vifaavyo, mistari hiyo haisemi kuwa Mungu anapenda binadamu wote wakiwa kwenye hali yao ya sasa yenye dhambi. Inasema aliwapenda. Kitenzi cha Kigriki "agapao" (kinachomaanisha kupendwa) katika hali iliyopita na hisia za sasa (kueleza ukweli) kwa hivyo, ni tendo moja lililokamilika, si neno la wakati wa sasa, "anawapenda" ila ni neno la wakati uliopita "aliwapenda". Sasa, kabla uanze kuogopa, upendo wake UNAPATIKANA kwa kila mtu, hata kwa mtu mwovu zaidi, hili ni kweli. Ni lazima uelewe kuwa Yesu alikufa kama ***SADAKA YA DHAMBI,*** na si kifuniko cha kimiujiza kwa wale wanaochagua kutenda dhambi kihiari.

Kitendo ambacho Yesu alikifanya Msalabani SI kuchukua nafasi ya mtu yeyote, ILA kujitoa mwenyewe kama SADAKA YA DHAMBI. ***Waebrania 9:14 "damu ya Kristo ambaye kwa njia ya Roho wa milele ALIJITOA mwenyewe kwa Mungu kama sadaka isiyokuwa na doa, itazisafisha dhamiri zetu zaidi sana kutokana na matendo yaletayo kifo, na kutuwezesha kumtumikia Mungu aliye hai?"***

Mbona Yesu alifanya hili? Kumkomboa binadamu na kumwondoa kwenye giza na kumwelekeza kwenye Mwangaza, kutoka kwenye nguvu za Shetani hadi kwa Mungu! ***Matendo ya Mitume 26:18 "Ninakutuma ukawafungue macho yao ili watoke kwenye giza waingie nuruni na watoke katika nguvu za shetani wamgeukie Mungu; ili wapokee msamaha wa dhambi na wapate nafasi pamoja na wote ambao wanatakaswa kwa kuniamini."***

Kwa kweli Mungu alifanya haya katika wakati uliopita akiwa na upendo kwa dunia iliyojaa dhambi kwa kuwapa Mwokozi, hilo ni dhahiri. Ila haiashirii kuwa Mungu anawapenda watu wote bila masharti. Maandiko yanasema kinyume chake kabisa. Yanasema kuwa Mungu huwa hapendi wanadamu waovu na anasikitika kuwa aliwaumba. Ukweli huu unafaa kuelezwa, si kufichwa kwa uongo kama "kanisa" linalokiri linavyofanya sasa.

***Mwanzo 6:5-6 " Mwenyezi-Mungu alipoona wingi wa uovu wa binadamu duniani, na kwamba kila analokusudia binadamu***

***moyoni mwake ni ovu daima, Mwenyezi-Mungu ALISIKITIKA SANA KWA KUMUUMBA BINADAMU DUNIANI. Mwenyezi-Mungu alihuzunika sana moyoni mwake"***

Mtu anaweza kusema kuwa hata kama Mungu anasikitika kuwa alimuumba mwanadamu, bado anawapenda katika uovu wao. Unajua ... " **Mungu anachukia dhambi, lakini anapenda mwenye dhambi."** Shida ni kuwa msemo huu unaotumika sana si wa kimaandiko na ulizungumzwa na mmoja wa watu waovu zaidi duniani, Mahatma Gandhi.

Gandhi, mfanyakazi wa dhambi, alisoma maandiko mengi ya kidini na alikuwa chukizo kwa Mungu Mmoja wa Kweli (Yesu). Aliamini miungu mingi na makufuru nyingi.

*"Wakati alipokuwa Afrika Kusini, pamoja na maandiko na misemo ya uhindu na dini zingine za kihindi, Gandhi alisoma maandiko yaliyotafsiriwa ya Kikristo kama Biblia, na Kiislamu kama Kurani. Misheni ya wafuasi wa Quaker Afrika Kusini ilijaribu kumbadilisha awe Mkristo. Gandhi alijiunga nao katika maombi na kujadiliana nao Theolojia ya Kikristo, lakini alikataa kubadilika kwa kusema kuwa hakuamini theolojia ile au kuwa Kristo alikuwa ndiye mwana wa pekee wa Mungu.*

*Masomo yake ya ulinganisho wa dini na ushirikiano wake na wasomi, ulimfanya kuheshimu dini zote na pia kumfanya kuwa na wasiwasi kuhusu kasoro kwa zote na ufafanuzi usiofaa wa mara kwa mara. Gandhi alipendelea Uhindu na aliita Bhagavad Gitaas kuwa kamusi yake ya kiroho na kishwishi kikuu katika maisha yake." [Wikipedia]*

KUNA MASHARTI YA KUPOKEA UPENDO WA MUNGU. Ikiwa tunataka kupendwa na Mungu, ni lazima ***“tutii amri zake".*** Hili linasemwa mara kwa mara katika Neno. Mifano michache ambayo Yesu alisema bayana ni:

***Yohana 15:10 "  MKIZISHIKA AMRI ZANGU mtakaa ndani ya pendo langu kama mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake;"***

***Yohana 14:23 "Mtu akinipenda ATASHIKA MAFUNDISHO YANGU NA BABA YANGU ATAMPENDA,"***

***Yohana 14:21 "Mtu ANAYEZISHIKA AMRI ZANGU NA KUZITI MIZA NDIYE ANAYENIPENDA. Na mtu anayenipenda, BABA YANGU ATAMPENDA; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.”***

Maandiko yanasema kwa uwazi mtu ambaye Mungu anampenda...

***Zaburi 146:8 "BWANA huwapenda WENYE HAKI.”***

***Mithali 8:17 "  Nawapenda wale wanipendao.”***

***"... kwa kuwa mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu ... nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na KUZISHIKA AMRI ZANGU." (Kutoka 20:5-6, amri ya pili)***

Kulingana na mistari hiyo, wote ambao hawatii Amri za Mungu wanaeza kuwa na uhakika kuwa Mungu hawapendi (chochote kilicho kinyume na hili ni uongo).
Mkristo bandia anayetenda dhambi ameambiwa tena na tena kuwa: **"Mungu anakupenda na ana mpango mzuri juu ya maisha yako..."** Kwa huzuni, kauli hii ii mbali sana na ukweli; kwani mwisho wao ni maangamizi ya milele. Wale ambao ni "vuguvugu" hawatafika mbinguni (***Ufunuo wa Yohana 3:15-16).***

Mungu huwa hakusikilizi ukiwa kwenye dhambi:

***Yohana 9:31 " Tunajua ya kuwa Mungu hawasikilizi wenye dhambi, lakini huwasikiliza wote wanaomwabudu na kumtii."***

***Isaya 59:1-2 " Msifikiri mkono wa Mungu ni mfupi, hata asiweze kuwaokoeni; au masikio yake yamezibika, hata asiweze kuwasikieni. Dhambi zenu ndizo zinazowatenga na Mungu wenu, dhambi zenu ZIMEMFANYA AJIFICHE MBALI NANYI HATA ASIWEZE KUWASIKIEN.."***

Moja ya ukweli mkuu unaokosa katika "Kanisa kuu" ni kuwa huwa KAMWE hawahubiri ni nini na nani ambaye Mungu anachukia. Kwa kuwa Mungu anachukia kikamilifu na kupenda kikamilifu. Mungu, tofauti na sisi, ni mkamilifu katika sifa zake **ZOTE**. Kwa hivyo, chuki, hasira, na wivu ni kamilifu kabisa zinapoonyeshwa na Mungu.

Kwa mfano, binadamu anapokuwa na wivu, huwa ni ubinafsi ulio na msingi wa kukerwa mwenyewe kwa kupoteza mamlaka, mali, na vilevile kudunishwa. Roho wa wivu mkubwa wa binadamu ni mwovu, na mara nyingi, unamjaa mtu mzima na kutesa waathiriwa! Lakini Mungu anapokuwa na wivu, huwa ni sahihi na kwa wema.

Kuna kiumbe mmoja tu kama Mungu; ambaye ni mkamilifu na mwenye haki. Tofauti na sisi, anaweza kuchukia kikamilifu na kupenda kikamilifu kwa wakati mmoja. Anampenda mwenye dhambi kwani anatamani aweze kutoka kwenye uasi wake na amrudie, na ANATOA huruma, msahama, na namna ya kufanya hivyo. Wakati uleule, anachukia matendo, mwelekeo wa roho, na azimio za wanadamu wabinafsi. Bila watu wabinafsi, hakungekuwa na dhambi duniani; kwa hivyo kuchukia dhambi na si mwenye dhambi ingekuwa haipatani kimawazo. Hili ndilo jambo hasaa linalofanyika ikiwa anawapenda watoto wake.

Watoto wa Mungu waliookoka wanaelewa kuwa kwa kuwa sifa zao si ***kamilifu*** kama za Mungu (kwa hakika ni lazima ziwe kamilifu kibiblia kama wanavyoamuriwa), hakuna msingi wa kuchukia yeyote. Je, Mkristo wa kweli anapenda kwa jinsi gani? Kwa kuwakemea wenye dhambi kama alivyoamuriwa:

***Warumi 19:17 "USIMWEKEE KISASI NDUGU YAKO moyoni mwako, bali upatane daima na jirani yako ili usije ukatenda dhambi."***

***Matayo 5:43-44 "43Mmesikia kwamba ilisemwa: Mpende jirani yako na kumchukia adui yako. 44Lakini mimi nawaambieni, wapendeni adui zenu na kuwaombea wale wanaowadhulumu ninyi"***

***Luka 10:27 " 27Akamjibu, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa nguvu zako zote na kwa akili yako yote. Na, mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe."***

Tunafaa kuchunguza kwa usahihi hali ya sasa ya mwenye dhambi (hukumu ya haki tuliizungumzia kwa kina; inayoitwa "chuki" na wenye dhambi wasiotubu), tuwaonye kuhusu hukumu itakayokuja: na tuwaonyeshe uwepo wa upendo, neema, na msahama kupitia toba na imani katika Yesu Kristo. Ikiwa mwenye dhambi hatatubu, hasira ya Mungu ii juu yake:

***Yohana 3:36 " 36Anayemwamini Mwana anao uzima wa milele; asiyemtii Mwana hatakuwa na uzima wa milele, bali*** *GHADHABU YA MUNGU HUBAKI JUU YAKE."*

***Zaburi 5:5 "Wenye majivuno hawastahimili mbele yako; wewe*** *WAWACHUKIA* ***wote watendao maovu.*** (WENYE DHAMBI)***."***

***Zaburi 11:5 "Mwenyezi-Mungu huwapima waadilifu na waovu;*** *HUWACHUKIA* ***kabisa watu wakatili."***

Sasa kwa sababu unajua kuwa Mungu anapenda na kuchukia kikamilifu, je utakubali ukweli na utubu kutoka kwa hali yako

ya vuguvuvu na kutoamini? Ninaomba uchague barabara nyembamba inayoelekea kwenye UZIMA WA MILELE.

***Mithali 13:18 "Umaskini na fedheha zitampata yeye akataaye kurudiwa; Bali yeye aangaliaye maonyo ataheshimiwa."***

***Mithali 15:10 "Adhabu kali ina yeye aiachaye njia; Naye achukiaye kukemewa atakufa."***

***Mithali 15:31-32 "Yeye asikilizaye maonyo yatoayo uzima***

***atakuwa miongoni mwa wenye hekima.***

***32 Yeye anayedharau maonyo hujidharau mwenyewe,***

***bali yeyote anayekubali maonyo hupata ufahamu."***

***Mithali 17:10 "Lawama hupenya moyoni mwa mwenye ufahamu, Kuliko mapigo mia moyoni mwa mpumbavu. "***

Kumbuka ukweli huu tunapotamatisha sura hii:

*Mungu ni upendo.* **Lakini aliwafukuza Adamu na Hawa kutoka kwenye shamba la Edeni.**

*Mungu ni upendo.* **Lakini alizichanganya lugha za watu eneo la Shinar (Babiloni).**

*Mungu ni upendo.* **Lakini aliangamiza Sodomu, Gormora, Adama, na Zeboimu.**

*Mungu ni upendo.* **Lakini aliokoa mioyo minane tu alipoyatuma mafuriko kuhukumu dunia na mioyo mingine yote ilibebwa kwenye mafuriko.**

*Mungu ni upendo.* **Lakini aliwakubalisha wana wa Israeli kupelekwa utekwani na adui zao.**

*Mungu ni upendo.* **Lakini aliwaangamiza wote ambao hawakumwamini baada ya kuokoa watu kutoka Misri.**

*Mungu ni upendo.* **Lakini aliumba jehanamu mahali ambapo moto hauzimiki. Ni mahali pa giza ya daima na kuna machozi, kilio, na uchungu mwingi.**

Kuwa makini unaposema Mkristo anafaa kuhubiri "upendo" tu au kuwa Yesu, ambaye ni Neno la Mungu, alihubiri tu "upendo". Ni sahihi kusema kuwa "Yesu alihubiri upendo", ila, wengi hawajui upendo halisi wa Mungu, Upendo NA chuki zake ni kamilifu.

**Upendo** ni kutii amri za Mungu.

Je, unajua upendo wa Mungu?

Unajiweka katika upendo wa Mungu?

Ikiwa sivyo, ninaomba uweze kumtafuta **leo.**

# SURA YA 6: TOBA YA KIBIBLIA

"Kanisa" linalokiri linaamini toba ya uwongo inayoenezwa kutoka kwenye madhabahu wiki baada ya wiki. Ninapenda kuiita "toba ya Billy Graham" inayojumuisha "ombi la wenye dhambi" ambalo halipatikani KOKOTE duniani. Ni huzuni hafifu ya kidunia inayoelekeza "toba" hii na haiokoi. Katika sura hii nitaelezea bayana toba ya kweli ya kibiblia ya KUTOKA kwenye dhambi hadi kwenye UTAKASO. Sura hii inaweza pia kuwa usukani unaouhitaji ukuelekeze kwenye toba ya kweli.

Toba ilikuwa muhimu sana katika misheni ya Yesu kama inavyoelezwa kwenye injili zote nne. Kutoka mwanzo mwa huduma ya Yesu duniani hadi tamati, alihubiri toba. Yesu alipoanza huduma yake kama tunavyoona wazi katika Marko na Matayo, aliwaita watu watubu na waamini. ***Marko 1:14-15 Yohana mbatizaji alipokamatwa na kutiwa gerezani, Yesu alikwenda Galilaya akaanza kutangaza Habari Njema za Mungu,*** [15] ***akisema, "Wakati umefika: Ufalme wa Mungu umewasili. Tubuni*** (ACHANENI NA DHAMBI)***, muamini Habari Njema."***

Maneno ya kwanza kabisa ya Yesu kwenye huduma YAKE yalikuwa kuwaita watu watubu. Mitume wa Yesu walifanya vivyo hivyo ***Matayo 4:17 "Tangu wakati huo, Yesu alianza kuhubiri akisema: "Tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia."*** Yesu alieleza kwa uwazi ni nani aliyekuwa

anamwita kwenye toba. ***Luka 5:32 "32Sikuja kuwaita watu wema, bali WENYE DHAMBI, ili wapate kutubu."***

Yesu, kwa hakika aliita MIJI MIZIMA itubu. ***Marko 6:11-12 "11Mahali popote ambapo watu watakataa kuwakaribisheni au kuwasikiliza, ondokeni hapo na kuyakung'uta mavumbi miguuni mwenu kama onyo kwao." 12Basi, wakaondoka, wakahubiri watu watubu."***

Yesu alipokuwa anaondoka dunia, kwa mara nyingine aliweka wazi kuwa wafuasi wake walifaa kuhubiri toba. ***Luka 24:46-48 "46Akawaambia, "Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na siku ya tatu atafufuka kutoka wafu, 47na kwamba ni lazima, kwa jina lake, mataifa yote kuanzia na Yerusalemu yahubiriwe juu ya kutubu na kusamehewa dhambi. 48Ninyi ni mashahidi wa mambo hayo."***

Mtume Yohana alipopokea Kitabu cha Ufunuo kutoka kwa Yesu baada ya ufufuo wake, Yesu kwa mara nyingine tena alizungumza kwenye barua saba kwa makanisa saba na **anawaita watubu mara nane**! Je unaona jinsi toba ilivyo na umuhimu kwa Bwana Yesu na kwa moyo wako?

Waongo wengi wanaamini kuwa Mungu humlazimisha mtu kutubu na kuwa mwanadamu hana usemi kamwe, hawaamini katika uhuru wa matendo. Hawaamini kuwa inabidi mwanadamu atubu na afanye "kazi za kwanza". Biblia inakemea wazushi hawa. ***Ufunuo wa Yohana 2:5 "5Basi, pakumbuke pale ulipokuwa kabla ya kuanguka, UKAYAACHE***

***MADHAMBI YAKO, na kufanya kama ULIVYOFANYA PALE AWALI. La sivyo, naja kwako na KUKIONDOA KINARA CHAKO mahali pake."***

Mtu "huokolewa na neema kwa imani" baada ya toba ya kweli "inayovumilia hadi tamati". Bila toba ya kweli, hakuna Neema. Bila ubadilishaji kamili wa mawazo na moyo, mtu hawezi kuwa na imani ya kibiblia inayohitajika ili kushuhudia wepesi wa Neema.

***Warumi 5:1-2 "1Sasa, kwa vile tumekubaliwa kuwa wadilifu kwa imani, basi, tunayo amani na Mungu kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo. 2Kwa imani yetu, yeye ametuleta katika hali hii ya neema ya Mungu ambamo sasa tunaishi. Basi, tunajivunia tumaini tulilo nalo la kushiriki utukufu wa Mungu."***

***Waefeso 2:5 "5hata, ingawa tulikuwa tumekufa kwa sababu ya dhambi, alitufanya hai pamoja na Kristo. Kwa neema ya Mungu ninyi mmeokolewa."***

Bila Kutubu = Hakuna Mabadiliko = Hakuna Wokovu

Watenda dhambi ni lazima **wanyenyekee** na kwa hivyo kushushwa kwenye sehemu inayoweza kuitwa "chumba cha chini kabisa." Ni kutoka hapa ambapo kuna uwezekano wa "kuinuliwa".

***Luka 14:7-11 "7Yesu aliona jinsi wale walioalikwa walivyokuwa wanajichagulia nafasi za heshima, akawaambia mfano: 8Kama mtu akikualika arusini, usiketi mahali pa heshima isije ikawa amealikwa mwingine mheshimiwa kuliko wewe; 9na mwenyeji wenu ninyi wawili atakuja na kukwambia: Mwachie huyu nafasi. Hapo utaaibika mbele ya wote na kulazimika kwenda kuchukua nafasi ya mwisho. 10Bali ukialikwa kwenye karamu, keti mahali pa mwisho, ili mwenyeji wako atakapokuja akwambie: Rafiki, njoo hapa mbele, mahali pazuri zaidi. Hapo utakuwa umeheshimika mbele ya wote wanaoketi pamoja nawe. 11Kwa maana yeyote anayejikweza atashushwa, na anayejishusha, atakwezwa."***

Tazama masharti yaliyotolewa ya toba hapa. Huu ndio moyo utakaopokea neema yake ila si "mwenye dhambi aliyeokoka" ambaye bado "hutenda dhambi" kihiari kila siku kama "asilimia 99 ya makanisa makuu" wanavyohubiri leo.

***Yakobo 4:6-10 "6Lakini, neema tunayopewa na Mungu ina nguvu zaidi; kama yasemavyo Maandiko: "MUNGU HUWAPINGA WENYE MAJIVUNO*** (WENYE DHAMBI) ***lakini huwapa neema wanyenyekevu." 7Basi, JIWEKENI CHINI ya Mungu; MPINGENI IBILISI naye atawakimbieni. 8MKARIBIENI MUNGU, NAYE ATAKUJA KARIBU NANYI. OSHENI MIKONO*** (ACHENI KUTENDA DHAMBI) ***YENU ENYI WAKOSEFU! SAFISHENI MIOYO yenu enyi wanafiki! 9ONENI HUZUNI, LIENI NA KUOMBOLEZA*** (HAYA NI MASHARTI)***; kicheko chenu na kiwe kilio; na furaha yenu iwe huzuni kubwa. 10NYENYEKEENI mbele ya Bwana, naye atawainueni."***

Kiungo kinachokosa katika “makanisa makuu” ni toba ya kweli ya kibiblia. Hii ni nini? Biblia inaeleza wazi:

***2 Wakorintho 7:10-11 “10Kuwa na huzuni jinsi atakavyo Mungu, husababisha badiliko la moyo, badiliko lenye kuleta wokovu; hivyo hakuna sababu ya kujuta. Lakini huzuni ya kidunia huleta kifo. 11Sasa mnaweza kuona matokeo ya kuona huzuni jinsi Mungu atakavyo: ninyi mmepata kuwa sasa watu wenye jitihada, wenye hoja, mnashtuka na kuogopa, mna bidii na mko tayari kuona kwamba haki yatekelezwa. Ninyi mmethibitisha kwa kila njia kwamba hamna hatia kuhusu jambo hili.”***

Je, umeona toba inajumuisha nini? Si “ombi la watenda dhambi” ambalo “mchungaji” husema “sema maneno haya baada yangu”. Si huzuni ya kiulimwengu ambapo unaenda kwa Mungu kupata unachohitaji kutoka kwake. Ni TAMAA ya KUJITOA kikamilifu kutoka kwenye dhambi na maovu yote, kisha wokovu unafanyika, **Ili toba ya kweli** kufanyika mambo yafuatayo ni lazima yawe yameshatendeka:

1) Msimu wa huzuni nzito kama jinsi anavyotaka dhidi ya dhambi – inalosababishwa na kazi ya Roho wa Kweli ( ***Yohana 16:8).***

2) Mvuto wa imani unaokata ndani ya moyo (Baada ya kuachana na dhambi.

3) Jitihada za KUJITOA kutoka kwenye maovu yote kinyume na matakwa ya Mungu (na kujirudia panapohitajika).

4) Mwao na uwoga unaosababisha tamaa kali ya KUACHANA na dhambi.

5) Kujiidhinisha na USAFI wa moyo ***(2 Wakorintho 7:10-11 & Yakobo 4:7-10).***

Kila tukio la toba kwenye Biblia linafuata mchakato huu. (Usimkubalishe mtu yeyote kukwambia vinginevyo, na kwa kweli watajaribu). DHAMBI inakoma unapotubu ... Mtu wa zamani ANAKUFA hapa ... Ubinadamu unasulubiwa HAPA; SI baadaye kama wengi watakavyokwambia. Tamaa na tabia ZINABADILISHWA hapa (ama hazitawahibadilishwa) KUTII Mungu kunafuata UPYA wa maisha na "***vitu vyote vinakuwa vipya".***

***Warumi 6:4-6 "4Tulipobatizwa tuliungana na kifo chake, tukazikwa pamoja naye, ili kama vile Kristo alivyofufuliwa kutoka wafu kwa kitendo kitukufu cha Baba, sisi pia tuweze kuishi maisha mapya. 5Maana, kama sisi tumeungana naye katika kufa kama yeye, vivyo hivyo tutaungana naye kwa kufufuliwa kutoka wafu kama yeye. 6Tunajua kwamba utu wetu wa kale ulisulubiwa pamoja na Kristo, ili hali ya dhambi iharibiwe, tusiwe tena watumwa wa dhambi."***

***2 Wakorintho 5:17 "17Mtu yeyote akiungana na Kristo HUWA KIUMBE KIPYA, mambo ya kale*** (DHAMBI NA TAMAA ZA DHAMBI) ***yamepita, HALI MPYA IMEFIKA."***

Ikiwa HUJAPITIA haya na HUNA mawazo yoyote yanavyomaanisha, HUJAOKOKA kwenye ROHO. Kwa ufupi, hujazaliwa tena katika toa yako ya uwongo.

Unaweza kuwa kwa kweli ‘UMEMPOKEA’ Kristo, na ‘kuamini’ jina lake (kwa kurudia maneno fulani) lakini shetani PIA huamini. ***Yakobo 2:19 “19Je, wewe unaamini kwamba yuko Mungu mmoja? Sawa! Lakini hata PEPO HUAMINI HILO, NA HUTETEMEKA kwa hofu.”***

Usimkubalishe mtu mwingine yeyote kukwambia vinginevyo, Biblia inaeleza wazi kuwa mtu HUOKOLEWA kwa MATENDO na SI kwa “imani pekee” kama jinsi wengi wanavyohubiri, uwongo. IMANI ya kweli inamaanisha kuwa MWAMINIFU. Wanapinga Maandiko na huwa hawahubiri MAFUNDISHO KAMILI ya MUNGU. ***Matendo ya Mitume 20:27 “27Kwa maana sikusita hata kidogo kuwatangazieni azimio lote la Mungu.”*** Hatuwezi kamwee kutupilia mbali baadhi ya Maandiko ili kutengeneza mafundisho yetu. Ni aidha tuamini yote au tusiamini yote. ***Yakobo 2:24 “24Mnaona basi, kwamba mtu hukubaliwa kuwa mwadilifu kwa matendo yake na si kwa imani peke yake.”*** Sehemu ya MATENDO yake INAANZA na TOBA hii (“kujisafisha” kama inavyoelezwa katika ***2 Wakorintho 7:11*** na “kujiosha mikono” kama inavyoelezwa katika ***Yakobo 4:8,*** n.k.).

***Matendo ya Mitume 26:20 “20Ila nilianza kuhubiri kwanza kwa watu wa Damasko, halafu kwa wale wa Yerusalemu na nchi yote ya Yudea, na pia kwa watu wa mataifa mengine.***

***Niliwahimiza WAMGEUKIE MUNGU na KUONYESHA KWA VITENDO KWAMBA WAMEBADILISHA MIOYO YAO.*** (MATENDO)***."***

(Contemporary Christian Music) tembelea **(https://eternalevangelism.com/ccm),** kwa somo la maana ya ibada ya kweli ya kibiblia, tembelea **(https://eternalevangelism.com/instruments).**

***Luka 16:15 "15Hapo akawaambia, "Ninyi mnajifanya wema mbele ya watu, lakini Mungu anaijua mioyo yenu. Kwa maana kile kinachoonekana kuwa kitukufu mbele ya watu, Mungu anakiona kuwa takataka."***

Usifanye kosa lolote kuhusu hili, maridhiano haya madogo yanafaa kukemewa mara moja. Siwezi kukumbuka ni kwa mara ngapi ambazo nimeona na kushauri watu walioridhiana na mambo haya, na punde si punde, wengi wanajipata kwenye ukengefu kamili au ndani kwenye uwongo wa kiukumeni wa "Kanisa Kuu" wakielekea kwenye moto wa mateso. Ni huzuni kubwa na yote inatokana na kuwa na mwelekeo wa kuwaheshimu watu na "kutopenda jirani yako" kwa uhalisi.

***Matendo ya Mitume 10:34-35 "34Hapo Petro akaanza kusema: "Sasa nimetambua kwamba hakika Mungu hana ubaguzi. 35Mtu wa taifa lolote anayemcha Mungu na kutenda haki anapokelewa naye.."***

Ni lazima umwogope Mungu, ila si binadamu.

***Matayo 10:28 "28Msiwaogope wale wauao mwili, lakini hawawezi kuiua roho. Afadhali zaidi kumwogopa yule awezaye kuuangamiza mwili pamoja na roho katika moto wa Jehanamu."***

Labda hutaki kumkasirisha rafiki au mwanafamilia? Ikiwa ndivyo, basi haupo pamoja na Kristo na kwa hakika wewe umejawa na chuki. Wacha tutazame maana ya upendo kwenye Biblia. Majeraha hupona, mabusu huua.

***Mithali 27:5-6 " Afadhali mtu ANAYEKUONYA waziwazi, kuliko yule afichaye upendo. MAKARIPIO YA RAFIKI YAONESHA UAMINIFU, LAKINI BUSU*** (MARIDHIANO) ***la adui ni udanganyifu."***

Ni lazima TUPENDE KWA KWELI kama tulivyoamurishwa. ***2 Timotheo 4:2 " 2hubiri huo ujumbe, sisitiza kuutangaza (iwe ni wakati wa kufaa au wakati usiofaa), karipia, onya na himiza watu ukiwafundisha kwa uvumilivu wote. "***

Waunge waovu, au, usiwaite kamwe kutoka kwenye dhambi zao (nyamaza “ili udumishe amani”), na una hatia.

***Mithali 24:23-25 " Hii pia ni misemo ya wenye hekima:***

***Kuonyesha upendeleo katika hukumu si vyema:24 Yeyote amwambiaye mwenye hatia, “Wewe huna hatia,” Kabila zitamlaani na mataifa yatamkana. 25Bali itakuwa vyema kwa wale watakaowatia hatiani wenye hatia, nazo baraka tele zitawajilia juu yao."***

Kuwaunga mkono wanaotenda dhambi hukupa tiketi ya kuelekea kwenye moto wa mateso.

***Mithali 17:15 " Yeye asemaye kwamba asiye haki ana haki; naye asemaye kwamba mwenye haki hana haki;** HAO WOTE WAWILI NI CHUKIZO **kwa** BWANA."*

***Mithali 11:18-21 " Mtu mwovu hupata ujira wa udanganyifu,***

*BALI YEYE APANDAYE HAKI HUVUNA TUZO YA UHAKIKA.*
***19 Mtu mwenye haki kweli kweli hupata uzima,***

***bali yeye afuatiliaye ubaya huendea kifo chake.***
***20 Bwana huwachukia sana watu wenye moyo wa upotovu,***

***bali** HUPENDEZWA NA WALE AMBAO NJIA ZAO AZINA LAWAMA. **21 Uwe na hakika na hili: Waovu hawataepuka kuadhibiwa,** BALI WENYE HAKI WATAKUWA HURU."*

upendo ni kukemea dhambi na kuwaonya kuwa hata dhambi moja tu la hiari linamwelekeza mtu kwenye moto wa mateso wa milele.

***Marko 10:19-22 " 19Unazijua amri: Usizini; Usiue; Usiibe; Usitoe ushahidi wa uongo; Usidanganye; Waheshimu baba na mama yako." 20Naye akamjibu, "Mwalimu, hayo yote nimeyazingatia tangu ujana wangu." 21Yesu akamtazama, akampenda, akamwambia,*** (AKAMKEMEA) ***"UMEPUNGUKIWA NA KITU KIMOJA: nenda ukauze vitu ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo nifuate." 22Aliposikia hayo, alisikitika, akaenda zake akiwa na huzuni, kwa maana alikuwa na mali nyingi. "***

Ukimwona mtu “akiyarudia mambo ya kale”, ni lazima umpende na umkemee kwa matumaini kuwa atatubu.

***Waebrania 10:38 " 38Lakini mtu wangu aliye mwadilifu ataamini na kuishi; walakini akirudi nyuma, mimi sitapendezwa naye."***

Mfalme Daudi alijua maana ya upendo wa kimungu.

***Zaburi 141:5 " Afadhali MTU MWEMA anipige kunionya; lakini sikubali kamwe kusifiwa na wabaya, maana nasali daima dhidi ya maovu yao."***

**PIGA = H1986 hâlam [haw-lam'] kupiga, kugongelea (kwa nyundo), kushinda, kuchapa, kuvunja.**

Ikiwa mtu mwema atanipiga kwa ukali wa maneno, nitalichukulia kama tendo la ukarimu na wema; kwa mkono mwingine, maneno matamu (upendo wa uwongo) wa “mwenye dhambi aliyeokoka), yaliyo laini kama mafuta, yanajeruhi kushinda mikuki yenye makali, naomba Mungu anilinde kutokana nayo. Au, kwa maneno mwngine, ni afadhali nikatwe kwa maneno makali (yaliyo na uwezekano wa kuponya roho yangu na kwa maombi kunielekeza kutubu na kuachana na dhambi zangu) ya mtu mtakatifu kuliko kupakwa mafuta kwa maneno yasiyo na heshima ya “wakristo wema” waliojawa na uovu  na wanaohubiri “upendo” wa uongo unaolaani.

UTAKUWA UMECHELEWA SANA YESU ATAKAPORUDI AU UTAKAPOPUMUA PUMZI YA MWISHO!

***Yohana 16:8-11 " 8Naye atakapokuja atawathibitishia*** (YESU) ***walimwengu kwamba WAMEKOSEA KUHUSU DHAMBI, UADILIFU na HUKUMU YA MUNGU. 9Wamekosea kuhusu dhambi kwa sababu hawaniamini; 10kuhusu uadilifu, kwa sababu naenda zangu kwa Baba, nanyi hamtaniona tena; 11KUHUSU HUKUMU kwa sababu mkuu wa ulimwengu huu*** (Shetani) ***amekwisha hukumiwa. "***

***Ufunuo wa Yohana 22:11 " 11Kwa sasa anayetenda mabaya na aendelee kutenda mabaya, na aliye mchafu aendelee kuwa mchafu. Mwenye kutenda mema na azidi kutenda mema, na aliye mtakatifu na azidi kuwa mtakatifu."***

Kukemea kunakubalika na vilevile kufunga nira ("kushirikiana") na wenye dhambi. ***Ephesians 5:11 "And have NO FELLOWSHIP with the unfruitful works of darkness*** (SINNERS)***, but rather REPROVE THEM."***

Scripture is given for reproof and correction. Never be a coward and not use it when commanded.

***2 Timotheo 3:16 " 16Maandiko yote Matakatifu yameandikwa kwa uongozi wa Mungu, na yanafaa katika kufundishia ukweli, kuonya, kusahihisha makosa, na kuwaongoza watu waishi maisha adili,"***

Ni bora kutembea peke yako kuliko kutembea na wajinga mia moja watakaokuelekeza kwenye moto wa mateso. Kuwa na imani kuwa Yesu atakupa kila kitu; si vitu tu vya haja za kimwili mbali pia manabii wakimungu ambao unaweza kushirikiana nao. Hili linatuelekeza katika sura inayofuata itakayoeleza jinsi Mkristo hafai kuwa ***"rafiki wa wenye dhambi".***

## SURA YA 11: YESU HAKUWA RAFIKI WA WENYE DHAMBI

Kuna misemo mingi inayotumika sana katika ulimwengu wa makanisa ya leo na kwa mara mingi huwa ni uongo tu wa kuwavutia wanaotenda dhambi kihiari wengi zaidi wenye hamu kubwa. Mojawapo wa misemo hii ni kuwa ***"Yesu ni rafiki wa wenye dhambi".*** Maana ya rafiki ni: *"anayempenda mtu mwingine, anayeburudisha mtu mwingine kuonyesha heshima na upendo, inayoelekeza kwa hamu ya kutaka kutumia muda naye, na kutaka kumzidishia furaha na ufanisi; kinyume na adui."*

***Mithali 17:17 "Rafiki hupenda wakati wote."***

Kuna sehemu yoyote katika vitabu vyote 66 vya Biblia panapotaja kuwa Mungu ni rafiki wa wanaotenda dhambi? Kwa uhakika na uwazi, hakuna! Ila "Wakristo" wengi wanaokiri husema kuwa hili ni kweli. Wametengeneza "mungu" anayelingana na mtindo wao wa maisha na utamaduni wao ambaye hakaribiani na Mungu wa Biblia. Wanapoonyeshwa Mungu wa kweli, hawamjui na wanamwita mtu anayewashuhudia mchukivu, wazimu, pinduani, n.k. Wanawadharau Wakristo wa kweli kuliko madharau yatokao mapagani!

***Waebrania 7:26 " 26Basi, Yesu ndiye Kuhani Mkuu ambaye anatufaa sana katika mahitaji yetu. Yeye ni mtakatifu, hana hatia wala dhambi ndani yake; HAYUMO KATIKA KUNDI LA WENYE DHAMBI na ameinuliwa mpaka juu mbinguni. "***

“***hayumo katika kundi la wenye dhambi***” – Yesu hakujihusisha na watu hawa hivi. Hakushiriki katika hisia zao, mipango, raha (mifano ya sasa ni vilabu, baa, michezo ya kibiashara, sinema za Hollywood n.k.). Ingawa alijichanganya nao, ilikuwa tu kuwafanya mema (kuwaita watubu), na katika maisha yake yote, kulikuwa na utengano kamili kutoka kwenye hisia, kanuni, na maoni ya walimwengu watenda dhambi. Ilikuwa vivyo hivyo kwa ndugu waongo.

***1 Wakorintho 5:11 " 11Nilichoandika ni hiki: msishirikiane na ndugu Mkristo aliye mzinzi, mchoyo, mwenye kuabudu sanamu, mchongezi mlevi na mlaghai. Mtu wa namna hiyo, hata kula msile naye."***

Nyingi za ***miziki ya kisasa ya “Kikristo”*** huimarisha shetani: uongo wa kishetani. Mmoja wa wimbo kama huo no wa Casting Crowns’ "Yesu, Rafiki wa Wenye Dhambi”. Waongo kama hawa hudai kuwa Yesu anapenda kila mtu. Watasema mara kwa mara kuwa “Yesu ni rafiki wa wenye dhambi”? Umbali wa kiasi gani ambao waongo hawa wapo kutoka kwa ukweli?

Katika ***Yohana 15:14,*** Yesu anasema kwa uwazi ni watu wagani hasa walio marafiki wake. Tazama kwa makini kwani huwezi kuepuka Neno Takatifu la Mungu. ***Yohana 15:14 " 14Ninyi ni rafiki zangu MKIFANYA NINAYOWAAMURU. "*** Je wenye dhambi mtii Yesu? Hapana wao ni ***"watoto wa kutotii"***.
***Waefeso 2:2 “2Wakati ule mliishi kufuatana na mtindo mbaya wa ulimwengu huu, mkawa mnamtii mtawala wa pepo wenye nguvu wa anga, pepo ambao huwatawala sasa watu wasiomtii***

***Mungu.”***. Ghadhabu ii juu ya watenda dhambi hawa*. **Waefeso 5:6 “6Msikubali kudanganywa na mtu kwa maneno matupu; maana, kwa sababu ya mambo kama hayo ghadhabu ya Mungu huwajia wote wasiomtii.”*** Na ***Wakolosai 3:6 6Kwa sababu ya mambo hayo hasira ya Mungu huwajia wote wanaomwasi.*** *”.* Kwa hakika tunaweza kumaliza mjadala huu sasa ivi. Yesu anaeleza kwa uwazi watu ambao ni rafiki zake. Wacha tuendelee kudhihirisha kuwa Yesu SI rafiki wa wenye dhambi.

***Yohana 9:31 " 31Tunajua kwamba Mungu hawasikilizi watu wenye dhambi, ila humsikiliza yeyote mwenye kumcha na kutimiza mapenzi yake.”***

Mungu hata huwa **hawasikilizi** wenye dhambi ila watubu kwa kweli ***(wakiri NA waache dhambi zao).*** Tulizungumza kuhusu toba ya kweli katika sura ya sita. Msemo kuwa Yesu ni “rafiki wa watenda dhambi” si wa kimaandiko na haujafunzwa kwenye Biblia, mahali popote. Wacha tuangalie chanzo na upuuzi wa kauli kama hii.

Viongozi wa kidini wakati Yesu alitembea duniani walidai kuwa Yesu alikuwa “rafiki wa wenye dhambi” kama njia ya kumhafifisha mbele ya watu. Hii ni hukumu ya uongo! ***Matayo 11:19 “19Mwana wa Mtu akaja, anakula na kunywa, nao wakasema: Mtazameni huyu, mlafi na mlevi, RAFIKI YAO WATOZA USHURU NA WAHALIFU! Hata hivyo, hekima ya Mungu inathibitishwa kuwa njema kutokana na matendo yake.”*** Ikiwa unaamini kiwa Yesu alikuwa rafiki wa wenye dhambi, basi ni lazima uamini kuwa alikuwa mlafi na mlevi, na

hilo pia ni kufuru! ***Luka 7:34 "34Akaja Mwana wa Mtu; anakula na kunywa, mkasema: Mwangalieni mlafi huyu na mlevi; rafiki ya watoza ushuru na wenye dhambi!"*** Wazushi hawa walikuwa wanamdhihaki na yote waliyoyasema yalikuwa **UWONGO!**

Wahayudi walijua wazi kuwa Yesu **hakuwa** rafiki wa watenda dhambi. Alikasirishwa na waovu "kila siku": ***Zaburi 7:11 "Mungu ni hakimu wa haki; kila siku hulaumu maovu."*** Na dhambi ambazo "***dhambi zimewatenganisha"*** na Mungu. ***Isaya 59:2 "Dhambi zenu ndizo zinazowatenga na Mungu wenu, dhambi zenu zimemfanya ajifiche mbali nanyi hata asiweze kuwasikieni.***" Watenda dhambi kihiari ("wokovu watenda dhambi") humlilia Mungu na huwa hawasikii. ***Mika 3:4 "Ndipo watakapomwomba BWANA, asiwaitikie; naam, atawaficha uso wake wakati huo, kwa kadiri walivyotenda mabaya kwa matendo yao."***

Walikuwa wanamshtaki kuwa alikuwa ***anashirikiana na giza*** ambalo lingemfanya mshiriki wa giza ile. Ni wazi kuwa watakatifu hawafai kuwa na ushirikiano na watenda dhambi (wasioamini); hili ni kweli kwa Yesu pia.

***2 Wakorintho 6:14-18 " 14Msiambatane na watu wasioamini. Je, wema na uovu vyapatana kweli? Mwanga na giza vyawezaje kukaa pamoja? 15Kristo anawezaje kupatana na Shetani? Muumini ana uhusiano gani na asiyeamini?***

***16Hekalu la Mungu lina uhusiano gani na sanamu za uongo? Maana sisi ni hekalu la Mungu aliye hai. Kama Mungu mwenyewe alivyosema: "Nitafanya makao yangu kwao, na***

***kuishi kati yao; Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu." 17Kwa hiyo Bwana asema pia: "ONDOKENI KATI YAO, mkajitenge nao, msiguse kitu najisi, nami nitawapokea.***
***18Mimi nitakuwa Baba yenu, nanyi mtakuwa watoto wangu, waume kwa wake, asema Bwana Mwenye Uwezo. "***

Wazushi hawa pia walisema kuwa Yesu ni Beelzebuli aliyekuwa anaemdeshwa na nguvu za shatani. Je, tunafaa kuamini kuwa kauli hizi pia ni za kweli? KWA HAKIKA HAPANA! Uzushi wa “Yesu ni rafiki wa watendadhambi” ulikusudiwa kupinga utakatifu wake. Tunaona kwa uwazi kuwa urafiki na DUNIA unakufanya kuwa ADUI wa MUNGU. Mungu (Yesu) kwa kweli hawezi kujipinga.

***Yakobo 4:4 " 4Ninyi ni watu msio na uaminifu kama wazinzi. Je, hamjui kwamba kuwa rafiki wa ulimwengu ni kuwa adui wa Mungu? Yeyote anayetaka kuwa rafiki wa ulimwengu anajifanya adui wa Mungu."***

***Warumi 8:7 " 7Maana, mwenye kutawaliwa na fikira za mwili ni adui wa Mungu; haitii sheria ya Mungu, wala hawezi kuitii.”***

Ikiwa Yesu ni rafiki wa watenda dhambi, na tunajua kwa kweli kuws ***“wote wametenda dhambi”*** kama Biblia inavyosema, basi kimawazo hawezi kuwa na maadui. Yesu akiwa rafiki wa watenda dhambi inahitaji kuwa Mungu ni rafiki wa **watenda dhambi wote'**.

Viongozi wa kidini wa siku hizo **walijua** kuwa kuna tofauti katika maingiliano na Yesu **yaliyowatenda** na **kukaribisha**

wengine. Ilhali Yesu alikuwa rafiki wa watu wengine, hakuwa rafiki wao kamwe. ***Matayo 3:7 "7Lakini alipowaona Mafarisayo wengi na Masadukayo wanamjia ili awabatize, aliwaambia, "Enyi kizazi cha nyoka! Ni nani aliyewadokezea kwamba mnaweza kuiepuka ghadhabu inayokuja?"*** Jesus was quite clear on whom His enemies were. Surely He was not a "friend of sinners".

***Yohana 2:15-16 "15Akatengeneza mjeledi wa kamba, akawafukuza wote nje ya Hekalu pamoja na kondoo na ng'ombe wao, akazimwaga sarafu za wenye kuvunja fedha na kupindua meza zao. 16Akawaambia wale waliokuwa wanauza njiwa, "Ondoeni vitu hivi hapa. Msiifanye nyumba ya Baba yangu kuwa soko!"***

*Mbona?* Kwa sababu viongozi wa kidini walikosa kuleta matunda (yaliyostahili) ya toba. Tulizungumzia kwa kina kuwa ni ubora wa toba ya kweli unaofanya mtenda dhambi apokelewe na Mungu. "***huzuni ya kimungu huleta wokovu kutokan an toba ..."*** Kumbuka wezi wawili msalabani. **Wote** walikuwa watenda dhambi, lakini mmoja *tu* ndiye alkiyepokea wokovu/ushirikiano na Kristo BAADA ya kutubu kwa kweli. Kwa hakika Yesu alijua moyo wake alipokuwa akikiri na kuachana na dhambi zake huku amening'inia msalabani kando ya Yesu.

***Matayo 9:13 " 13Basi, kajifunzeni maana ya maneno haya: Nataka huruma, wala si dhabihu. Sikuja kuwaita watu wema, bali wenye dhambi. "***

Toba si tendo la mara moja (ombi la watenda dhambi) au kuwa na huzuni katika wakati ule. Toba ya kweli ni kukubali dhambi dhidi ya Mungu na kuacha kutenda dhambi tena na kuutafuta utakatifu. Toba ya kweli inaonekan katika mwonekano unachukia dhambi. Tunaona dunia jinsi Yesu anavyoiona tunapomfuata kwa kweli.

Mungu hotoa neema YAKE kwa wanaonyenyekea kinyume na watenda dhambi. ***1 Petro 5:5 "5Kadhalika nanyi vijana mnapaswa kujiweka chini ya mamlaka ya wazee. Ninyi nyote mnapaswa kuwa na unyenyekevu mpate kutumikiana; maana Maandiko Matakatifu yasema: "Mungu huwapinga wenye majivuno, lakini huwajalia neema wanyenyekevu."*** Na wokovu, ambayo wanaotubu huletwa kwa Mungu na kufanywa marafiki wake, huja kwa neema. Kando na toba ya dhambi, sisi ni adui wa Mungu, na ghadhabu yake ii juu yetu ***(Yohana 3:36)*** na bado tunahitaji msahama na wokovu kutoka kwa Mungu. ***Warumi 5:10 " 10Maana, tulipokuwa bado adui zake, Mungu alitupatanisha naye kwa kifo cha Mwanae. Na kwa vile sasa tumepatanishwa naye, ni dhahiri zaidi kwamba tutaokolewa kwa uzima wa Kristo."***

Kuna makosa gani kumwonyesha Mungu kuwa rafiki wa watenda dhambi? Kimisingi, ni uongo unaoelekeza watu wengi kwenye moto wa mateso na tunajua mahali waongo watakapoishia. ***Ufunuo wa Yohana 21:8 " 8Lakini watu waoga, wasioamini, wapotovu, wauaji, wazinzi, wachawi,*** (pamoja na wanaotumia dawa za kulevya) **waabudu *sanamu, na waongo***

***wote**, mahali pao patakuwa ndani ya lile ziwa linalowaka moto na kiberiti; hicho ndicho kifo cha pili.* ("

Tafakari, mtenda dhambi ambaye bado ni "rafiki wa Mungu" hana haja kabisa ya kutubu (kuachana na dhambi) kwa sababu wanaamini tayari wamekubaliwa na Mungu. Inaonyesha mwanadamu kuwa tayari yeye ni "kamili" bila haja ya daktari. ***Matayo 9:12 "12Yesu aliwasikia, akasema, "Watu wenye afya hawahitaji daktari; wanaomhitaji ni wale walio wagonjwa. Sikuja kuwaita watu wema, ila wenye dhambi."*** Shida ni, mtenda dhambi SI kamili; na kwa huzuni, wanak eti kwenye viti kanisani wakidhani kuwa wataoingia mbinguni. Mafundisho haya ya uwongo humfanya binadamu asione umuhimu wa kutubu, ambayo ndio njia tu ya kuweza kuwa rafiki wa Mungu, kwa hivyo kuangamiza roho wa binadamu katika kifo cha milele. Kwa kusoma haya, wengine wanaweza kusema, "lakini mimi ni mwenye dhambi!" Basi jibu la pekee kwako ni kuwa unafaa kutubu kama tulizungumza katika sura ya sita, kisha usome sura ya 14.

Wewe *si* rafiki wa Mungu ikiwa bado upo kwenye dhambi ***(Zaburi 5:4-6; II Wakorintho 6:14-16; Matayo 7:23-24; Yohana 12:46; 1 Yohana 1:6, 2:4).***

Habari Njema kwa watenda dhambi si kwamba Yesu ni rafiki yako, ila kuwa si lazima uwe mtumwa wa dhambi ***(Warumi 6:1-22, 8:2-13; 1 Yohana 3:8-10).*** Unaweza kubadilika, na kupitia mabadiliko haya unaweza kufanya ***rafiki wa Mungu.*** Kwa hakika ninaomba ufuate ushauri wake na uje kwake kwa

masharti yake ila si yako au ya “wachungaji” wako ikiwa hayalingani na maandiko ya Biblia.

## SURA YA 12: KUANGUKA KUTOKA KWA NEEMA

Uongo mkubwa unaosemwa na “kanisa” la wanaokiri ni kuwa “unapookoka utabaki kuwa umeokoka” ama “ulinzi wa milele” ama “uvumilivu wa watakatifu.” Wanauamini uongo aliombiwa Haw na ibilisi kwenye shamba. ***Mwanzo 3:4 “Hutakufa:”*** Haya ni mafundisho ya uongo ambayo pekee yametuma na yanaendelea kutuma mioyo mingi kwenye moto wa mateso na shetani anafurahi. Ni wazi kaisa kuwa mtu anaweza kuupoteza wokovu kwa kurudisha “zawadi hii ya bure” kwa Mungu! Tutadhihirisha uongo huu kutoka kwa Maandiko. Nilipenda uongo huu kutoka mwaka wa 2006 hadi 2012 nilipokuwa naishi kama “mtenda dhambi aliyeokoka” nikifikiri kuwa nitaingia moja kwa moja hadi mbiguni huku “nikianguka kwenye dhambi.” Hakuna mtu yeyote anayechagua kutenda dhambi. Ningeishia kwenye moto wa mateso na ninashukuru Mungu kwa ukweli wake uiofichika na ni lazima tuushiriki.

***Ufunuo wa Yohana 22:19 “Mtu yeyote akipunguza chochote katika maneno ya unabii yaliyomo katika kitabu hiki, Mungu atamnyang'anya sehemu yake katika ule mti wa uzima, na sehemu yake katika mji mtakatifu, ambavyo vimeelezwa katika kitabu hiki.”***

Huwezi “kutolewa” kutoka kwenye “kitabu cha uzima” ikiwa tayari hukuwa ndani. Ikiwa haya hayatoshi, tazama ukweli ufuatao wa kibiblia ulio hapa chini. Ninaomba uje kwenye UKWELI kwani wengi wa “Wakristo” wanaokiri wanaamini uongo wa “ulinzi wa milele” usio na masharti.

Kulingana na Neno la Mungu, HAKUNA ***(BINADAMU)*** anayeweza kukutoa kutoka mikononi mwake:

***Yohana 10:27-30 "27Kondoo wangu huisikia sauti yangu; mimi nawajua, nao hunifuata. 28Mimi nawapa uzima wa milele; nao hawatapotea milele, wala HAKUNA MTU atakayeweza kuwatoa mkononi mwangu. 29Baba yangu ambaye ndiye aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote, wale hakuna awezaye kuwatoa mikononi mwake Baba. 30Mimi na Baba, tu mmoja."***

Kwa hivyo, ni wazi **mtu** mwingine hawezi "FAULU" kumfanya mtu mwingine aanguke kutoka kwa Kristo; hili halijapinga uwezo wa mtu binafsi kujiondoa, au uwezo wa kudanganywa na kuuondokea na kufanya wahitaji kubadilishwa kwenye ukweli. ***"YEYOTE KATI YENU"*** inamaanisha mtu yeyote ambaye ameokoka kwa sasa anaweza ***"kuondokea ukweli".*** Ikiwa hawatatubu na waendelee katika uasi-imani wao, hawajaokolewa kutoka kifo cha milele. Jina la kwanza katika mstari huu linasema, "ndugu". ***Yakobo 5:19-20 "19Ndugu zangu, MMOJA WENU akipotoka kuhusu ukweli, na mwingine akamrudisha, 20fahamuni kwamba, huyo anayemrudisha mwenye dhambi kutoka njia yake ya upotovu, ataiokoa roho yake kutoka kifo, na dhambi nyingi zitaondolewa."***

Mstari huu UNADHIHIRISHA kuwa **"NDUGU"** wanaweza **"KUPOTOKA KUHUSU UKWELI",** ahitaji **"KURUDISHWA"** tena na wanaitwa **"WATENDA DHAMBI"** hadi hapo. **IKIWA** na **IKIWA TU** watatubu kutoka "kupotoka kwenye njia zao", **BASI**

roho **“INAOKOLEWA KUTOKA KIFO”**.  Wacha tuangalie mifano mingine iliyodhahiri zaidi.

***1 Timotheo 1:19 “Watu wengine HAWAKUSIKILIZA DHAMIRI ZAO na hivyo WAKAIHARIBU imani yao.”*** Mioyo hii hapo awali ilikuwa na imani ya kweli, ila wakaanguka kwa ujeuri, lakini hatimaye; kwani meli zilizoharibika haziwezi zikaokolewa baadaye. Huu ni uharibifu kamili wa imani kama vile meli inavyoharibika kabisa inapogonga jabali na kuzama.

***1 Timotheo 6:10, 21 “Watu wengine wametamani sana kupata pesa, hata WAMETANGATANGA MBALI NA IMANI ...”*** ina maanda, tumetangatanga kabisa – tumeondoka kwa njia ya hatari kutoka kwenye dini ya Kristo.

***Luka 8:13 “HUSADIKI KWA KITAMBO TU, na wanapojaribiwa HUKATA TAMAA.”*** Tazama mfano wa mpandaji ***Matayo 13:1-23.***

Je inachukua nini ili mtu asemekane ameondoka kwenye mzabibu? Ninachomaanisha ni, ni nini hasaa kinachofanya mtu “aondoke”? Biblia inasemaaje?

Ulichokifanya labda bila kukiwaza sana labda ni kuanguka kwenye mafundisho hatari ya shetani; hoja moja ya Wakalvanisti, “uvumilivu wa watakatifu” (“P” iliyo kwenye neno TULIP), inatojulikana pia kama Unapookoka Utabaki Kuwa Umeokoka. Kuwa mambo mengi sana yaliyoandikwa kuhusu haya naviona vingumu kuchagua baadhi tu ya

Maandiko ninayoweza kutoa mifano. Kwa hivyo nitatoa baadhi kutoka kwenye agano la kale, baadhi kutoka kwa Yesu, baadhi kutoka kwa Yohana, baadhi kutoka kwa Paulo, baadhi kutoka kwa Luka, na baadhi kutoka kwa Yuda. YOTE yameelekezwa na MUNGU.

Pia ninaweza kutaja kanisa la mwanzo (miaka 325 kabla ya Yesu) kuhusu walichokifunza na kukiamini, kwa sababu HAWAKUWAHI kufunzwa Unapookoka Utabaki Kuwa Umeokoka, ila, walihubiri dhidi yake kwa uwazi.

Je, ni nini kilichowafanya Adamu na Hawa kuacha kufuata mzabibu? Jibu rahisi ni; kuamini uongo uliowafanya watende dhambi. Waliamini kama wengi wanavyofanya leo na katika siku za Noa kuwa hawatakufa kwani "wamehifadhiwa ndani yake" haikujalisha matendo yao. Walitegemea siku zao za zamani kuhifadhi maisha yao ya usoni. Mungu alitoa onyo tofauti katika ***Mwanzo 2:16-17*** "***Mwenyezi-Mungu alimwamuru huyo mwanamume, "Waweza kula matunda ya mti wowote katika bustani; lakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya, usile, maana siku utakapokula matunda ya mti huo, hakika utakufa."***

***Ezekieli 3:20-21 "Tena <u>mtu mwenye haki aiachapo haki yake, na kutenda uovu</u>, nami nikiweka kikwazo mbele yake, atakufa; kwa sababu hukumwonya, <u>atakufa katika uovu wake, wala matendo yake ya haki aliyoyatenda hayatakumbukwa;</u> lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. 21 Bali ukimwonya mwenye haki, kwamba yule mwenye haki asitende dhambi,***

***tena ikiwa yeye hatendi dhambi, hakika ataishi, kwa sababu alikubali kuonywa; nawe umejiokoa roho yako.***

***2nd Mambo ya Nyakati 15:2 "2Naye akatoka kwenda kumlaki mfalme Asa, akamwambia, "Nisikilize, ee mfalme Asa na watu wote wa Yuda na Benyamini! Mwenyezi-Mungu yu pamoja nanyi, ikiwa mtakuwa pamoja naye. MKIMTAFUTA, mtampata, LAKINI MKIMWACHA NAYE ATAWAACHA."***

***Luka 8:13 "13Zile zilizoanguka penye mawe zinaonyesha watu wale ambao wanaposikia juu ya lile neno hulipokea kwa furaha. Hata hivyo, kama zile mbegu, watu hao hawana mizizi maana husadiki kwa kitambo tu, na wanapojaribiwa hukata tamaa."***

MWANA MPOTEVU NI BAYANA PIA ALIPOTEA NA ALIREJESHWA KWENYE SEHEMU YA HAKI BAADA YA TOBA YA KWELI.

***Luka 15:18 "18Nitarudi kwa baba yangu na kumwambia: Baba, NIMEMKOSEA MUNGU, na nimekukosea wewe pia"***

Mwana huyu alionekan kujua kuwa aliacha kuufuata mzabibu. Maandiko yanadhihirisha bayana kuwa alikuwa amekufa na akarudishwa hai ***tena.*** Hii ni picha ya Wakristo ***"wanaoacha kumfuata"*** na ***"wanafanywa hai tena"*** katika maisha haya na kurejeshwa baada ya kutubu.

***Luka 15:24 "24Kwa sababu huyu MWANANGU ALIKUWA AMEKUFA, kumbe yu mzima alikuwa AMEPOTEA, lakini sasa AMEPATIKANA. Wakaanza kufanya sherehe."***

***Luka 15:32 "32Ilitubidi kufanya sherehe na kufurahi, kwa sababu huyu NDUGU YAKO ALIKUWA AMEKUFA, kumbe YU MZIMA; ALIKUWA AMEPOTEA, lakini sasa amepatikana."***

Mwana huyu aliacha kumfuata alipoamini kuwa angeweza kuishi maisha yake binafsi mbali na babake, kwa maneno mengine, alipoamini kuwa hakubidi kumfuata. Yesu anasema:

***Yohana 15:5-6 "5Mimi ni mzabibu, nanyi ni matawi yake. AKAAYE NDANI YANGU, NAMI NDANI YAKE, huyo atazaa matunda mengi, maana bila mimi hamwezi kufanya chochote. 6Mtu yeyote asipokaa ndani yangu hutupwa nje kama tawi litupwalo nje hata likakauka*** (kupungua katika kiroho katika maisha haya)***; watu huliokota tawi la namna hiyo*** (kuwakusanya kwenye wokovu au upotevu katika kifo cha kimwili)***, na kulitupa motoni liungue*** (kifo cha pili, kifo cha kiroho Jehanamu na kwenye Ziwa la moto)."

**"NYINYI NI MATAWI":** Si kazi zenu, si zawadi zenu za usoni, ***NYINYI ni!*** "Ikiwa binadamu" ambaye anaashiriwa na "matawi" hatakaa ndani yake, nini kinachomtendekea? ANATUPWA kama tawi. Kwa sababu Biblia haiainishi mimea kama iliyohai au "yenye uhai" kama wengi wetu tunavyofanya, haisemi mmea unakufa, ila inatumia maneno "kukauka, fifia" inayotoa picha dhahiri kwa kukauka kwa tunda la mzabibu na

uharibifu wa tawi kwa uozo wa tunda lake. Katika ***Yakobo 2:26*** “*__26__**Basi, kama vile mwili bila roho umekufa, vivyo hivyo imani bila matendo imekufa.***” na ***Matayo 10:28*** *__28__**Msiwaogope wale wauao mwili, lakini hawawezi kuiua roho. Afadhali zaidi kumwogopa yule awezaye kuuangamiza mwili pamoja na roho katika moto wa Jehanamu.”***

Ukweli huu (“matawi”) kinyume na wanachokifunza waongo wa Unapookoka utabaki kuwa umeokoka, hauzungumzii dunia. Haya yalizungumza kwa Wanafunzi, kumi na mmoja baada ya Yuda kuondoka kumsaliti Yesu katika chakula cha mwisho. Anawaonya wafuasi hao kuwa mbali na kubaki ndani yake, wafunze haya kwa wanaoamini. Pia, haashirii alichokifanya Yuda kama “akiwa mtu ambaye si mwaminifu” kwani huweezi kuwa vuguvugu, aidha Yuda kwa wakati fulani alikuwa anaamini na akaanguka kama ilivyotabiriwa au hakuwahi mjua Yesu na Yesu “hakuwahi mjua”. Alijulikana na Yesu na akafanya miujiza kwa jina la Yesu, alitoa mapepo, akahubiri injili, na kwa mwonekano alikuwa mtakatifu hadi wanafunzi walijishuku binafsi kama wasaliti kabla kumfikiria Yuda!

Mifano (ilani) kwenye Biblia za watu waliokuwa wameokoka, lakini wakaanguka na kupoteza wokovu wao:

**ANANIA AND SAFIRA** walikuwa wameokoka na roho na mioyo yao ilikuwa moja nay a kanisa (tafadhali soma **Matendo ya Mitume 4:32-5:1)**, hadi wakakubali kudanganya Roho Mtakatifu na wakati huohuo wakauawa (soma **Matendo ya Mitume 5:1-11**). “***Neema kubwa ilikuwa juu yao wote ....”***,

pamoja na Anania na Safira **(Matendo ya Mitume 4:33)**.

***Ezekieli 18:24-26 "24 Bali mwenye haki atakapoghairi, na kuiacha haki yake, na kutenda uovu, na kufanya machukizo yote kama yale afanyayo mtu mwovu, je, ataishi? Katika matendo yake yote ya haki aliyoyatenda halitakumbukwa hata mojawapo. Katika kosa lile alilolikosa, naam, katika dhambi yake aliyoitenda, atakufa. 25 Lakini ninyi mwasema, Njia ya Bwana si sawa. Sikilizeni sasa, Enyi nyumba ya Israeli; Je! Njia yangu siyo iliyo sawa? Njia zenu sizo zisizo sawa? 26 Mwenye haki atakapoghairi, na kuiacha haki yake, na kutenda uovu, akafa katika uovu huo; katika uovu wake alioutenda atakufa."***

**WAFUNZI WENGI** "hawakumfuata Yesu tena". ***Yohana 6:66 66Kutokana na hayo, wengi wa wafuasi wake walirudi nyuma wasiandamane naye tena."*** Wakati mwingine waliamini lakini wakati wa majaribu "wakaanguka". ***Luka 8:13 "13Zile zilizoanguka penye mawe zinaonyesha watu wale ambao wanaposikia juu ya lile neno hulipokea kwa furaha. Hata hivyo, kama zile mbegu, watu hao hawana mizizi maana husadiki kwa kitambo tu, na wanapojaribiwa hukata tamaa." "Walirudi nyuma" (Waebrania 10:26-39).*** Kumpokea na kumkiri hufanya mtu azaliwe tena, kwa hivyo waliomwamini kwa muda walikuwa na neem ya kuanguka kutoka. ***Yohana 1:12 "12Lakini wale wote waliompokea na kumwamini, hao aliwapa uwezo wa kuwa watoto wa Mungu."*** na ***1 Yohana 5:1 "1Kila mtu anayeamini kwamba Yesu ni Kristo, huyo ni mtoto wa Mungu; na, anayempenda mzazi humpenda pia mtoto wa huyo mzazi."***

**IBILISI** hakuwa na dhambi na alitembea katika njia za Mungu kikamilifu kufikia wakati alipotenda dhambi. ***Ezekieli 28:11-17 "11Tena neno la Mwenyezi-Mungu lilinijia: 12"Wewe mtu! Imba wimbo wa maombolezo juu ya mfalme wa Tiro. Mwambie kuwa mimi Bwana Mwenyezi-Mungu nasema hivi: Wewe mfalme wa Tiro ulikuwa upeo wa ukamilifu; ulijaa hekima na uzuri kamili. 13Ulikaa Edeni, bustani ya Mungu. Ulipambwa kwa kila namna ya johari, akiki, topazi, yaspi, zabarajadi, berili, sardoniki, johari ya rangi ya samawati, almasi na zumaridi. Ulikuwa na mapambo ya dhahabu. Yote uliwekewa tayari siku ulipoumbwa. 14Nilimteua malaika kukulinda, uliishi katika mlima wangu mtakatifu na kutembea juu ya vito inavyometameta. 15Uliishi maisha yasiyo na lawama, tangu siku ile ulipoumbwa, hadi ulipoanza kufanya uovu. 16Ufanisi wa biashara yako ulikujaza dhuluma, ukatenda dhambi. Kwa hiyo nilikufukuza kama kinyaa, mbali na mlima wangu mtakatifu. Na yule malaika aliyekulinda akakufukuzia mbali na vito vinavyometameta. 17Ulikuwa na kiburi kwa sababu ya uzuri wako. Uliharibu hekima yako kwa sababu ya fahari yako. Nilikubwaga chini udongoni, nikakufanya kuwa kioja kwa wafalme."*** Alianguka kutoka kwenye mapendeleo ya Mungu na akafukuzwa mbinguni. ***Isaya 14:12-14 "Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa! 13 Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. 14 Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu".*** Akawa mtenda dhambi na mwenye tamaa. ***Yohana 8:44 "44Ninyi ni watoto wa baba yenu Ibilisi na mnataka tu***

***kutekeleza tamaa za baba yenu. Yeye alikuwa muuaji tangu mwanzo; hana msimamo katika ukweli, kwani ukweli haumo ndani yake. Kila asemapo uongo, husema kutokana na hali yake ya maumbile, maana yeye ni mwongo na baba wa uongo."*** Na amekusudiwa kuishia kwenye moto wa mateso kwa alichokuwa kwa uamuzi wake mwenyewe (soma **Ufunuo wa Yohana 20:1-1**). ***Matayo 25:41 "41Kisha atawaambia wale walio upande wake wa kushoto, Ondokeni mbele yangu enyi mliolaaniwa! Nendeni katika moto wa milele aliotayarishiwa Ibilisi na malaika wake."***

**ZAIDI YA THULUTHI YA MALAIKA WATAKATIFU WA MUNGU** waliasi na Ibilisi. ***Ufunuo wa Yohana 12:3 "3Ishara nyingine ikatokea mbinguni: joka kubwa jekundu na lenye pembe kumi na vichwa saba; na kila kichwa kilikuwa na taji."***

***Ufunuo wa Yohana 12:7-12 "7Kisha kukazuka vita mbinguni: Mikaeli na malaika wake walipigana na hilo joka, nalo likawashambulia pamoja na malaika wake. 8Lakini joka hilo halikuweza kuwashinda, na hatimaye hapakuwa tena na nafasi mbinguni kwa ajili yake na malaika wake. 9Basi, joka hilo kuu likatupwa nje. Joka hilo ndiye yule nyoka wa kale ambaye huitwa pia Ibilisi au Shetani. Ndiye anayeudanganya ulimwengu wote. Naam, alitupwa duniani, na malaika wake wote pamoja naye. 10Kisha nikasikia sauti kubwa kutoka mbinguni ikisema: "Sasa ukombozi utokao kwa Mungu umefika! Nguvu na Utawala wa Mungu wetu umedhihirika. Na Kristo wake ameonyesha mamlaka yake! Maana yule mdhalimu wa ndugu zetu, aliyesimama mbele ya Mungu akiwashtaki usiku***

***na mchana, sasa ametupwa nje. 11Ndugu zetu wameshinda kwa damu ya Mwanakondoo na kwa nguvu ya ukweli walioutangaza; maana hawakuyathamini maisha yao kuwa kitu sana, wakawa tayari kufa. 12Kwa sababu hiyo, furahini enyi mbingu na vyote vilivyomo ndani yenu. Lakini, ole wenu nchi na bahari, maana Ibilisi amewajieni akiwa na ghadhabu kuu, kwa sababu anajua kwamba siku zake zilizobakia ni chache.")*** na kukusudiwa kuishia kwenye moto wa mateso na Ibilisi ***(Tazama Matayo 25:41, Isaya 24:21, 2 Petro 2:4) Yuda 1:6-7 "6Na, malaika ambao hawakuridhika na cheo chao, wakayaacha makao yao ya asili, Mungu amewafunga gizani kwa minyororo ya milele wahukumiwe Siku ile kuu. 7Kumbukeni pia Sodoma na Gomora, na miji ya kandokando yake; wenyeji wake walifanya kama wale malaika; walifanya uzinzi na mambo yaliyo kinyume cha maumbile, wakapewa hukumu ya moto wa milele, iwe onyo kwa watu wote.").***

**ADAMU NA HAWA** waliumbwa kwa upendeleo na neema ya Mungu. ***Mwanzo 1:26-31 "Kisha Mungu akasema, "Tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; atawale samaki wa baharini, ndege wa angani, wanyama wa kufugwa, dunia yote na viumbe vyote vitambaavyo." Basi, Mungu akaumba mtu kwa mfano wake; naam, kwa mfano wake Mungu alimuumba. Aliwaumba mwanamume na mwanamke. Mungu akawabariki na kuwaambia, "Zaeni muongezeke, mkaijaze nchi na kuimiliki; muwatawale samaki wa baharini, ndege wa angani, na kila kiumbe hai kitembeacho duniani." Kisha Mungu akasema, "Tazama, nawapeni kila mmea duniani uzaao mbegu, na kila***

***mti uzaao matunda yenye mbegu; mbegu zao au matunda yao yatakuwa chakula chenu. Nao wanyama wote duniani, ndege wote wa angani, viumbe vyote vitambaavyo, naam, kila kiumbe chenye uhai, chakula chao kitakuwa majani yote ya mimea." Ikawa hivyo. Mungu akaona kila kitu alichokifanya kuwa ni chema kabisa. Ikawa jioni, ikawa asubuhi; siku ya sita."*** Walianguka kutoka kwa neema kwa kutenda dhambi na wakapoteza maisha ya milele ambayo wangekuwa nayo ikiwa hawangekuwa wametenda dhambi. (***Mwanzo 2:17, 3:1-19, Warumi 5:12-21). 2 Wakorintho 11:3 "3Lakini naogopa kwamba, kama vile yule nyoka kwa hila zake za uongo alimdanganya Hawa, fikira zenu zaweza kupotoshwa, mkauacha uaminifu wenu wa kweli kwa Kristo".*** Hakuna kitu kinachosemwa kuhusu wokovu wao kutoka kwenye dhambi. Hawajajumuishwa na waaminifu kwenye Agano la Kale katika Waebrania 11. Alikuwa Mwana wa Mungu. ***Luka 3:38 "38mwana wa Enosi, mwana wa Sethi, mwana wa Adamu, aliyekuwa wa Mungu"***, kwa hivyo, ni wazi kuwa kuwa mwana wake si hakikisho kuwa utapata uzima wa milele. Mungu anaahidi kuadhibu kila malaika au binadamu anayetenda dhambi bila kujali uhusiano au kuwa ni mwana wake.
**WAISRAELI WENGI** walikuwa na injili ile ile tuliyo nayo. d the same gospel we have. ***1 Wakorintho 10:1-13 "1Ndugu, nataka mjue kwamba babu zetu wote walikuwa chini ya ulinzi wa lile wingu, na kwamba wote walivuka salama ile bahari. 2Wote walibatizwa katika umoja na Mose kwa lile wingu na ile bahari. 3Wote walikula chakula kilekile cha kiroho, 4wakanywa pia kinywaji kilekile cha kiroho, maana walikunywa kutoka ule mwamba wa kiroho uliowafuata; mwamba huo ulikuwa Kristo***

*mwenyewe. 5Hata hivyo, wengi wao hawakumpendeza Mungu, na maiti zao zilisambazwa jangwani.*

*6Sasa, mambo hayo yote ni mfano tu kwetu; yanatuonya sisi tusitamani ubaya kama wao walivyotamani. 7Msiwe waabudu sanamu kama baadhi yao walivyokuwa; kama yasemavyo Maandiko: "Watu waliketi kula na kunywa, wakasimama kucheza." 8Wala tusizini kama baadhi yao walivyozini, wakaangamia siku moja watu ishirini na tatu elfu. 9Tusimjaribu Bwana kama baadhi yao walivyomjaribu, wakauawa na nyoka. 10Wala msinung'unike kama baadhi yao walivyonung'unika, wakaangamizwa na Mwangamizi! 11Basi, mambo hayo yaliyowapata wao ni kielelezo kwa wengine, na yaliandikwa ili kutuonya sisi, ambao mwisho wa nyakati unatukabili. 12Anayedhani amesimama imara ajihadhari asianguke. 13Majaribu mliyokwisha pata ni ya kawaida kwa binadamu. Mungu ni mwaminifu, naye hataruhusu mjaribiwe kupita nguvu zenu, ila pamoja na majaribu, yeye atawapeni pia nguvu ya kustahimili na njia ya kutoka humo salama.*

*Wagalatia 3:6-14, Waebrania 4:2 “2Maana Habari Njema imehubiriwa kwetu kama vile ilivyohubiriwa kwa hao watu wa kale. Lakini ujumbe huo haukuwafaa chochote, maana waliusikia lakini hawakuupokea kwa imani”.* ila walipotenda dhambi, waliondolewa kutoka kwa Mungu na wakapotea (*Kutoka 32:32-33, Waebrania 4:1-7). Yuda 1:5 “5Nataka kuwakumbusheni mambo fulani ambayo mmekwisha yajua: kumbukeni jinsi Bwana alivyowaokoa watu wa Israeli na kuwatoa katika nchi ya Misri, lakini baadaye aliwaangamiza wale ambao hawakuamini.”*

**SAULI** alibadilisha moyo na akapokea Roho Mtakatifu. ***1st Samueli 10:9-13 "9Ikawa Sauli alipogeuka kumwacha Samweli, Mungu aliubadilisha moyo wa Sauli, na ishara hizi zote zikatimizwa siku ile. 10Walipofika Gibea, akakutana na kundi la manabii. Roho wa Mungu akaja juu yake kwa nguvu, naye akajiunga nao katika kutoa unabii kwao. 11Ikawa wale wote waliomfahamu hapo mwanzo walipomwona akitoa unabii pamoja na manabii, wakaulizana, "Ni nini hiki kilichomtokea mwana wa Kishi? Je, Sauli naye pia yumo miongoni mwa manabii?" 12Mtu mmoja ambaye aliishi huko akajibu, "Je, naye baba yao ni nani?" Basi ikawa mithali, kusema, "Je, Sauli pia yumo miongoni mwa anabii?" 13Baada ya Sauli kumaliza kutoa unabii, alikwenda mahali pa juu."*** na ***1 Samueli 10:21-24 "21Kisha akalisogeza mbele kabila la Benyamini, ukoo kwa ukoo, nao ukoo wa Matri ukachaguliwa. Mwishoni Sauli mwana wa Kishi akachaguliwa. Lakini walipomtafuta, hakuonekana. 22Wakazidi kuuliza kwa BWANA, "Je, huyo mtu amekwisha kufika hapa?"***
***Naye BWANA akasema, "Ndiyo, amejificha katikati ya mizigo."23Wakakimbia na kumleta kutoka huko, naye aliposimama katikati ya watu, alikuwa mrefu kuliko watu wengine wote. 24Samweli akawaambia watu wote, "Je, mnamwona mtu ambaye BWANA amemchagua? Hayupo aliye kama yeye miongoni mwa watu wote."***
***Ndipo watu wakapiga kelele, wakasema, "Mfalme na aishi maisha marefu".*** Sauli alienda kwenye Spiritualismi ***(1 Samueli 28, Walawi 19:31, 20:6).*** Alipoteza Roho Mtakatifu ***(1 Samueli 16:12-23)*** na akafa kifo kilichosababishwa na Mungu. ***1 Samueli 31:1-6 1Basi Wafilisti wakapigana dhidi ya Israeli. Waisraeli***

***wakakimbia mbele ya Wafilisti, na wengi wakauawa kwenye Mlima wa Gilboa. 2Wafilisti wakawasonga Sauli na wanawe kwa nguvu, na kuwaua wanawe Yonathani, Abinadabu na Malki-Shua. 3Mapigano yakawa makali sana kumzunguka Sauli, nao wapiga upinde wakampata na kumjeruhi vibaya. 4Sauli akamwambia mchukua silaha wake, "Futa upanga wako unichome nao, la sivyo hawa jamaa wasiotahiriwa watakuja kunichoma na kunitendea vibaya."***
***Lakini mchukua silaha wake aliogopa na hakuweza kufanya hivyo, basi Sauli akachukua upanga wake mwenyewe na kuuangukia. 5Mchukua silaha wake alipoona Sauli amekufa, naye pia akaangukia upanga wake akafa pamoja naye. 6Basi Sauli, wanawe watatu, mchukua silaha wake na watu wake wote wakafa pamoja siku ile ile.".*** Sauli ***"hakutii amri zake"*** na akatenda dhambi nyingi mbaya kabla ya kifo chake. ***1 Mambo ya Nyakati 10:13-14 "13Sauli alikufa kwa sababu hakuwa mwaminifu kwa BWANA. Hakulishika neno la BWANA, hata akataka shauri kwa mwaguzi kwa ajili ya uongozi, 14hakumwuliza BWANA. Kwa hiyo BWANA alimwua, na ufalme akampa Daudi mwana wa Yese."***

**YUDA** kuna mara moja aliyookolewa kwa sababu alikuwa ***"rafiki anayeaminiwa na Yesu".*** KUMBUKA ili uwe rafiki wa Yesu ni lazima uwe unafuata amri zake, na Yuda wakati ule alikuwa anazifuata. ***Zaburi 41:9 9Hata rafiki yangu wa karibu, niliyemwamini, yule aliyekula chakula change ameniinulia kisigino chake."*** Jina la Kiebrania la neno rafiki ni "batah"– **kumwamini mtu kama vile kuhisi ana amani bila uwoga** na limetumika katika muktadha huu mara 107. Je Yesu angeita mtu yeyote ambaye hajaokoka au shetani, "***Rafiki wangu***

***ninayemwamini***"? Aliitwa kuwahubiri kwani mitume wote walikuwa wametumwa. ***Matayo 10:7 "7Wakati mnapokwenda, hubirini mkisema, 'Ufalme wa Mbinguni umekaribia."*** Alikuwa sehemu ya huduma ya mitume na Mtume pia. ***Matendo ya Mitume 1:16-20 "Ndugu zangu, ilibidi maandiko yatimie yale ambayo Roho Mtakatifu alitabiri kupitia kwa Daudi kumhusu Yuda aliyewaongoza wale waliomkamata Yesu. 17Yuda alikuwa mmoja wetu, kwa maana na yeye alichaguliwa ashiriki katika huduma hii." 18(Basi Yuda alinunua shamba kwa zile fedha za uovu alizopata; akiwa huko shambani akaanguka, akapasuka na matumbo yote yakatoka nje. 19Kila mtu huko Yerusalemu akasikia habari hizi, kwa hiyo wakapaita mahali hapo kwa lugha yao, Akeldama, yaani Shamba la Damu). 20"Kama vile ilivyoandikwa katika kitabu cha Zaburi," 'Mahali pake na pawe ukiwa wala asiwepo mtu atakayekaa humo,'  na," 'Mtu mwingine aichukue nafasi yake.'"***

Yuda alitumwa kama mmoja wa wale kumi na wawili kuwakilisha Yesu Israeli. ***Matayo 10:5-6 "5Hawa kumi na wawili, Yesu aliwatuma akawaagiza, "Msiende miongoni mwa watu Mataifa wala msiingie mji wo wote wa Wasamaria. 6Lakini afadhali mshike njia kuwaendea kondoo wa nyumba ya Israeli waliopotea."*** Alikuwa na Roho Mtakatifu ndani yake. ***Matayo 10:19-20 "19Lakini watakapowapeleka humo, msisumbuke kufikirifikiri mtakalosema, kwa maana mtapewa la kusema wakati huo. 20Kwa sababu si ninyi mtakaokuwa mkinena, bali ni Roho wa Baba yenu atakayekuwa akinena kupitia kwenu."*** Yuda alianguka kwa sababu ya dhambi kutoka kwenye huduma na utume. ***Matendo ya Mitume 1:25 "25ili achukue nafasi ya huduma ya utume ambayo Yuda aliiacha ili aende mahali pake mwenyewe."***

Yuda angewezaje kufanya haya ikiwa alikuwa ibilisi au binadamu ambaye hajaokoka? HAIWEZEKANI! Shetani aliingia Yuda mwishoni mwa huduma ya Yesu, kudhihirisha kuwa hakuwa mtumishi wa shetani wakati wote, mbali ibilisi mwenyewe. ***Luka 22:3 "3Shetani akamwingia Yuda, aliyeitwa Iskariote, mmoja wa wale Kumi na Wawili."*** na ***Yohana 13:2 "2Wakati alipokuwa akila chakula cha jioni na wanafunzi wake, ibilisi alikuwa amekwisha kutia ndani ya moyo wa Yuda Iskariote, mwana wa Simoni, wazo la kumsaliti Yesu."*** Kwa hivyo alirudi nyuma, na akawa mwizi. ***Yohana 12:6 "Yuda alisema hivi si kwa kuwa aliwajali maskini, bali kwa kuwa alikuwa mwivi, kwani ndiye aliyekuwa akitunza mfuko wa fedha akawa anaiba kile kilichowekwa humo."*** Shetani na msaliti. ***John 6:70 "70Ndipo Yesu akajibu, "Je, sikuwachagua ninyi kumi na wawili? Lakini mmoja wenu ni ibilisi."*** Kwa hakika Yuda alikuwa anaonyesha tabia za kishetani wakati ule Yesu anaouzungumzia.

Kumfanya Yuda "mmea" kutoka mwanzo, "shetani" na mtu ambaye hajaokoka ni kupuuza ukweli dhahiri wa Biblia. Alikuwa "ameokka" na alikuwa na ahadi ya maisha ya milele, inavyodhihirishwa katika ***Yohana 17:2*** tunakosoma kuhusu Yesu akitoa uhai wa milele "***kwa wote waliokuwa wamempa***"; kisha katika ***Yohana 17:12*** inasema "***12Nilipokuwa pamoja nao, niliwalinda, wakawa salama kwa lile jina ulilonipa. Hakuna hata mmoja aliyepotea, isipokuwa yule aliyekusudiwa, ili Maandiko yapate kutimia.*** Tazama ***Yohana 7:2 "2Kwa kuwa umempa mamlaka juu ya wote wenye mwili ili awape uzima wa milele wale uliompa."*** Je, haya yanaweza kuelezwa kwa uwazi

kiasi gani tena? Yuda alikuwa amepewa uhai wa milele, zaidi, alikuwa amepewa  Yesu na Yesu alikuwa amewahi kumpa wokovu! Kwa huzuni, aliupoteza.

**WATU WENGI MAKANISANI** walikuwa wameokoka lakini baadaye wakatishiwa na uangamizo wakataapo kutubu. ***Ufunuo wa Yohana 2:5 "5Kumbuka basi ni wapi <u>ulikoanguka</u>! <u>Tubu na ukafanye matendo yale ya kwanza</u>. <u>Kama usipotubu</u>, nitakuja kwako na <u>kukiondoa kinara chako</u> cha taa kutoka mahali pake."***, ***Ufunuo wa Yohana 2:16 "16Basi tubuni! Ama sivyo, nitakuja kwako upesi na kupigana na watu hao kwa upanga wa kinywa changu."*** BWANA anaita watu watubu kutoka kwenye dhambi mara kwa mara. ***Ufunuo wa Yohana 3:3-6 "3Kumbuka basi yale uliyoyapokea na kuyasikia, yatii na ukatubu. Lakini usipoamka, nitakuja kama mwivi wala hutajua saa nitakayokuja kwako.***
***4"Lakini bado una watu wachache katika Sardi ambao hawajayachafua mavazi yao. Wao wataenda pamoja nami, wakiwa wamevaa mavazi meupe, kwa maana wanastahili. 5Yeye ashindaye atavikwa vazi jeupe kama wao, nami sitafuta jina lake kutoka katika kitabu cha uzima, bali nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu na mbele za malaika wake. 6Yeye aliye na sikio na asikie yale ambayo Roho anayaambia makanisa."***

Ni lazima uteseke na ushinde ili kuridhi uhai wa milele. ***Ufunuo wa Yohana 2:10-11 "10Usiogope mateso yatakayokupata. Nakuambia Shetani atawatia baadhi yenu gerezani ili kuwajaribu, nanyi mtapata dhiki kwa muda wa***

***siku kumi. Uwe mwaminifu, hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima.***
***11"Yeye aliye na sikio na asikie yale ambayo Roho anayaambia makanisa. Yeye ashindaye hatadhuriwa na mauti ya pili."*** Usiposhinda, utaishia kwenye moto wa mateso milele. ***Ufunuo wa Yohana 21:7-8 "7Yeye atakayeshinda atayarithi haya yote, Nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu. 8Lakini waoga, wasioamini, wachafu, wauaji, wazinzi, wachawi, waabudu sanamu, pamoja na waongo wote, mahali pao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili."***

**HYMENAYO & ALEKSANDA:** *1 Timotheo 1:18-20* ***"18Mwanangu Timotheo, ninakupa agizo hili, kwa kadiri ya maneno ya unabii yaliyosemwa kukuhusu, ili kwa kuyafuata upate kupigana vile vita vizuri, 19ukiishikilia imani na dhamiri njema ambayo*** *WENGINE WAMEVIKATAA* ***na hivyo,*** *WAKAANGAMIA KWA HABARI YA IMANI YAO.* ***20Miongoni mwao wako Himenayo na Aleksanda,*** *AMBAO NIMEMKABIDHI SHETANI* ***ili wafundishwe wasije wakakufuru."***

**HYMENAYA & FILETO:** *2 Timotheo 2:16-18* ***"16Jiepushe na maneno mabaya, yasiyo na maana, yasiyo ya utauwa, kwa maana hayo huzidi kuwatosa watu katika kukosa heshima kwa Mungu. 17Mafundisho yao yataenea kama kidonda kisichopona. Miongoni mwao wamo Himenayo na Fileto 18ambao*** *WAMEIACHA KWELI,* ***wakisema kwamba ufufuo wa wafu umekwisha kuwako na kupotosha baadhi ya watu."***

**DEMA:** ***2 Timotheo 4:10 "10<u>kwa sababu Dema, kwa kuupenda ulimwengu, AMENIACHA</u> na amekwenda Thesalonike. Kreske amekwenda Galatia na Tito amekwenda Dalmatia."*** Dema anatajwa sana katika ***Wakolosai 4:14*** "***Luka, daktari mpendwa, na DEMA, nawasalimu."*** Pia. Dema aliitwa na Paulo "***mfanyakazi mwenzangu"*** kama ilivyotajwa bayana katika ***Filemoni 1:24 "Marko, Aristarko, DEMA, Luka, watenda kazi wenzangu wanakusalimu."*** Na kisha ***"Ameniacha"*** hapo juu katika ***2 Timotheo 4:10!***

Ni lazima mtu "ajishikilie vuzuri"! ***Ninakuja upesi. Shika sana ulicho nacho, ili mtu asije akaichukua taji yako."*** Tunajua kuwa watu VUGUVUGU huangamia know the LUKEWARM perish. ***Ufunuo wa Yohana 3:16 "16Hivyo kwa kuwa u uvuguvugu, kwamba wewe si baridi wala si moto, nitakutapika utoke kinywani mwangu."*** Kando na mifano hii iliyo hapa juu ya kuondolewa kutoka nkwenye neema ya MUngu kwa sababu ya dhambi, Biblia inaeleza kwa sheria wazi (zaidi ya 1,000 katika Agano Jipya pekee) na ilani za adhabu kwa wale wanaorejelea dhambi. Haya yanaweka wazi kuwa hakuna ahadi na agano lolote zisizo na masharti kwenye Maandiko. Vifungu ambavyo hakuna masharti yanayotolewa moja kwa moja zinaongozwa na mamia ya mistari inayosema masharti ni LAZIMA yafuatwe.

Je, mtu yeyote anawezaje kupinga KUONDOKA na tayari kumetajwa katika Biblia? Kumeandikwa kwa uwazi. Ni WAZI KABISA Sasa na wale wanaopinga labda tayari wameshaondoka. KUANGUKA NI LAZIMA KUFANYIKE KWANZA kabla Yesu arudi ***(2 Wathelasonike 2:3).***

***Matayo 24:10-13 "10Wakati huo, wengi wataacha imani yao, nao watasalitiana kila mmoja na mwenzake na kuchukiana. 11Watatokea manabii wengi wa uongo, nao watawadanganya watu wengi. 12Kwa sababu ya kuongezeka kwa uovu upendo wa watu wengi utapoa, 13Lakini yule atakayevumilia hadi mwisho ndiye atakayeokoka. "***

Tazama mambo ambayo unaweza kuyatumia ili kukemea wazushi waongo wa "ulinzi wote usio na masharti":

WAKRISTO (wale "waliookoka kwa kweli") WANAWEZA:

**- Kuondokea imani (1 Timotheo 4:1)**
**- Kutangatanga kutoka kwenye imani (1 Timotheo 6:10)**
**- Kuiacha imani (1 Timotheo 6:21)**
**- Kuachana na imani (1 Timotheo 5:12)**
**- Kuzamisha imani yetu (1 Timotheo 1:19)**
**- Kuondoka kutoka kwa imani (Wagalatia 5:4)**
**- Kumwacha aliyemwita na kugeukia injili mbadala (Wagalatia 1:6)**
**- Kupokea imani ya Mungu bila mafanikio (2 Wakorintho 6:1)**
**- Kuiacha imani, kuangusha imani ya watu wengine (2 Timotheo 2:18)**
**- Kuondokea ukweli (Waebrania 2:1)**
**- Kuwa na moyo mwovu na usioamini na kuelekeza wengine kuanguka kutoka kwa Mungu anayeishi (Waebrania 3:12)**

**- Kufanywa wagumu kwa uwovu wa dhambi**
**(Waebrania 3:12-14)**
**- Kosa kufikia ahadi ya kuingia mapumzikoni mwake**
**(Waebrania 4:1)**
**- Kuanguka kwa sababu ya kutotii na kutoingia mapumzikoni mwake (Waebrania 4:11)**
**- Kuanguka na kukuwa kuwa haiwezekani kurudishwa katika toba (Waebrania 6:4-6)**
**- Kuendelea kutenda dhambi kihiari na kukotuwa na sadaka ya dhambi (Waebrania 10:26-27)**
**- Kurudi nyuma (Waebrania 10:38)**
**- Kukosa kupata neema ya Mungu (Waebrania 12:15)**
**- Kutangatanga kutoka kwenye ukweli (Yakobo 5:19-20)**
**- Kuiacha njia inayofaa (2 Petro 2:15)**
**- Kuingia ndani yake na kushinda BAADA Ya kuzihepa (2 Petro 2:20-21)**
**- Kubebwa ba makosa ya wasiofuata sheria na kuupoteza udhabiti wao (2 Petro 3:17)**
**- Kutenda dhambi inayosababisha kifo (1 Yohana 5:16)**
**- Kuacha kufuata nafunzo ya Kristo (2 Yohana 1:9)**
**- Kukana imani na kuwa mwovu zaidi ya kafiri**
**(1 Timotheo 5:8)**

MANENO MENGINE YANAYOTUMIKA KUMAANISHA "KUONDOKA":

**- Kuzamisha imani yao (1 Timotheo 1:19-20)**
**- Kuanguka kutoka kwa imani (Wagalatia 5:4)**

**- Kugeuka upande mwingine na kumfuata Shetani (1 Timotheo 5:15)**
**- Kuondokea imani na kufuata mvuto wa roho na mafundisho nya shetani (1 Timotheo 4:1)**
**- Pua wewe utaondolewa ... kama Israeli walivyo (Warumi 11:23)**
**- Kuondoka kwa Mungu anayeishi Milele (Waebrania 3:12-15)**
**- Tuchukuliwa mateka na shetani (2 Timotheo 2:26)**
**- Kutegwa na kushindwa TENA na uchafuzi wa dunia (2 Petro 2:21) (Walitoroka na kisha kurudi kwenye dhambi)**
**- Kama mbwa anayerudi kwenye matapishi yake (2 Petro 2:22)**
**- Kuwa kama nguruwe jike aliyeoshwa anayejitia matopeni**

**(2 Petro 2:22)**
**- MBAYA zaidi kuliko ikiwa hawakuwa wamewahi kuamini**

**(2 Petro 2:21)**

Hivi ndivyo Paulo alivyoandika kujihusu:

***1Wakorintho 9:27 "27la, bali nautesa mwili wangu na <u>kuutumikisha</u> ili nikiisha kuwahubiria wengine, mimi nisiwe <u>MTU WA KUKATALIWA</u>"***

Ikiwa Paulo, akiandika kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu, alikuwa na uhakika kabisa kuwa wokovu wake wa milele ulikuwa "umelindwa milele" bila hatari ya kuwahi kupotezwa,

MBONA aliandika kuwa ALIOGOPA kuwa **MLAANIWA**? Jina **KUTUPWA MBALI** inamaanisha **KULAANIWA** katika Kigriki. Jina lile lile lililotumika katika Warumi 1:28. Kumbuka, yeye ndiye pia aliyeandika mistari yote yenye kauli ya **MASHARTI "IKIWA"**, zinazoeleza kwa uwazi kuwa ili upate uzima wa milele kuna masharti unayofaa kutimiza. **IMANI TENDAJI katika Kristo.** Wacha tutazame kwa makini maana ya "kutupwa mbali". Maneno yaliyoelekezwa ya Biblia yana maana na yanahitaji kusomwa kila siku.

KUTUPWA MBALI - (KIGRIKI) G96
ἀδκιμος
adokimos
ad-ok'-ee-mos
Kutoka kwa GI (kama sehemu hasi) na G1384; **isiyokuabaliwa**, yaani, **imakataliwa**; kimaana **haina maana** (kihalisi au kimaadili): - kutupwa mbali, kukataliwa, **kutupwa.**

Mungu hakubaliani kabisa na " unapookoka utabaki kuwa umeokok". Mafunzo kamili yanaweza lupatikana hapa **([https://eternalevangelism.com/osas](https://eternalevangelism.com/osas)).**

## SURA YA 13: JE WEWE NI MWANAFUNZI?

Ninapenda kuwaza itakavyokuwa siku ya hukumu Mungu akiniuliza maswali yanayokaribia haya. ***"James, una kitabu cha cheki ya pesa na kitabu cha cheju cha wakati. Wacha tutazame jinsi ulivyoniheshimu katika maeneo haya ukilinganisha na kila kitu kingine na watu wengine."*** Watu wengi sana kuwa watatupwa kwenye moto wa mateso katika siku ya hukumu kwa sababu walitumia zaidi ya muda na pesa Mungu alizowapa kwa ajili yao binafsi na marafiki; kujiburudisha, kununua vitu visivyo vya msingi, likizo ghali, kuwatuma watoto kwenye chuo zinazofunza mambo ya kidunia, masomo yanayochukiza Mungu yanayogharimu makumi ya maelfu ya madola, n.k. badala ya kumhudumia Mungu mtakatifu. Swali ni, je "vitabu vyako vya cheki" vinaonekana aje machoni mwa Mungu?  Je una ***"dini safi na kamili" (Yakobo 1:27),*** au wewe ni ***"rafiki wa dunia" (Yakobo 4:4)?*** Ninaomba iwe sivyo!

Ninataka kukupa changamoto uhakikishe kuwa unatembea kwa njia ya kweli na Yesu jinsi anavyotaka; kama mwanafunzi wa kweli anayetengeneza wanafunzi. Je huwa unawapeleka watoto wako shule za umma zinazofunza uchafuzi usio wa kimungu kama ubinadamu, mabadiliko, hoja ya ushoga, na mengine mengi ambayo Mungu anayachukia? Na je shule ya "Kikristo" ya kibinafsi inayofundisha mafundisho yaliyotengenezwa na watu? Mtu hawezi kutofautisha kati ya shule  "Kikristo" au shule ya umma kwani zote hazifundishi ukweli. Ni lazima ufanye unayofaa kufanya ili uweze kufundishia mtoto wako umependaye nyumbani.

Je Yesu alifanya nini katika miaka yake mitatu duniani? Kwanda katika mbuga za kusisimua na makumbusho ya

“Kikristo”? kuwa na aina zote za “masemina” zinazochukua kiasi kikubwa cha pesa kwa namna iliyo kinyume na mapenzi ta Mungu kutoka kwa “wasio na uwezo”, n.k.? HAPANA! Mchana na usiku alitumia kupenda wengine kwa kuwaita watubu na kuwahudumia.

***1 Yohana 2:6 “6Ye yote anayesema anakaa ndani yake hana budi kuenenda kama Yesu alivyoenenda.”***

Tunajua kuwa Yesu alichukiwa kinyama na kuuawa na “watu wake”, Wayahudi. Manabii walichukiwa na watu wao binafsi. ***Yohana 4:44 “44(Basi Yesu mwenyewe alikuwa amesema kwamba nabii hapati heshima katika nchi yake mwenyewe.)”*** Wote ila Mtume mmoja walichinjwa kwa kuhubiri **“Habari Njema”** (walijaribu kumuua Yohana kwa kumchemsha ndani ya matufa).

Kukuwa mwanafunzi wa Yesu hukugharimu kila kitu. Utapoteza karibu wote wa marafiki na memba wa familia (wote ambao hawajaokoka; na “Wakristo wa Jumapili Asubuhi” wanaokiri na bandia watakuchukia kwa kiasi kikubwa zaidi). Huenda ukapoteza kazi au hata ukaipoteza, ukaenda jela, ukaumizwa kimwili au hata kuchinjwa. Unaweza ukatemewa mate, usiipendwe, uonekane mchukivu, uondolewe kutoka kwenye “Kanisa Kuu”, watoto wako wakugeuke na vilevile wazazi, na wengineo. Je, utavumilia?

Kuna watu wengi katika kila upande wa mtaro huu sawasawa na katika maswala mengine katika Ukristo. Kundi la kwanza

linahusishwa na kujenga “makanisa” makubwa na “memba” wengi. Wana “memba” 100, 500, au 5000 na wanajiskia kuwa wameunganishwa katika njia ya kispesheli na kuuita “umoja”.

Ukweli ni kuwa, ikiwa Neno la Mungu linahubiriwa kwa uaminifu katika ushirika na kuna watu kumi ambao wana moyo wa mahubiri yale, basi kwa kuangalia madhari ya sasa ya Marekani nan chi zinginezo, huo utakuwa ushirika mkubwa. Karibia kila nambari za wanamemba kanisa huongezwa kwa njia zinginezo. Hivi karibuni nilizingatia jinsi mistari hii inavyoeleza njia ifaayo ya kuhesabu memba wa ushirika kinyume na njia za binadamu.

***Numbari 1:1-3 " 1BWANA alisema na Mose katika Jangwa la Sinai, katika Hema la Kukutania, siku ya kwanza ya mwezi wa pili, katika mwaka wa pili baada ya Waisraeli kutoka nchi ya Misri. Akamwambia, 2“Hesabu watu wa jumuiya yote ya Waisraeli kwa kufuata koo zao na jamaa zao, ukiorodhesha kila mwanaume kwa jina lake, mmoja mmoja. 3Wewe na Aroni mtawahesabu kwa migawanyo yao wanaume wote katika Israeli wenye miaka ishirini na kuendelea ambao wanaweza kutumika katika jeshi."***

Ni watu wangapi ambao hata wapo katika nafasi ya kuvaa deraya zote za Mungu na kupigana wakiwa wamevaa mavazi yale kama Maandiko yanavyoamuru katika ***Waefeso 6:10-20?*** Ndani ya ushirika jibu la swali hili NI kiwango halisi cha ushirika.

Ninaamini kwa kweli kuwa Marekani sasa kufuata njia hii ushirika mkubwa utabaki kuwa ushirika halisi wa watu kumi tu na kanisa kubwa kabisa litabaki watu takriban 20. Hakuna mioyo ya kutosha iliyookoka inayotosha kufanya eneo liwe na makanisa mengi makubwa katika mji mmoja. Watu wa Marekani kwa kawaida hudunisha nguvu ya maana ya kuwa Mkristo jatika hali yao vuguvugu na huhatarisha kusababisha Vita vya Ukweli na hawazingatii kuwa ikiwa kwa kweli kuna kikundi ambacho ni kanisa la Kibiblia ambalo linamaanisha kuwa viwango vyao vya maana ya kanisa kubwa, hukumu ambayo wangepata kutoka kwa ushuhuda kama ule itakuwa kubwa kushinda uwezo wao.

Kiasi cha jamii na muungano unaposaidiana kwa njia ya kweli, ya kimungu, ya ushirika wa kimungu huwa haionekani vila. Katika kanisa, mfano lenye memba 200, huwa wanahisi umoja wakiwa na kiongozi mwenye haiba, hujitambulisha na kwaya kubwa na vitu kama hivyo. Lakini kusema ukweli, hawajuani, hawajatubu kwa kweli (kukiri na kuachana na dhambi zote kwa hivyo hata si Wakristo) au hata kujua maswala ya kweli ambayo mtu anayoweza kuwa nayo. Wanapenda kujitambulisha na mahali, kiongozi, na kikundi kikubwa. Lakini la kufurahisha kuhusu haya yote ni kuwa ingawa Mungu anawapenda na anatamani umoja, ni faida ya ziada tu inayotokana na kumpenda na KUMTII Yesu na kuhudumiana, si lengo kivyake.

***Utume mkubwa*** si wa kukutana na kusherekea (ishi “maisha bora sasa hivi”). Ni ***“kuacha yote”*** (***Luka 14:33 “33Vivyo hivyo, ye yote miongoni mwenu ambaye hawezi kuacha vyote alivyo***

***navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.”),*** KUENDA kwa waliopotea na KUWAFANYA WANAFUNZI. Ushirika unafaa kujuana KWA KWELI na kusimama pamoja kusaidiana katika mambo yote. “Kanisa Kuu” la kawaida linalolenga kujenga majengo na kupata memba wengi katika muundo wa kale hugeuza Utume Mkubwa kuwa KUJA badala ya NENDAna uwafanye wanafunzi. Yesu aliwaamuru Mitume KUENDA (kuhubiri) kwa waliopotea. Njia ya kimungu zaidi ya mkutano wa kanisa ni makanisa madogo (pamoja na manyumbani) kwani inakata matumizi na mahali pale panaleta ukaribu mtakatifu zaidi. Kwa hakika, katika sehemu nyingi za dunia, kanisa fiche nyumbani ndio chaguo pekee. Zaidi, hakuna Wakristo wa kweli katika eneo moja linalotosha kutumia kanisa kubwa.

Inabidi tufanye uevanjelisti kama ulivyoelezwa katika ***Luka Sura ya 10*** ambayo Yesu aliwafundisha watu wake kutumia. Walienda NJE ya “kuta 4” za kanisa/ushirika kuwasaidia washirika wengine na kuhudumia wale ambao walikuwa na mahitaji {maskini, wajane, yatima, waliopotea, n.k.). Wakristo wanaokiri sasa hutumia kila raslimali zao kwa kujenga manyumba ya kupendenza na “vitu” za kidunia kuburudisha mioyo iliyopotea, jambo ambalo kanisa la kwanza HALIKUWAHI kufanya. Kwa hakika hatufai kuachana na ushirika na ndugu na mikutano ya kienyeji ya kila wiki Jumapili, haya yameamuriwa pia lakini ni kusoma na kutayarishwa kufanya kazi ya BWANA, si kuburudishwa au “kutiwa moyo”. Mtu aliwa katika ushirika wa kweli, “ni

ushirika wa siku 7 kwa wiki", si saa moja au mawili Jumapili na labda saa mojaa Jumatano usiku.

Kama msimamizi wa wamishenari wa kienyeji katika bara Afrika na Asia, nimeshuhudia muundo wa kanisa la kishirika kote duniani na kusema ukweli, itakuwa ni jambo gumu sana kubadilisha kanisa la kitamaduni kwani mashirika hupinga mabadiliko. Karibu kila mtu anaamini mfumo wa Kikristo wa Kimagharibi wa "jengo ndilo kanisa". Hii ni pamoja na manyumba ya kifahari, mziki wa kisasa "wa kikristo", maduka, na kuvaa mavazi ya kuvutia wanapoenda "kanisani". Wanapenda muundo huu na unapendeza unapokuwa na "kiongozi mmwenye haiba" wanayempenda. Wanaabudu "kiongozi" wanayejitambulisha naye na muundo wa Kimagharibi wa kanisa la kimashirika. Hii ndiyo nafasi mwafaka kabisa ya kiongozi wa kidunia na mahali penye watu wakiwa wameshika sehemu ya katikati. Tunafaa kuwa na kanisa inayoweka KRISTO sehemu ya katikati ila si kanisa iliyo na BINADAMU kama sehemu ya katikati. Kwa kweli kuna viongozi na mpango katika kanisa ya kibiblia, ila si "mabwana" wasio wa kibiblia waliopo makanisano mengi ya leo.

Viongozi (mchungaji/askofu/mzee wa kanisa) wana hukumu kali zaidi kwa hivyo ni muhimu kuwa "wanachaguliwa" kwa makini (kwa hakika watoke kwa Mungu na wanaishi kwa utakatifu). Asilimia zaidi ya "99%" ya walio katika nafasi hizi hawafai kusimamia chochote kile! Ni mbweha wanaotumia sukari kudanganya watu.

*Waebrania 13:7-17 " 7WAKUMBUKENI VIONGOZI WENU, wale waliowaambia neno la Mungu. Angalieni matokeo ya mwenendo wa maisha yao mkaiige imani yao. 8Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele.*
*9MSICHUKULIWE NA KILA AINA YA MAFUNDISHO YA KIGENI. Ni vyema mioyo yenu iimarishwe kwa neema, wala si kwa sheria kuhusu utaratibu wa vyakula, ambavyo havina faida kwa wale wanaozishika hizo sheria. 10Sisi tunayo madhabahu ambayo wale wanaohudumu katika hema hawana haki ya kula vile vitu vilivyowekwa juu yake.*
*11Kuhani mkuu huchukua damu ya wanyama na kuiingiza Patakatifu pa Patakatifu, kama sadaka ya dhambi, lakini miili ya hao wanyama huteketezwa nje ya kambi. 12Vivyo hivyo Yesu naye aliteswa nje ya lango la mji ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe. 13Kwa hiyo basi na tumwendee nje ya kambi, tukiichukua aibu aliyobeba. 14Kwa kuwa hapa hatuna mji udumuo, bali tunautafuta ule ujao.*
*15Basi kwa njia ya Yesu, tuzidi kumtolea Mungu dhabihu ya sifa, yaani, matunda ya midomo inayolikiri Jina*
*lake. 16Msiache kutenda mema na kushirikiana vile mlivyo navyo, kwa kuwa dhabihu kama hizo ndizo zinazompendeza Mungu.*
*17WATIINI VIONGOZI WENU NA KUJINYENYEKEZA CHINI YA MAMLAKA YAO. Kwa maana wao wanakesha kwa ajili yenu kama watu watakaopaswa kutoa hesabu. Watiini ili kwamba wafanye kazi yao kwa furaha, wala si kama mzigo, maana hiyo haitakuwa na faida kwenu. "*

Unapopata ushirika mzuri, hizi ndizo amri. Sasa, ikiwa hakuna yeyote aliye karibu naye, omba uweze kuenda karibu na

mmoja haraka iwezekanavyo. Ni rahisi sana kuanguka unapotembea peke yako.

***Waebrania 10:23-27 "23Tushike kwa uthabiti lile tumaini la ukiri wetu bila kuyumbayumba, kwa maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu. 24TUANGALIANE NA KUHIMIZANA SISI KWA SISI KATIKA UPENDO NA KATIKA KUTENDA MEMA. 25WALA TUSIACHE KUKUTANA PAMOJA, KAMA WENGINE WALIVYO NA DESTURI YA KUKUTANA, TUHIMIZANE SISI KWA SISI KADIRI TUONAVYO SIKU ILE INAKARIBIA.***
***26Kama tukiendelea kutenda dhambi kwa makusudi baada ya kupokea ufahamu wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi. 27Lakini kinachobaki ni kungoja kwa hofu hukumu ya moto uwakao utakaowaangamiza adui za Mungu."***

Kanisa la kwanza lilikuwa muhimu. Ilitafuta mioyo iliyopotea duniani na kufunza mitume kazi ya huduma. Ushirika wa waumini (mikutano ya kanisa) ni wa kutia makali panga zao kwa matayarisho ya KUENDA kufanya wanafunzi na kuishi maisha yenye utakatifu yanayompendeza Mungu; si kwenda kanisa kuburudishwa! Nimeshuhudia kufuru nyingi, kutoka kwa kanisa "wakivaa jezi za timu za michezo wazipendazo" na "kanisa" kufanya sherehe venye uwovu hadi kuleta mchanga wenye uzito wa ratili 25,000 madhabahuni ili kuwa na "Jumapili ya Ufukwenu". pounds of sand brought to the alter to have a "beach Sunday". Ni KICHAA! Kanisa inafaa kutumika kutoa huduam ya neno la Mungu na kufundisha ndugu kufanya uevanjelisti na huduma ya Bwana. Huwezi kufanya wanafunzi ikiwa wewe binafsi si mwanafunzi. Na kama wewe si mwanafunzi hutafika mbinguni.

Kuna gharama kubwa ya kuwa mwanafunzi wa kweli wa Yesu. Mbweha walio katika "Kanisa Kuu" hawatahubiri hili kwa sababu itakuwa watakosa kazi zao.

***Luka 14:25-33 "25Umati mkubwa wa watu ulikuwa ukisafiri pamoja na Yesu, naye akageuka, akawaambia, 26"Mtu ye yote anayekuja kwangu hawezi kuwa mwanafunzi wangu kama hatanipenda mimi zaidi ya baba yake na mama yake, mke wake na watoto, ndugu zake na dada zake, naam, hata maisha yake mwenyewe. 27Ye yote asiyeuchukua msalaba wake na kunifuata hawezi kuwa mwanafunzi wangu. 28"Ni nani miongoni mwenu ambaye kama anataka kujenga nyumba, hakai kwanza chini na kufanya makisio ya gharama aone kama ana fedha za kutosha kukamilisha? 29La sivyo, akiisha kuweka msingi naye akiwa hana uwezo wa kuikamilisha, wote waionao wataanza umdhihaki, 30wakisema, 'Mtu huyu alianza kujenga lakini hakuweza kukamilisha.' 31"Au ni mfalme gani atokaye kwenda kupigana vita na mfalme mwingine, ambaye hakai chini kwanza na kufikiri iwapo akiwa na jeshi la watu 10,000 ataweza kupigana na yule anayekuja na jeshi la watu 20,000? 32Kama hawezi, basi wakati yule mwingine akiwa bado yuko mbali, yeye hutuma ujumbe wa watu na kuomba masharti ya amani. 33Vivyo hivyo, ye yote miongoni mwenu ambaye*** *HAWEZI KUACHA VYOTE ALIVYO NAVYO, HAWEZI KUWA MWANAFUNZI WANGU."*

Yesu alikuwa anawafanya watu kuwa wanafunzi na aliwaamuru wanafunzi wake waende wakafanye wanafunzi zaidi. Huu ndio Utumwa Mkuu kwenye Maandiko. Ni njia yake

ya kupanua Ufalme wa Mungu. Ni lazima uachane na "YOTE" kwanza. Sikiliza amri YAKE iliyodhahiri hapa ***"yeyote miongoni mwenu ambaye hawezi kuacha vyote alivyo navyo,...".***

KUACHA, v.t. pret. forsook; pp. kuachwa. Tazama tafuta.

1. **Kuacha au kuondoka kabisa**; kuacha peke yake, kuondoka kutoka. "marafiki" na waongo hutuacha wakati wa shinda.

"***Waache wajinga, na uishi." Mithali 9.***

2. **Kuacha**; kukataa.

"***Achana na hasira, na ukatae kero." Zaburi 37.***

3. **Kuondoka;** kufeli. Katika hasira, rangi huondokea mashavu. Wakati wa majaribu, usikubali uvumilivu ukuondokee.
4. Katika Maandiko, Mungu kuondokea watu wake, anapoondoa usaidiz wake, au mwangaza wa uso wake.

Huwa hatuskii haya katika "kanisa" la kisasa. Huwa tunasikia kufuru za "ishi maisha bora sasa hivi", "abudu Mungu na upokee baraka za kidunia" (manyumba, magari, likizo ghali, viatu na nguo nyingi, pikipiki, boti, n.k.). Swali la milele; je umekana kwa kweli madai yako kwa vitu VYOTE vya kiulimwengu, pamoja na maisha yako na ukachagua Mungu mmoja, Yesu, na yeye pekee?

Mkristo ni mwanafunzi anayefanya watu wengine kuwa wanafunzi kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Huu ndio Utumwa Mkuu unaozungumziwa katika Biblia. Je, unatimiza Utumwa Mkuu?

***Matayo 28:16-20 "16Wale wanafunzi kumi na mmoja walikwenda Galilaya kwenye ule mlima aliowaagiza Yesu. 17Walipomwona, wakamwabudu, ingawa wengine walikuwa na mashaka. 18Yesu akaja karibu, akawaambia, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. 19Nendeni basi, mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wanafunzi wangu; mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. 20Wafundisheni kushika maagizo yote niliyowapeni. Nami nipo pamoja nanyi siku zote; naam, mpaka mwisho wa nyakati."***

Huwezi kufanya wanafunzi ikiwa wewe si mwanafunzi wa Kristo na kwa hakika utaishia kwenye moto wa mateso. Wengi wa "waumini" wanaokiri husoma kuhusu kuyaacha yote wamfuate Yesu lakini bado wana mguu mmoja bado duniani na hili huwafanya kuwa vuguvugu. Ni uajibikaji wa aidha asilimia mia au asilimia sufuri. Hakuna njia nyingine ya kwenda kwa Yesu. Yesu alimaanisha yote aliyoyasema, kutoka ***Mwanzo 1:1 hadi Ufunuo wa Yohana 22:21.*** Ni lazima uelewe kuwa unahitaji kukana KILA KITU. Yesu anataka ushirikiano wako kamili. Ni lazima uachane kabisa na Ukristo (wa Kanisa Kuu) unaoenda "kanisa" mara moja au nbuku kwa wiki tu. Unahitaji kumfuata Yesu na utii amri zake zote ili kuwa mwanafunzi wa Yesu na kuwafanya wengine kuwa wanafunzi. Hakuna njia nyingine ila njia Yake.

Upande mwingine wa mtaro huu tunaouona kila wakati ni pale watu wanapoacha ushirika kabisa. Hii pia ni hatari. Ikiwa umejawa na Roho Mtakatifu, inabidi ushirikiane na waumini wengine kwa sababu nyingi, baadhi zimetajwa hapo juu.

Wengi wa "Wakristi wa Kanisa Kuu" wanaokiri" si wanafunzi na hawatafika Mbinguni. Ni "waumini" tu. Baadhi ni "wachungaji", "walimu" wa Biblia, walimu wa shule, polisi, wakulima, akina baba, akina mama, n.k. wanaofikiri kuwa kwenda "kanisa" na kuwa katika kikundi kimoja au viwili vidogo ni kuwa mwanafunzi wa Kristo. Wanafikiri kuwa watu waliowaalika wanaohudhuria kanisa mara kwa mara ni wanafunzi pia. Lakini hakuna yeyote kati yao, au wengi miongoni mwa "Wakristo" wanaokiri wamewahi kupewa mwito wa kibiblia wa kuwa mwanafunzi wa kweli na kwa hakika kulipa gharama ya uanafunzi. Mguu mmoja duniani na mguu mmoja kwenye Ufalme ni jambo lisilowezekana, shetani anamiliki ukuta! Mkristo wa kweli na aliyekomaa (ambaye amesoma Maandiko, na kufundishwa na mzee katika imani, n.k.) ana WANAFUNZI. Ikiwa hujafanya ivi, unahitaji kutubu na kuanza kutii Mungu Mkuu, mtengenezaji wa wanafunzi Mkuu. Ninaomba kitabu hiki kimefungua macho yako ikiwa hutembei kama alivyotembea.

Katika ***Luka 14***, kwa mfano, tunaona jinsi Yesu anavyoeleza maana ya mwanafunzi na tunaona wito halisi wa uanafunzi. Yesu hawaulizi watu "waiamini kazi aliyoifanya msalabani" au "waipokee kazi aliyoikamilisha ili waokoke". Hata

hakuwaahidi mbinguni pasipo toba yak we;I na kuvumilia "hadi mwisho katika utiifu."
Yesu aliwaambia wayaache "YOTE" waje wamfuate. Je huyo ni wewe? Umeyaacha "yote" kumfuata Kristo?

Karibia kila mmoja hufunzwa kwa mojawapo ya njia mbili. Wote "waliookoka" ni wanafunzi, au au polepole kwa hakika mtu huwa mwanafunzi kadri anavyokuwa karibu na Yesu kupitia kwa kusoma neno na maombi. Huu ni uongo wa "utakaso endelevu" (mtu anaelekea kuwa mwanafunzi baada ya kipindi cha muda, "tembea alivyotembea"). Kwanini tusitazame alichokifanyaYesu? Tunaamrishwa kutembea kama yeye (***1 Yohana 2:6***) si kwa wakati ujao mbali wakati wa sasa. Si wakati mtu "anapofuzu" katika hali kuu ya kiroho au kutoka kwa seminari au chuo cha Bibilia za kizushi, lakini sasa hivi! Tunapaswa kutazama alichoamuru Yesu wala si mbwa mwitu katika madhabahu wanaopotosha wengi.

Swali: Kwanini tunamwita Bwana na hatutendi anavyotuamuru wala kuzifuata njia zake?

***Luka 6:46 "Kwa nini mnaniita, Bwana, Bwana, nanyi hamfanyi ninayowaambia?"***

Maneno yake ya kwanza baada ya tubuni maana Ufalme wa Mungu umekaribia, ni haya **"NIFUATENI MIMI"**

***Matayo 4:17-19 "Tangu wakati huo, Yesu alianza kuhubiri akisema: "Tubuni, maana Ufalme wa Mbinguni umekaribia.***

***18Wakati Yesu alipokuwa anatembeakando ya Bahari ya Galilaya aliwaona ndugu wawili, Simoni aitwaye Petro na Andrea ndugu yake. Walikuwa wakizitupa nyavu zao baharini kwa maana walikuwa wavuvi. 19 Yesu akawaambia, "NJOONI NIFUATENI, nami nitawafanya muwe WAVUVI WA WATU."***

Kanisa lisilo la kweli huwaita waamini kwa maisha rahisi na "maisha bora sasa hivi" kwa ahadi ya uzima wa milele kwa wale ambao wakati mmoja katika maisha yao waliomba "ombi la watenda dhambi." Hawazungumzii kamwe kuzitii sheria za kimaadili ambazo Yesu anaamrisha na kwa hakika huwezi kuwatofautisha na "ulimwengu" kwa sababu wao ni wa ulimwengu. Hii ndio inaitwa "Mfumo wa Kanisa Chipuka" au kama ninavyoiita "Kanisa Kuu". Linganisha hilo na mwito wa Yesu wa kuacha na kukana yote. Kwa miaka mia tatu kanisa lilipitia mateso kwa sababu ya kukataa kumkana Bwana wao na wakalipia gharama kuu. Walitambulika kwa "***kutembea alivyotembea"***; kuwalisha maskini, kwenda "***ulimwenguni kote"*** kufanya wanafunzi, kuwajali walio wadogo miongoni mwao na kuishi maisha matakatifu. Haya ndio matunda ya watu walioitwa kuwa wanafunzi.

Na kwa hakika "wakristo" wengi "hawakuziacha nyavu zao" na kwenda kuvua mioyo iliyo na dhamana. Petro na Andrea waliacha nyavu zao na kumfuata Yesu. Matayo alipoitwa hakuangalia nyuma katika meza ya watoza ushuru. Ingawaje Zakayo alibaki katika taaluma yake, alibadilisha maisha yake na kuyapa kipaumbele mambo ya Ufalme wa Mungu. "Kanisa" linalokiri huweka kazi na mambo mengine mbele katika maisha yao na itabidi waanze upya kumfuata Yesu

anavyoamrisha au waangamie katika imani yao potovu.

Kama mfanyibiashara pagani kwa muda mrefu wa utu uzima wangu, nilitumia zaidi ya masaa 70 kila wiki kuijenga biashara yangu. Muda wangu mwingi nilitumia katika biashara yangu nijitengenezee pesa zangu binafsi na vile vile za "marafiki" na "kuishi maisha bora sasa hivi" (Ndoto ya Mmarekani). Muda wangu wa ziada ulitumika kufurahisha mwili na wengine nikijaribu kubadilisha maisha ya kweli na takatifu, na "raha". Kwa sasa ninavyomfuata Kristo kwa utiifu kamili (kuishi kitakatifu), ameekeza moyoni mwangu kumfanyia kazi usiku na mchana. Singetaka iwe njia nyingine ile. Jukumu langu ni kumfuata yeye, na sio mipango ambayo nimejitengenezea. Mapenzi yake, na si yangu.

***Isaya 55:6-7 "Mtafuteni BWANA, maadamu anapatikana, mwiteni, maadamu yu karibu:7 Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake, Na amrudie BWANA, naye atamrehemu, Na arejee kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa.8 Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema BWANA. 9 Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu."***

Nilipompa Kristo maisha yangu kikamilifu, niliachana na ile "Ndoto ya Mmarekani". Nikapangua PAKUBWA mipangilio yangu ya kibiashara na nitakwambia, hakuna furaha inayokaribia kumtumikia Mfalme wa Wafalme na Bwana wa

Mabwana. Sasa basi, usichanganye ninachokifundisha hapa, tusipofanya kazi hatupaswi kula kwa mfano ***2Wathesalonike 3:10 "Kwa maana hata tulipokuwa pamoja nanyi, tuliwapa amri ili kwamba: "Mtu yeyote asiyetaka kufanya kazi, wala asile."*** Kwa hivyo ninapohubiri mafunzo ya Bibilia kwa kuacha **KILA KITU**, inamaanisha kwamba unaki kwa maoni kuwa yote ufanyayo ni kwa ajili ya Yesu.
Ni lazima ufanye kazi kwa bidii.

Hakuna chochote ambacho ulimwengu huu unaezakukupa kama kutii mapenzi na amri zake ili mtazamo wa mtu usiwe tena kwa kile cheo kikubwa au kujifanyia kazi binafsi ila kufanya kazi kwa bidii kwa sababu ya Ufalme wa Mbinguni na wengine.  Sina furaha nyingine ninapotumia faida za biashara yangu kuwasaidia wamishonari wa kienyeji wanapowafanya watu wanafunzi na kuwashughulikia mayatima, wajane na walio wadogo miongoni mwao. Wewe pia waweza kuwa na "**AMANI KAMILI"** ikiwa pia utakuwa mwanafunzi hakika na kufanya wengine wanafunzi.

Ikiwa wewe sio mwanafunzi unayefanya wanafunzi, unahitaji kusoma sura ifuatayo (Njia ya Msalabani) na uanze kutoka mwanzo. Kwa upendo wa nafsi yako, ninaomba ufanye hivyo. Mwisho wa jambo hili?

***Mhubiri 12:13-14 " 13 Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa: MCHE MUNGU, NAWE UZISHIKE AMRI ZAKE, MAANA KWA JUMLA NDIYO IMPASAYO MTU. 14Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno***

***la siri, likiwa jema*** (UTAKATIFU WA UHAI WA MILELE) ***au baya*** (DHAMBO INAYOELEKEZA KIFO)***."***

## SURA YA 14: NJIA YA MSALABANI

Nilifurahi sana kuandika kitabu hiki na ninaomba kiweze kukubadilisha. Ninaweza kufikiwa ikiwa una maswali na ninatazamia kuzungumza na wanaomtafuta Yesu Kristo kwa kweli. Kwa upendo wa uzima wa milele, nitamalizia kwa wito wa injili. Hii inahusisha mambo mengi zaidi kuliko "ombi la watenda dhambi" ambalo watu wengi wamelizoea.  Soma kwa makini, unaweza ukawa huna kesho na ukaenda katika hukumu ya mwisho, leo.

Yesu alisema, katika ***Matayo 7:13-14,*** kuwa kuna njia mbili tu za kuchagua, NJIA NYEMBAMBA NA NJIA PANA.

***Matayo 7:13-17 "13Ingieni kwa kupitia mlango mwembamba. Kwa maana njia inayoongoza kwenye maangamizi ni pana, na mlango wa kuingilia humo ni mpana; waendao njia hiyo ni wengi. 14Lakini njia inayoongoza kwenye uzima ni nyembamba, na mlango wa kuingilia humo ni mwembamba; ni watu wachache tu wanaoweza kuigundua njia hiyo. 15Jihadharini na manabii wa uongo. Wao huja kwenu wakionekana kama kondoo kwa nje, lakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali. 16Mtawatambua kwa matendo yao. Je, watu huchuma zabibu katika miti ya miiba, au tini katika mbigili? La! 17Basi,***

***mti mwema huzaa matunda mema, na mti mbaya huzaa matunda mabaya."***

Lakini Yesu akasema wengi watachagua barabara inayochagua KIFO CHA KIROHO. Wewe upo kwenye barabara gani? Kuna baadhi ya vitu ambavyo mtu anapaswa kufanya kuhakikisha wapo kwenye njia nyembamba, mbali na hizi HAKUNA wokovu ni kifo tu. ***1 Yohana 5:12 "12Yeyote, aliye na Mwana wa Mungu anao uzima huo; asiye na Mwana wa Mungu, hana uzima."***

Ukweli ni rahisi; TUBU na UWACHANE NA DHAMBI ZOTE. Kisha ubatizwe. Kwa kupitia hiari yako na uwezo uliopewa na Mungu, kwa kutubu unakufa na Kristo na kusulubisha mwili "wako"; ***Wagalatia 2:20 "20na sasa naishi, lakini si mimi tena, bali Kristo anaishi ndani yangu. Maisha haya ninayoishi sasa naishi kwa imani, imani katika Mwana wa Mungu aliyenipenda hata akayatoa maisha yake kwa ajili yangu."*** Na moyo wako unafanya SAFI na imani yako ikijumuishwa na upendo. ***1 Petro 1:22-23 22Maadamu sasa, kwa kuutii ukweli, ninyi mmezitakasa roho zenu na kuwapenda wenzenu bila unafiki, basi, pendaneni kwa moyo wote. 23Maana kwa njia ya neno hai la Mungu, ninyi mmezaliwa upya, si kama watoto wa baba awezaye kufa, bali baba asiyekufa milele."***

Ushahidi wa imani inayookoa; ***Wagalatia 5:6 "6Maana ikiwa tumeungana na Kristo Yesu, kutahiriwa au kutotahiriwa hakuna maana; cha maana ni imani ifanyayo kazi kwa mapendo."***

Sasa UNAMTII MUNGU ukiwa umeoshwa kabisa kutoka uwovu na dhambi zote; ***Wagalatia 5:24-25 "*****24*****Wale walio wa Kristo wameisulubisha hali yao ya kidunia pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake.*** ***25Tukiishi kwa msaada wa Roho, na tuufuate mwongozo wake.*** ***26Basi, tusijivune, tusichokozane wala kuoneana wivu.."*** na kuweza kupokea kwa unyenyekevu neno LINALOWEZA KUOKOA ROHO YAKE. ***Warumi 6:4-6 "4Tulipobatizwa tuliungana na kifo chake, tukazikwa pamoja naye, ili kama vile Kristo alivyofufuliwa kutoka wafu kwa kitendo kitukufu cha Baba, sisi pia tuweze kuishi maisha mapya.*** ***5Maana, kama sisi tumeungana naye katika kufa kama yeye, vivyo hivyo tutaungana naye kwa kufufuliwa kutoka wafu kama yeye.*** ***6Tunajua kwamba utu wetu wa kale ulisulubiwa pamoja na Kristo, ili hali ya dhambi iharibiwe, tusiwe tena watumwa wa dhambi."*** Na; ***Yakobo 1:21-23 "21Kwa hiyo, tupilieni mbali mwenendo mchafu na tabia zote mbovu; jiwekeni chini ya Mungu na kupokea ule ujumbe uliopandwa mioyoni mwenu, ambao waweza kuziokoa nafsi zenu.*** ***22Msijidanganye wenyewe kwa kusikiliza tu neno lake, bali litekelezeni kwa vitendo.*** ***23Yeyote anayesikiliza hilo neno lakini halitekelezi, huyo ni kama mtu anayejiangalia sura yake mwenyewe katika kioo."***

Njoo kwa huzuni ukifuata Huruma ya Mungu, UKIWA UMEONDOLEWA dhambi zote kwa KUZIACHA ZOTE (dhambi za kale, si dhambi za siku zijazo); ***Warumi 3:25 "25Mungu alimtoa Yesu kusudi, kwa damu yake, awe njia ya kuwaondolea watu dhambi zao kwa imani yao kwake. Alifanya hivyo ili apate kuonyesha kwamba yeye ni mwadilifu. Hapo zamani Mungu alikuwa mvumilivu bila kuzijali dhambi za watu;"*** na kufidia

panapohitajika. Kwa tamaa kubwa moyoni KUMTII na juhudi na mapenzi mengi, bila hofu na kwa kuomba msamaha.

***2 Wakorintho 5:11-21 "11Basi, sisi tunajua umuhimu wa***
***kumcha Bwana, na hivyo tunajitahidi kuwavuta watu. Mungu***
***anatujua waziwazi, nami natumaini kwamba nanyi pia***
***mnatujua kinaganaga. 12Si kwamba tunajaribu tena***
***kujipendekeza kwenu, ila tunataka kuwapa ninyi sababu zetu***
***za kuona fahari juu yenu, ili mpate kuwajibu wale***
***wanaojivunia hali yao ya nje zaidi kuliko jinsi walivyo***
***moyoni. 13Ikiwa tumeonekana kuwa wendawazimu, hiyo ni kwa***
***ajili ya Mungu; na ikiwa tunazo akili zetu timamu, hiyo ni kwa***
***faida yenu. 14Maana mapendo ya Kristo yanatumiliki sisi***
***ambao tunatambua ya kwamba mtu mmoja tu amekufa kwa***
***ajili ya wote, na hiyo ina maana kwamba wote wanashiriki kifo***
***chake. 15Alikufa kwa ajili ya watu wote, ili wanaoishi wasiishi***
***kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa,***
***akafufuliwa kwa ajili yao.***

***16Basi, tangu sasa, sisi hatumpimi mtu yeyote kibinadamu.***
***Hata kama kwa wakati mmoja tulimpima Kristo kibinadamu,***
***sasa si hivyo tena. 17Mtu yeyote akiungana na Kristo huwa***
***kiumbe kipya, mambo ya kale yamepita, hali mpya***
***imefika. 18Yote ni kazi ya Mungu mwenye kutupatanisha sisi***
***naye kwa njia ya Kristo, akatupa nasi jukumu la***
***kuwapatanisha watu naye. 19Ndiyo kusema: Mungu, amekuwa***
***akiupatanisha ulimwengu naye kwa njia ya Kristo, bila kutia***
***maanani dhambi zao binadamu. Yeye ametupa ujumbe kuhusu***
***kuwapatanisha watu naye.***

***20Basi, sisi tunamwakilisha Kristo, naye Mungu mwenyewe anatutumia sisi kuwasihi ninyi. Tunawaombeni kwa niaba ya Kristo, mpatanishwe na Mungu. 21Kristo hakuwa na dhambi, lakini Mungu alimfanya ahusike na dhambi kwa ajili yetu, ili sisi kwa kuungana naye, tupate kuushiriki uadilifu wake Mungu."***

Huu ndio Muundo wa Ukombozi unaotumiwa kwenye Biblia; ***2 Wakorintho 7:10-11 "10Kuwa na huzuni jinsi atakavyo Mungu, husababisha badiliko la moyo, badiliko lenye kuleta wokovu; hivyo hakuna sababu ya kujuta. Lakini huzuni ya kidunia huleta kifo. 11Sasa mnaweza kuona matokeo ya kuona huzuni jinsi Mungu atakavyo: ninyi mmepata kuwa sasa watu wenye jitihada, wenye hoja, mnashtuka na kuogopa, mna bidii na mko tayari kuona kwamba haki yatekelezwa. Ninyi mmethibitisha kwa kila njia kwamba hamna hatia kuhusu jambo hili."***

Kwa hivyo MAANA YA KWELI YA UKOMBOZI WA KIBIBLIA NI: **Kutolewa utumwani kwa malipo ya gharama kubwa.**

***Matayo 20:28 "28Jinsi hiyohiyo, Mwana wa Mtu hakuja kutumikiwa, bali kutumikia na kutoa maisha yake kuwa fidia ya watu wengi."***

***1 Timotheo 2:5-6 "5Maana yuko Mungu mmoja, na pia yuko mmoja anayewapatanisha watu na Mungu, binadamu Kristo Yesu, 6ambaye alijitoa mwenyewe kuwakomboa watu wote. Huo ulikuwa uthibitisho, wakati ufaao ulipowadia."***

Alichokifanya Yesu msalabani HAIKUWA kuchukua nafasi ya mtu yeyote, LAKINI kujitoa binafis kama SADAKA YA DHAMBI; ***(Waebrania 9:14 "14Lakini, kwa damu ya Kristo, mambo makuu zaidi hufanyika! Kwa nguvu za Roho wa milele, Kristo ALIJITOLEA MWENYEWE dhabihu kamilifu kwa Mungu. Damu yake itatutakasa dhamiri zetu kutokana na matendo yaletayo kifo, ili tupate kumtumikia Mungu aliye hai."*** kufidia binadamu na kumtoa kwenye giza na kumwelekeza kwenye Mwangaza, kutoka kwa nguvu ya Shetabi hadi ya Mungu***; Matendo ya Mitume 26:18 "18Utayafumbua macho yao na kuwawezesha watoke gizani na kuingia katika mwanga; watoke katika utawala wa Shetani, wamgeukie Mungu; ili kwa kuamini, wapate kusamehewa dhambi na kuchukua nafasi yao kati ya wale ambao wamepata kuwa watu wa Mungu."***

Kwa hivyo "kazi" za SHETANI ZINAHARIBIWA na binadamu anaweza kurudishwa katika moyo imara***. 1 Yohana 3:7-8 "7Basi, watoto wangu, msikubali kupotoshwa na mtu yeyote. Mtu atendaye matendo maadilifu ni mwadilifu kama vile Kristo alivyo mwadilifu kabisa. 8Lakini atendaye dhambi ni wa Ibilisi, maana Ibilisi ametenda dhambi tangu mwanzo. Lakini Mwana wa Mungu alikuja duniani kuiharibu kazi ya Ibilisi."***

Sasa Biblia inaeleweka! **MATENDO (KAZI / MATUNDA / KUTII SHERIA ZAKE)** yatakuwa ndiyo viamuzi kwa tamati katika wokovu wako wa mwisho, ila si "imani" yako katika uwongo.

***Warumi 2:7-11 "7Wale wanaozingatia kutenda mema, kutafuta utukufu na heshima ya Mungu na kutokufa, watapata uzima***

***wa milele. 8Lakini wale wengine wenye ubinafsi, wenye kukataa mambo ya haki na kufuata uovu, wataangukiwa na ghadhabu na hasira ya Mungu. 9Mateso na maumivu yatampata binadamu yeyote atendaye uovu. Yatawapata Wayahudi kwanza, na watu wa mataifa mengine pia. 10Lakini Mungu atawapa utukufu, heshima na amani wale wanaotenda mema; Wayahudi kwanza, na watu wa mataifa mengine pia. 11Maana Mungu hambagui mtu yeyote."***

***1 Petro 1:17 "17Mnapomtaja Mungu ninyi humwita Baba. Basi, jueni kwamba yeye humhukumu kila mmoja kadiri ya matendo yake, bila ubaguzi. Hivyo tumieni wakati wenu uliowabakia hapa ugenini katika kumcha Mungu."***

Wakristo wanaokiri leo wanaamini "kila kitu" ila Ukweli kwa sababu wengi wao HAWAJAWAHI dhihirikiwa na ukweli, na inawezekana sana kuwa wanachokifanya tu ni kujificha tu kutoka kwa ukweli huu. Ni hali inayohuzunisha kuwa mifumo yao ya imani ina mazoea ya kunyamazisha dhamira yao kwa NGUVU YA HUKUMU ya roho mtakatifu. Kwa hivyo, wanapousikia ukweli, hauwakati hadi moyoni; ***Matendo ya Mitume 2:37 "37Basi, watu waliposikia hayo, walichomwa moyo, wakawauliza Petro na wale mitume wenzake: "Ndugu zetu, tufanye nini?"*** kwa hivyo wanahimizwa kutubu. Mtu anaposhawishika kuwa baadhi ya mafundisho ni kweli, ni vigumu kuwashawishi vinginevyo. ***2 Wathesalonike 2:11-12 "11Ndiyo maana Mungu amewaweka chini ya nguvu ya upotovu, wauamini uongo. 12Matokeo yake ni kwamba wote wasioamini ukweli, ila wafurahia dhambi, watahukumiwa."***

Kwao Biblia inaunga mkono uongo wao na kuwasamehe kutoka **kutotii kwao.** Kwa sababu **"Muundo huu Mbadala"** hutoa kisingizio BORA ZAIDI cha dhambi, NAFASI kubwa wengi wataepuka mnato wake na kuona Mwangaza kabla ya wakati wao kuisha. Ikiwa unamwamini Mungu na unaamini kuwa Yesu ni Mwokozi UNAYEHITAJI elewa hili. Msingi unaosimamia unafaakuwa umeimarishwa kwenye Ukweli. Usitegemee mtu mwingine akuchimbie msingi. ***Luka 6:46-49 "46Mbona mwaniita Bwana, Bwana, na huku hamtimizi yale ninayosema? 47Nitawapeni mfano unaofaa kuonyesha alivyo yeyote yule anayekuja kwangu, akasikia maneno yangu na kuyatimiza: 48Huyo anafanana na mtu ajengaye nyumba, ambaye amechimba chini na kuweka msingi wake juu ya mwamba; kukatokea mafuriko ya mto, mkondo wa maji ukaipiga nyumba ile, lakini haukuweza kuitikisa, kwa sababu ilikuwa imejengwa imara. 49Lakini yeyote anayesikia maneno yangu lakini asifanye chochote, huyo anafanana na mtu aliyejenga nyumba juu ya udongo, bila msingi. Mafuriko ya mto yakatokea, mkondo wa maji ukaipiga nyumba ile, ikaanguka na kuharibika kabisa!"***

CHAGUA BARABARA SAHIHI NA UKUMBUKE **DHAMBI NI CHAGUO,** SI UGONJWA TUNAORIDHI AU TULIZALIWA KATIKA. Tubu kwanza; ***Isaya 55:7 "7Mtu mwovu na aiache njia yake na mtu mbaya na ayaache mawazo yake. Yeye na amrudie BWANA, naye atamrehemu,***
***arudi kwa Mungu wetu, kwa kuwa atamsamehe bure kabisa.."***

***Matendo ya Mitume 3:19 "19Tubuni basi mkamgeukie Mungu, ili dhambi zenu zifutwe, ili zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwepo kwake Bwana."***

Tafuta huruma YAKE, na UZALIWE TENA! Ni lazima ufe mara ya kwanza kwa dhmabi na uzaliwe tena. ***Yohana 3:3 "3Yesu akamjibu, "Amin, amin nakuambia, mtu hawezi kuuona Ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili."***

Roho Mtakatifu sasa anaweza kukaa ndani yako na kutoa matunda mazuri na kukuelekeza katika utakatifu na UKWELI. ***Waefeso 5:18 "18Pia msilewe kwa mvinyo, ambamo ndani yake mna upotovu, bali mjazwe Roho."***

Sasa, MWOGOPE MUNGU, weka tumaini lake katika huruma yake kuu, na uachane na mambo yote ya dunia na umtumikie hadi tamati. Baada ya kutubu kwa kweli, batizwa kama ishara ya kusafishwa. Mafunzo kamili pamoja na video ya ubatizo inaweza kupatikana hapa **(eternalevangelism.com/how-to-baptize).** Ubatizo kwa wanaokosa kutubu (wanaokosa kukiri NA kuachana na dhambi) haina maana ila tu hufanya mtu kuwa "mtenda dhambi aliyelowa maji". Unajidai tu kuwa umetubu, mwanafunzi mtiifu wa Kristo na unakosa kufuata amri yake ya kubatizwa ***(tazama Matendo ya Mitume 2:38, 1 Petro 3:21, n.k,).*** Hiki ni kipengele muhimu cha kuanza kufuatilizia toba ya kweli; ila ikiwa mtu bado anatenda dhambi na hafuati hafuati vipengele vyote vinavyofaa ilhali ni lazima wawe watiifu kwa neno la Mungu, basi ubatizo peke yake huna maana. Usiamini walimu waongo wa "neema kubwa" wanaokwambia kuwa unachohitaji kufanya tu ni kuomba

"ombi la watenda dhambi" ili "uokoke" na usiamini wazushi wa "urejeshaji kwa ubatizo" wanaofunza kuwa tendo la kubatizwa "huokoa" roho ya mtu. Ni lazima uubebe msalaba wako **(Upendo wa Mungu una masharti)** na unavumilia hadi wokovu wa mwisho, aangukapo ataangamia.

Je uko tayari kuchukiwa na dunia lakini upendwe na Mungu?

***Matayo 10:22 "22Nanyi mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya Jina langu. Lakini yeye atakayevumilia hadi mwisho ataokoka."***

***Yohana 15:19 " 19Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungeliwapenda kama vile unavyowapenda walio wake. Kwa sababu ninyi si wa ulimwengu, lakini mimi nimewachagua kutoka katika ulimwengu, hii ndiyo sababu ULIMWENGU UNAWACHUKIA."***

Kumalizia, ni lazima utubu, uishi maisha ya utakatifu na ukamilifu wa kibiblia kwa Mungu (Yesu) wa kweli mmoja unapopumua huku duniani. Yesu "hatakufunika" kutokana na dhambi ulizofanya kihiari haijalishi kiasi unachosema kuwa "unamwamini". Ikiwa unahitaji, na wengi wanahitaji, ninaomba utubu kwa kweli na umfuate Yesu, ninaomba kwa kweli. Nipo hapa kila wakati kuzungumza na wanaotafuta Ukweli kwa hakika. Hakuna tumaini kamwe baada ya kupumua pumzi yako ya mwisho. Chagua UHAI, si kifo. Utukufu wote uwe kwa Yesu. AMINA

*Waebrania 9:27 "27Kama vile mwanadamu alivyowekewa kufa mara moja tu na baada ya kufa akabili hukumu,"*

**Mimi ndiye mwanzilishi na msimamizi wa Misheni ya Kiulimwengu kwa Watoto (Global Mission for Children). Hii ni huduma ya Kikristo pamoja na wamishenari wa kale walio katika Ulimwengu wa Tatu. Vilevile ninasimamia Ushirikiano wa Wenye Imani Tendaji (Working Faith Fellowship) ambazo ni kanisa katika kila nyaja za umisheni. Tovuti za kila uwanja wa umisheni umeorodheshwa hapa chini. Ungana nasi katika kuwasaidia ndugu wapendwa waliokatika mstari wa mbele kila siku. Utukufu wote kwa Yesu.**
**- James Joseph Miller, Jr.**

**Makazi duni ya Kibera, (Nairobi) Kenya**

**kibera.WorkingFaithFellowship.com**

**Bangladesh**
**bangladesh.WorkingFaithFellowship.com**

**Moi's Bridge, (Magharibi) Kenya**
**moisbridge.WorkingFaithFellowship.com**

**Moyale, (Kaskazini) Kenya & (Kusini) Ethiopia**
**moyale.WorkingFaithFellowship.com**

**Misheni ya Kiulimwengu kwa Watoto tovuti**
**globalmissionforchildren.org**

**Tovuti yangu ya mafundisho**
**eternalevangelism.com**

**Unaweza kunifikia katika**
**jmiller@globalmissionforchildren.org**

I wrote this book for a few reasons, two of them being I learned how to truly love and I am commanded to share it. I do this with great joy. I used to believe that love was accepting everyone just as they are. This is the "unconditional love" the world teaches, sadly to it's destruction. I met a Man back on January 16th, 2006 and His name is Jesus. My life has never been the same. I hope you join me as I not only share my miraculous story, but I pray you receive this true love also. It's completely free in that you can't earn it, yet, it will cost you "everything". Come meet the One True God that freely gives life eternal to His faithful, obedient children who abide in Him.

